

**Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Tisa - Tarehe 14 Novemba, 2003**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. THOMAS S. NYIMBO (k.n.y. MHE. PIUS MSEKWA - MWENYEKITI WA TUME YA HUDUMA ZA BUNGE):**

Taarifa ya Utendaji na Hesabu za Tume ya Huduma za Bunge kwa kipindi cha mwaka 2002/2003.

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwulizaji wa kwanza, naomba kuwataarifu kwamba maswali yote yaliyobaki kipindi hiki yamo humu ndani. Kwa hiyo, leo yako mengi kuliko ilivyo kawaida. Kwa hiyo, naomba mzingatie hilo na kuyamaliza. Haya, swali la kwanza Mheshimiwa Aridi Uledi.

Na.115

**Upungufu wa Wafanyakazi Kituo cha Afya cha Michiga**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Michiga kinakabiliwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi, ukosefu wa vifaa na samani mbalimbali:-

(a) Je, ni lini Kituo hicho kitapatiwa wafanyakazi wa kutosha?

(b) Je, ni lini Kituo hicho kitapatiwa umeme, vifaa pamoja na samani mbalimbali zinazohitajika?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwananche Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara inatekeleza mchakato wa hatua 17 za maboresho katika awamu ya pili ya programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa kwa nia ya kuinua ubora wa huduma zinazotolewa ikiwa ni pamoja na Sekta ya Afya. Uchambuzi wa watumishi, vifaa na samani umefanywa na kwa mujibu wa taarifa zilizopo Kituo cha Afya cha Michiga kina jumla ya watumishi wanane na upungufu wa watumishi wanne ambao ni *Assistant Medical Officer, Clinical Officer, Maternal and Child Health Aider* na *Pharmaceutical Assistant*.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu uliopo ni mdogo ukilinganishwa na Vituo vingine nchini. Zoezi la kujaza nafasi zote kwa mujibu wa ikama na muundo mpya wa Halmashauri limeendelea kufanywa ikiwa ni pamoja na Serikali kuidhinisha nafasi 34 za ajira ya watumishi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa mwaka 2003/2004. Aidha, kibali cha ajira ya watumishi hao ikiwa ni pamoja na wa Kituo cha Afya cha Michiga kimeombwa toka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma kwa barua Na. *MDC/S.20/1/VOL.III/63* ya tarehe 31 Julai, 2003 na barua Kumb.Na. *MDC/S.20/1/VOL.III/85* ya tarehe 16 Oktoba, 2003.

Halmashauri inaendelea kufuatilia na kuhakikisha kuwa kipaumbele kinawekwa katika Sekta ya Afya kikiwemo Kituo cha Afya cha Michiga.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa sasa haina mpango wa kupeleka umeme katika Kituo cha Afya cha Michiga. Juhudi za Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa kiasi kikubwa zinategemea sana mpango wa Shirika la Ugavi wa Umeme nchini (*TANESCO*) wa kusambaza umeme katika Wilaya hiyo. Hata hivyo, Kituo cha Afya cha Michiga na vingine, kila mwezi hupata mgao wa mafuta ya taa kwa ajili ya kuchemsha vifaa mbalimbali na pia kutolea huduma nyingine wakati wa usiku kwa kutumia taa za kandili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhaba wa vifaa muhimu na samani za Kituo hicho, Halmashauri inatarajia kulishughulikia tatizo hilo katika bajeti ya mwaka

2004/2005. Serikali itaendelea kushirikiana na Halmashauri na Wananchi kwa ujumla kuhakikisha kuwa huduma katika Kituo cha Afya cha Michiga zinaboreshwa.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili yafuatayo:-

Kwa kuwa tatizo mojawapo sugu ni la ukosefu wa umeme na kwa kuwa kwenye jibu imeelezwa kuwa umeme wa *TANESCO* haupatikani; je, Serikali itakuwa tayari kukipatia Kituo cha Afya Michiga angalau umeme wa *solar* ili kusaidia kuweka majengo safi kutokana na kuchafuka kwa matumizi ya vibatari na taa za kandili? (*Makofi*)

Pili, kwa kuwa tatizo lingine sugu ni ukosefu wa maji, je, Serikali itakipatia Kituo cha Afya cha Michiga kisima cha maji cha kuaminika ili kihudumie wafanyakazi na wagonjwa Kituoni hapo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi ni kwamba suala la umeme si suala rahisi kwa hivi sasa kufanyika kwa Kituo kimoja tu au katika Tarafa moja. Kuna mradi wa Kitaifa ambao ni lazima umeme usambae nchi nzima.

Kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Mbunge awaeleze wananchi kwamba si jambo la kufanya upendeleo, lakini shughuli ya umeme, kila Wilaya ambayo haina umeme Wizara ya Nishati na Madini inalishughulikia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge afanye subira, awaambie ukweli wananchi kwamba umeme hautapatikana hivi sasa, lakini imo katika maandalizi. (*Makofi*)

Kuhusu maji, kama nilivyosema kuhusu umeme, si rahisi kuleta mradi wa Kitaifa mara moja. Lakini mimi naomba kuishauri Serikali ya Wilaya na pia Serikali ya Halmashauri na wananchi, mkae mlizungumze hili suala namna ya kupata maji kwa kupitia kisima. Lakini mkihamasishana, Serikali itawaunga mkono ili tuanze kutatua tatizo hilo wakati Serikali Kuu inafanya taratibu nyingine.

Na.116

### **Ujenzi wa Kituo Kikubwa cha Afya Mbuyuni**

**MHE. NJELU E.M. KASAKA (k.n.y. MHE. PAUL E. NTWINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya Mbuyuni ni Kituo pekee Jimboni Songwe kinachohudumia Kata zaidi ya sita na kwa kuwa Kituo hicho hakina usafiri wa uhakika wa kwenda Hospitali ya Wilaya Mwambani au Chunya Mjini ambako ni mbali na kwa kuwa Kata nne za Udinde, Kapalala, Gua na Ngwara zipo mbali na Kituo cha Afya Mbuyuni:-

Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kujenga Kituo kikubwa cha Afya kwenye eneo hilo na pia kuimarisha Zahanati zilizopo kwa kuzipatia Waganga, Wahudumu na madawa ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ina Vituo vitatu vya Afya ambavyo ni Mbuyuni, Chunya Mjini na Mtanila ambavyo vinahudumia wastani wa watu 260,615 kulingana na sensa ya mwaka 2002. Kituo cha Afya cha Mbuyuni kilichopo Tarafa ya Songwe kinahudumia watu wanaokadiriwa kufikia 61,073 katika Kata tano zenye Zahanati saba pamoja na Kituo cha Afya cha Mbuyuni. Zahanati hizo ni Kanga, Tete, Ifwenkenya, Galula, Magamba, Totowe na Namkukwe. Katika kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Chunya, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la *DFID* (Mradi wa Afya ya familia) ilijenga Zahanati katika Kata ya Kapalala ili kuwapunguzia kero wananchi waliokuwa wanategemea kwa kiasi kikubwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Mwambani.

Aidha, mwaka 2001/2002 ilifanya ukarabati wa Kituo cha Afya cha Mbuyuni kwa gharama ya shilingi 3,000,000/=, kwa kufanya kazi ya kuondoa *ceiling board* zilizooza na kubadilisha nyingine, kuezua mabati yaliyooza na kurudishia mengine na kuondoa kuta zilizoposuka na kujenga upya sehemu ya kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za Afya katika Wilaya, Watumishi wa Kata ya Tabibu, Wakunga na Wahudumu wa Afya wamepangwa kwa uwiano wa kutosha katika Zahanati. Hivi sasa gari la kuhudumia wagonjwa (*Ambulance*) aina ya *Toyota Land Cruiser - Hardtop* Na. SM 3957 lenye thamani ya shilingi 32,352,699/= limenunuliwa kupitia msaada wa Wahisani wa Shirika la Kimataifa la kuhudumia watoto (*UNICEF*) na limefika Wilayani Chunya kuanzia tarehe 10 Novemba, 2003 tayari kwa kupelekwa Kituo cha Afya cha Mbuyuni. Kutokana na jitihada hizi, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya haina mpango wa kujenga Kituo kikubwa cha Afya Mbuyuni hivi sasa bali kinachofanyika ni kuimarisha huduma zilizopo.

Lakini kama wanaona umuhimu wa kukipanua Kituo hicho kiwe Hospitali, basi ninamshauri Mheshimiwa Mbunge wakakae katika Vikao vya Serikali Kuu Wilayani na Halmashauri wakishirikiana na wananchi kuanza ujenzi huo kwa kutumia vigezo vya idadi ya watu, magonjwa yanayojitokeza na umbali wa maeneo.

**MHE. NJELU E.M. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza na pia namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Nataka niulize kwamba swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, alitaka kujua ujenzi wa Kituo cha Afya katika eneo la Kapalala, siyo kupanua Kituo cha Mbuyuni. Ni eneo la Kapalala ambalo liko mbali kutoka Kituo hicho. Je, ni mpango gani uliopo wa kuhakikisha kwamba katika eneo la Kapalala ambako kunjumuisha Kata za Ngwara na Gua, Kituo cha Afya kitajengwa? Hilo la kwanza.

La pili, nashukuru kwamba gari limepatikana kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mbuyuni pamoja na hapo nyuma lilipatikana gari kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Mtanila, lakini tatizo tulilonalo ni upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mafuta ili kuendesha shughuli zake kwa kusafirisha wagonjwa kuwapeleka kwenye Hospitali.

Je, utaratibu wa Serikali ukoje wa kuvipatia Vituo hivi fedha za kutosha ili waweze kuwa na diesel ya kutosha wakati wote wagonjwa wanapopatikana?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Paul Ntwina, alikuwa na tatizo kwamba Kituo cha Kapalala kinahitaji Kituo cha Afya, basi kama nilivyosema katika jibu la Msingi, ni kukaa katika uongozi wa Serikali Kuu, Tawala za Mikoa na wananchi kuanza mikakati ya ujenzi wa hicho Kituo, nina hakika Serikali itaona umuhimu kama nilivyosema kwamba kujenga Kituo cha Afya kunategemea umbali wa Kijiji na Kijiji ili wananchi wasipate taabu na pia kunategemea wingi wa watu na pia kunategemea magonjwa kama nilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna magonjwa mengi na wananchi ni wengi wako pale wanahitaji huduma na usafiri unakuwa wa matatizo, basi ianzie kwenu, halafu Serikali nina hakika italipokea na kuona jinsi gani ya kuweza kusaidia.

Kuhusu magari, kwanza mshukuru kupata gari. Sasa itakuwa kwamba baada ya kula wewe unasema mjomba je! Shangazi je! Lakini kwanza kitu muhimu kilichopatikana ni gari. Kuhusu mafuta, Serikali Kuu sidhani kama inaweza kugharamia ili kuendesha hiyo gari.

Kwa hiyo, bado nasema mrudi katika Halmashauri mwone mafungu gani katika Kamati za Fedha ambayo yanaweza kuwa yanatoka kwa ajili ya kutoa huduma katika magari haya mliyopewa. Kwa hiyo, mshukuru kwanza kupata gari, kabla ya kuomba mafuta. Nashukuru. *(Makofi)*

Na.117

### **Wafanyakazi wa Kiwanda cha Zana za Kilimo - Mbeya**

**MHE. YETE S. MWALYEGO (k.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Zana za Kilimo - Mbeya mpaka sasa hawajalipwa mapunjo ya malipo ya kuachishwa kazi licha ya ahadi iliyowahi kutolewa na Makamu wa Rais mwaka 1999 alipokitembelea kiwanda hivyo:-

- (a) Je, ni lini wafanyakazi wa kiwanda hicho watalipwa mapunjo hayo?
- (b) Kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi wanafukuzwa kwenye nyumba za Shirika hilo, je, isingekuwa busara kwa Serikali kuharakisha malipo yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi sasa Serikali imetumia jumla ya shilingi milioni 120.6 kulipa gharama za mafao ya kisheria ya wafanyakazi pamoja na mapunjo yaliyojitokeza baada ya kuhakikiwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

- Mafao kwa wafanyakazi 117 ni kiasi cha shilingi 54,500,000/=
- Malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi 84 walioachishwa kazi ni kiasi cha shilingi 9,746,735. Kiasi hiki kinajumuisha mapungu ya nauli na mizigo pamoja na mishahara ambayo baadhi ya wafanyakazi hawakulipwa katika kipindi cha Juni, 1997 na Mei, 1998.
- Malipo ya mafao kwa wafanyakazi 38 waliopunguzwa awamu ya pili ni kiasi cha shilingi milioni 15.6.
- Mafao ya wafanyakazi waliosahaulika ni kiasi cha shilingi milioni 2.4;
- Mafao ya wafanyakazi 14 waliobakizwa kiwandani ni kiasi cha shilingi milioni 6.6.
- Katika Bajeti ya Septemba hadi Desemba, 1998 gharama za umeme zililipiwa shilingi milioni 5.2. Gharama za mtaji kwa ajili ya uzalishaji mdogo uliolenga kulipa wafanyakazi waliobakizwa kiwandani ni kiasi cha shilingi milioni 1.73 na gharama za *PPF* ni kiasi cha shilingi milioni 24.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Tume iliunda Kamati ndogo ya wataalamu mwezi Agosti, 1999 iliyojumuisha Wajumbe kutoka Mipango na Ubinafsishaji, Viwanda na Biashara na *NDC* kama Shirika Mama ili kuhakiki matumizi ya fedha zilizotolewa na

Serikali baada ya mwakilishi wa wafanyakazi walioachishwa kazi kuwasilisha malalamiko yao katika Ofisi ya Rais na Ofisi ya Makamu wa Rais wakilalamikia matumizi mabaya ya fedha hizo. Taarifa ya Kamati ilibainisha kuwa fedha zilitolewa zilitumika kama zilvyokusudiwa na hivyo kmalalamiko ya wafanyakazi hayakuwa ya msingi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Zana za Kilimo - Mbeya walilipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria na mapunjo yaliyojitokeza baada ya malipo ya awali walilipwa. Hivyo wanatakiwa kuhama kutoka kwenye nyumba za Kiwanda walizopewa wakati wa utumishi wao. Kisheria utumishi wao ulikoma pale walipopewa barua za kuachishwa kazi na kulipwa mafao yao. Kwa hivi sasa kiwanda cha Zana za Kilimo kipo chini ya mfilisi *LART*.

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili.

Kwa kuwa wafanyakazi bado wanalalamika kwamba kuna mapunjo, je, Waziri haoni ni busara mkaunda Tume nyingine tofauti na ile ya mwanzo ili muwe na uhakika kwamba mmefanya haki?

Pili, je, kuna mipango gani ya Kiwanda hiki kukibinafsisha kwa sababu naona kwenye list hakipo? Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama wafanyakazi hawa bado wanalalamika kwa maana ya kupunjwa malipo yao, tutaangalia utaratibu wa kuhakiki tena kuona kwamba mapunjo hayo yametokana na nini. Lakini mara nyingi wafanyakazi hawa wanapolipwa malipo hayo, mara fedha zile zinapokwisha, hujitokeza tena na kutoa sababu nyingine kwamba bado wamepunjwa. Kwa hiyo, hilo tutaliangalia na tuone ukweli wake.

Pili, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mwalyego kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa sana sasa ya kuamsha viwanda vyetu hivi vya zana za kilimo tukianza na *UFI* na hiki cha Mbeya. Kwa hiyo, hiyo ni moja ya eneo ambalo liko katika mikakati wa Serikali. (*Makofi*)

Na.118

### **Matumizi ya *Waterguard***

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi wake maji safi na salama na ya kutosha na kuhakikisha kwamba maji hayo hayana madini au wadudu hatari kwa afya za binadamu na kwa kuwa Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) limetoa hati ya ubora na ruhusa ya kutumia dawa iitwayo *Waterguard* ili kuwahakikishia wananchi usalama wa maji wanayotumia:-

(a) Je, dawa hiyo ina kemikali na antiseptic gani zinazofanya maji kuwa salama?

(b) Je, dawa hiyo imefanyiwa uchunguzi gani wa kikemia na ki-microbiojia (*Chemical and Microbiological Tests*) ambazo majibu yake yanahalalisha madai kwamba maji yanakuwa salama yakiwekewa dawa hiyo?

(c) Je, Serikali haioni hatari ya mwananchi wa kawaida kuachana na mambo sahihi na ya msingi kama kuchemsha maji kwa kuamini kwamba dawa hiyo ndiyo jibu kwa maradhi yanayotokana na maji?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

(a) Dawa inayotumika katika Waterguard ni *Sodium Hypochlorite* na jina la *Waterguard* ni la kibiashara tu. Dawa hii siyo tofauti na ile inayotumika kusafisha maji ya bomba kwani kinachotumika kuulia vijidudu ni *chlorine* ambayo kiwango kinachotumika kinatakiwa kisizidi kiasi fulani. Kipimo maalum cha matumizi huifanya dawa yenyewe isizidi kiasi kinachokubalika kiafya. Katika misingi hii, *TBS* walitoa maelekezo kwa mtengenezaji kuonesha kiasi cha matumizi ya dawa kwa maji ya bomba, mito na maziwa.

(b) Uchunguzi wa kitaalam kwa mara ya kwanza ulifanywa na *TBS* mwezi Februari, 2003 ili kuona uwezo wa dawa ya *Sodium hypochlorite* kuua vijidudu ndani ya maji. Uchunguzi huu ulizingatia kiwango yaani standard cha Kampuni inayotengeneza dawa ya *Waterguard*.

Aidha, mwezi Juni, 2003, *TBS* kwa maelekezo ya Wizara na kwa kushirikisha Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali iifanya uchunguzi wa pili. Katika uchunguzi huu, kilichozingatiwa ni kiwango kinachokubalika na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo cha kati ya 5 -10 g/l. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kwamba dawa ya *Waterguard* ina uwezo wa kuua vijidudua na kiasi cha *chlorine* katika dawa hiyo ni 7.5 g/l ambayo inakubaliana na matakwa ya kiwango cha 5 -10 g/l.

(c) Dawa ya *Sodium hypochlorite* ingawa inafanya kazi ikitumiwa kwa usahihi, njia rahisi ambayo mwananchi anaweza kuimudu ni kuchemsha maji. Hivyo, suala la elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuchemsha maji linaendelea kusisitizwa. Aidha, *TBS* wametakiwa kufanya uchunguzi wa dawa ya *Waterguard* mara kwa mara ili kuhakikisha mtengenezaji hakiuki masharti ya viwango.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali moja dogo la nyongeza na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake. Nilitaka tu kuuliza kwamba kukosekana kwa umakini



katika kuratibu matangazo kama hayo, je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba mwananchi ataendelea kuwa mteja wa maradhi kama kipindupindu kama hatutakuwa makini? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kama hatuwezi kufuatilia vizuri matangazo ya biashara yanaweza kupotosha wananchi. Lakini muhimu kabisa ni ya kwamba hayo matangazo ya biashara yanafuatiliwa vizuri na Idara inayohusika yaani Taasisi ya *TBS* na pale ambapo wanakiuka hatua sahihi huchukuliwa. Lakini vile vile ni muhimu kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba kuhusu maji, dawa nzuri zaidi ni kuchemsha. Tukichemsha maji yetu ya kunywa tutakuwa tunajikinga zaidi kuliko kuzingatia tu matangazo ya biashara, kwa sababu mwenye biashara ana haki ya kutangaza biashara yake na hatuwezi kumzuia. Ahsante. (*Makofi*)

Na.119

### **Wawekezaji wa Madini**

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna tetesi za wawekezaji katika Sekta ya Madini kuwekeza katika Jimbo la Mwibara:-

(a) Je, ni Makampuni mangapi na ni madini yapi yaliyokwishapata kibali cha kufanya utafiti au kuchimba madini kwenye Jimbo la Mwibara?

(b) Je, ni lini Serikali itawekeana mikataba na Kampuni hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kuna Kampuni tano za madini zenye leseni ya utafiti katika Jimbo la Mwibara. Kampuni hizo ni *Empire Gold Limited*, *African Queen Mining Company Limited*, *Lakota Resources (T) Limited*, *Eb-Hance Company Limited* na *Letubi Mining Limited*.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna Kampuni ambayo imeshapata matokeo mazuri ya utafiti ili kuwezesha uchimbaji kuanza. Aidha, Serikali haijawekeana Mkataba na Kampuni yoyote katika hizi.

Hata hivyo ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba siyo kila Kampuni yenye leseni ya uchimbaji wa madini inawekeana Mkataba na Serikali kwani baadhi zinaridhika na masharti ya jumla yaliyopo kwenye Sheria ya Madini ya 1998 na mfumo wa kodi ambao unatumika kwa Kampuni zote.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wanasema kwamba ikiwa madini tuliyonayo nchini Tanzania yatauzwa kwa umakini, faida yake tu inaweza kuwajengea Watanzania wote nyumba za *self container* pamoja na kutengeneza miundombinu ya barabara bila kutegemea misaada kutoka nje, je, Serikali inasemaje kwa hilo? (*Kicheko/Makofi*)

Pili, ikiwa kutatokea tunayo madini, wananchi wa Jimbo la Mwibara wanakuombeni Serikali kabla wawekezaji kutoka nje kuingia mikataba na nyie wanaomba umiliki wa ubia kati ya Kijiji chenye madini au wananchi walioko katika maeneo hayo, hivyo basi wananchi walioko katika maeneo hayo waingie ubia na hao wawekezaji. Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kweli madini yanachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa na ndiyo maana Serikali imeweka sera nzuri ya madini, sheria nzuri ya madini na taratibu za madini ya uendeshaji wa shughuli za madini kuhakikisha kwamba Taifa letu linafaidika na uchimbaji huu wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala ambalo linaboreshwa wakati hadi wakati na tulikuwepo wote katika semina ya wiki iliyopita hapa na Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kutoa michango yao namna ya kuboresha uchimbaji wa madini ili uwe na manufaa zaidi kwa Taifa. Ni jambo ambalo Serikali ilishaahidi kwamba inalifanyia kazi kuhakikisha kwamba tunafaidika zaidi. Kuhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge, mimi nadhani kwa sababu hilo ni ombi, tuseme tu kwamba Serikali imesikia ombi hilo na labda baadaye Mheshimiwa Mbunge anaweza kutaka kulileta hilo katika njia ambazo zinafahamika zaidi ili tuweze kuona namna gani linaweza likashughulikiwa.

Na.120

### **Mikakati ya Kuwaendeleza Vijana**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshaona umuhimu wa vijana kuwa ni nguvukazi ya Taifa ndiyo maana imepanga mikakati mingi ya kuwaendeleza vijana kiuchumi na kwa kuwa moja kati ya mikakati hiyo ni pamoja na mikakati ya kuwawezesha vijana kujajiri wenyewe kupitia Sekta ya Kilimo kwa asilimia 70 na kwa kuwa katika hali ya kujajiri wenyewe kupitia Sekta hiyo ya Kilimo inaonekana kutowavutia vijana wengi ndiyo maana wanakimbilia Mijini kwa sababu hakuna uwezekano wa kupata mikopo, uhakika wa upatikanaji wa maji kwa mwaka mzima, kukosekana kwa masoko ya uhakika, mawasiliano duni, miundombinu ya barabara, mikakati ya burudani na kadhalika:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki vijana walioanzisha biashara Mijini na kuwataka warudi Vijijini wakalime, pasipo kurekebisha kasoro zilizotajwa hapo juu?

(b) Je, Serikali inasema nini kwa baadhi ya viongozi wanaowafukuza vijana waliokwisha kujajiri kibiashara na kuwapa maeneo ya kilimo bila maandalizi?

(c) Kwa kuwa uchumi mzuri unategemea nguvukazi ya vijana, je, kwa nini vijana wananyanyasika kiuchumi na hivyo kushindwa kutumia nguvukazi hiyo kuendeleza uchumi au kiuchumi?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa vijana kuwa ni nguvukazi ya Taifa, kupitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, Serikali imeandaa mikakati na programu mbalimbali zitakazowawezesha vijana kuboresha maisha yao ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Serikali haitamki wala kuwataka vijana walioanzisha biashara mijini warudi vijijini. Serikali inachofanya ni kuwaelimisha vijana wasio na ajira wajajiri katika sekta mbalimbali ikiwemo kilimo.

Aidha, Serikali itaendelea kuboresha shughuli za kilimo ili ziweze kuwaletea manufaa zaidi wakulima wakiwemo vijana. Msisitizo wa Serikali ni kuwataka vijana watumie raslimali zinazoweza kupatikana pale walipo katika kukuza ajira, kipato na kadhalika.

(b) Serikali inamini kuwa si haki kuwafukuza vijana waliokwishajajiri kibiashara kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Ni matumaini ya Serikali kuona kwamba, hata vijana wanaopewa maeneo kwa ajili ya kilimo maandalizi ya msingi yanakuwepo.

(c) Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, Serikali na wadau mbalimbali wameweka mazingira yanayowawezesha vijana kujikomboa kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na uimarishaji wa vikundi vya vijana vya kuzalisha mali, kuimarisha mfuko wa Maendeleo ya Vijana (*National Youth Revolving Fund*), kutenga 10% ya mapato ya kila Wilaya kwa maendeleo ya vijana na wanawake na kuimarisha Idara ya Vijana kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Taifa.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana sana Waziri na Serikali kwa majibu mazuri na vijana wameyasikia haya. (*Makofi*)

Nina swali moja la nyongeza. Je, pale inapotokea vijana hawa wananyanyaswa kama nilivyosema ndani ya swali langu Waziri anawaambia vijana hao wamwone nani ili watoe kilio chao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa vijana watanyanyaswa na mtu yoyote yule basi vijana wawasiliane na Serikali na Serikali kwa maana ya kutoka kwenye ngazi ya Wilaya pale DC yuko, kwenye ngazi ya Mkoa yuko Mkuu wa Mkoa na wakija kitaifa Wizarani kwetu yaani Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Lakini vile vile pale walipo Wabunge ni sehemu ya Serikali. Kwa hiyo, naomba Wabunge nao wawasaidie vijana ili wasinyanyaswe. Ahsante.

Na. 121

### **Watanzania Wanaofanya Kazi Nje ya Nchi**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi wanaweza kuchangia Pato la Taifa kwa njia moja au nyingine:-

(a) Je, kuna Watanzania wangapi wanaofanya kazi nje ya Tanzania?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwezesha Watanzania kupata kazi nje ya nchi na hivyo kuchangia Pato la Taifa?

(c) Je, Watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi wanachangia nini katika pato la Taifa?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaokwenda kufanya kazi nje, wamekuwa wanafanya hivyo kwa jitihada zao binafsi na kwa mantiki hiyo inakuwa ni vigumu sana kuelewa wapo wangapi, wanafanya kazi zipi na michango yao nyumbani inakuwa ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipitisha Sheria ya *The National Employment Promotion Services Act No. 9* ya mwaka 1999 na mojawapo ya malengo yake ni uanzishaji wa wakala binafsi wa kukuza ajira. Chini ya Sheria hii Wizara yangu chini ya Idara mpya ya Ajira, itaweka taratibu za kufahamu Watanzania wanaokwenda kufanya

kazi nje ya nchi, kwa lengo la kuhakikisha kwamba masharti yao ya kazi yanakuwa ya kibinadamu na vile vile kutazama uwezekano wa kupeleka wazalendo wenye sifa, ambao hawajapata ajira hapa nchini.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipana nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa uchumi halisi wa Taifa hupatikana kwa kuondoa mali yaliyozalishwa ndani ya nchi lakini bila kumilikiwa na Watanzania na kuongeza yale yaliyozalishwa nje ya nchi yakiwa yanamilikiwa na Watanzania. Je, Serikali haioni kwa kusema kwamba haijui ni kitu gani Watanzania walio nje wanazalisha, inaliambia Bunge hili kwamba haijui pato halisi la Taifa?

Pili, kwa kuwa Watanzania walio nje wanaporejea huweza kurudisha fedha nyingi za kigeni na kuweza kuchangia pato la Kitaifa. Ni kwa nini Serikali huweka vikwazo vya kodi kubwa kubwa na kuwakatisha tamaa na kwa hiyo wengine kuamua kuendelea kuwekeza huko na wasirudi kuwekeza Tanzania? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Naibu Spika, ukitumia hesabu za Pato la Taifa la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, tunatumia zote mbili yaani Pato la Taifa la wananchi katika nchi na Pato la Taifa linalotoka nje. Lakini hilo pato la Taifa linalotoka nje linajulikana siyo kama halijulikani, linajulikana.

Kwa maana hiyo basi, hesabu hizo ingawa siyo *presize* maana ni *estimate*. Ni kweli ni *estimate* lakini *estimate* ambazo zinakaribia zaidi uhakika kuliko *estimates* ambazo siyo za hakika. Kwa hiyo, kwa maana hiyo basi Pato la Taifa linajulikana na lina uhakika zaidi ya maendeleo kuonyesha ukuaji wa Pato la Taifa au kukua kwa Pato la Taifa la nchi. Nina uhakika na hili.

Kuhusu swali la pili, kodi lazima zitozwe kwa sababu ndiyo msingi wa Pato la Taifa. Lakini ziko sheria mbili katika nchi ambazo zinavutia wawekezaji. Kwa mfano, kuna Sheria ile ya mwaka 97 iliyoanzisha Kituo cha Uwekezaji yaani *Tanzania Investment Center* na Sheria ambayo tulipitisha mwaka jana hapa ya *EPZ*. Hizi zote zinaweka vivutio maalum kwa wale watu ambao wanataka kuwekeza katika nchi na hao ni wote Watanzania ambao wako nje wageni, kwa hiyo vivutio viko lakini suala la kodi lazima liendeleo kulifanyia kazi kwa sababu bila kodi Serikali haiwezi kupata mapato ya kujiendesha.

Na. 122

### **Huduma kwa Akina Mama Wajawazito**

**MHE. ASHA A. NGEDE** aliuliza:-

Kwa kuwa wanawake wengi wajawazito hawana uwezo wa kulipia gharama za hospitali binafsi (*Private Hospitals*) wakati wa kujifungua au kulipia gharama za daraja la kwanza katika hospitali za Serikali kwa kukosa vifaa vya uzazi kama vile pamba, *glove* na kadhalika na wengine hushindwa kabisa kuvipata vifaa hivyo kutokana na uwezo mdogo walio nao:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo na kama inalifahamu kwa nini isitenge fedha kwa ajili hiyo ili kuwasaidia akina mama wanaokwenda kujifungua hospitalini?

(b) Kutokana na akina mama wengi kutofahamu haki zao na taratibu zinazohusu upatikanaji wa vifaa hivyo, je, Serikali inawasaidiaje katika tatizo hilo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA (MHE. PROF. PHILLEMOM M. SARUNGI (k.n.y. WAZIRI WA AFYA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ngede, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika sera ya uchangiaji huduma za afya, Serikali imeweka bayana kwamba huduma za mama wajawazito zitolewe bila ya malipo katika vituo vyote vya afya vya uma.

Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya kununulia dawa na vifaa vya hospitali za umma mwaka hadi mwaka ili kuhakikisha kwamba wagonjwa wakiwemo mama wajawazito, hawakosi dawa au vifaa muhimu vya matibabu.

Vile vile katika jitihada za kuongeza mapato ya vituo vinavyotoa huduma za afya Serikali imeanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato vyenye madhumuni ya kupunguza uhaba wa dawa na vifaa muhimu vya tiba kama ifuatavyo:-

- (i) Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*).
- (ii) Mfuko wa Bima ya Afya (*NHIF*).
- (iii) *Drug Revolving Fund* (kwa wasio na msamaha).
- (iv) Uchangiaji wa Huduma za Afya kwa wasio na msamaha (*Cost-Sharing*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba dawa na vifaa muhimu vinapatikana katika vituo vya matibabu ili wananchi waweze kupata huduma kwa viwango vinavyokubalika kitaalam.

Wizara yangu inaendelea kuhamasisha uanzishaji wa Bodi za Afya za Halmashauri na Kamati za Afya za vituo vya kutolea huduma za afya ambazo zitakuwa na uwakilishi wa moja kwa moja wa jamii katika maeneo husika ili ziweze kusimamia upatikanaji na utunzaji wa vifaa muhimu vya matibabu. Bodi na Kamati hizi zitakuwa na

jukumu la kuchukua hatua za kinidhamu kwa wafanyakazi wanaokiuka maadili yao kwa kufanya wizi wa vifaa hivi na hivyo kuwalazimisha wagonjwa wavinunue.

**MHE. ASHA A. NGEDE:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa suala hili la vifaa vya uzazi vinatugusa wanawake wengi na katika nchi yetu ya Tanzania wapiga kura wengi ni wanawake na ndiyo walioiweka Serikali hii madarakani kwa matumaini ya kuwa ni mkombozi wao. Je, Waziri atakubaliana na mimi sasa Serikali kupitia Waziri wa Afya alivalie njuga suala hili kuweza kutokomeza kabisa matatizo yanayotugusa sisi akina mama? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA (MHE. PROF. PHILLEMOM M. SARUNGI (k.n.y. WAZIRI WA AFYA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango wa akina mama siyo kwamba ni wapiga kura tu lakini ni wazalishaji, wapiga kura wa kesho. Wazalishaji na walinzi wa kesho, wazalishaji wa nguvukazi ya kesho na wakina mama ndiyo wahimili wakubwa wa familia na wa Taifa. Kwa sababu hiyo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Kwanza, Serikali imeshatoa sera mbalimbali na zimepitishwa na Bunge hili sera zinazowatetea, kuwalinda na kuwawezesha akinamama. Katika Bajeti ya mwaka huu Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 16 hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia zaidi ya asilimia 20 kwa lengo la kununua dawa na vifaa mbalimbali na huduma za kina mama imepewa kipaumbele. (*Makofi*)

*Mheshimiwa Naibu Spika, Revolving Fund* iliyoanzishwa kwa mtaji wa shilingi bilioni 10 kwa msaada wa Benki ya Dunia ni mojawapo ya jitihada za Serikali, kwa kuwa mfuko huo dawa zinazonunuliwa zinazuzwa kwa nusu bei na fedha zinapopatikana zinasaidia kuwahudumia akina mama kwa kununua dawa na vifaa mbalimbali kama pamba, na *gloves*. Tatizo hapa siyo kukosekana tatizo ni usimamizi udhibiti wa matumizi kuhusu dawa na vifaa katika hospitali zetu.

Naomba Waheshimiwa Wabunge kwa kutumia Bodi za Hospitali na Kamati za Tiba ambazo zimeundwa katika kila hospitali ya Wilaya na Mkoa kusimamia huduma hizi kama ipasavyo. Tuwafichue wachache ambao wanatumia dawa hizo kwa manufaa yao badala ya kuwahudumia akina mama. (*Makofi*)

Na. 23

### **Mawasiliano Buchosa**

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano ya simu ni muhimu sana hasa katika ulimwengu wa sasa na kwa kuwa wananchi wa Buchosa wanayo shauku kubwa ya kupata mawasiliano ya simu za aina yoyote ile na hiyo ni haki yao na kwa kuwa mawasiliano ni njia mojawapo

inayoweza kutumika katika kupambana na ujambazi kama ilivyo kwa sehemu zile zenye mawasiliano na kwa kuwa wataalam walioko Mwanza walitoa fomu kwa wananchi waliotaka huduma hiyo na wananchi walijaza fomu hizo lakini hadi leo hakuna kilichofanyika:-

(a) Je, hiyo sio dalili ya kuwavunja moyo wananchi wa Vijiji vya Lugatta, Nyakasasa, Nyakarilo, Nyehunge, Kalebezo, Bupandwa na vijiji vingine vingi kwa kuwapa matumaini yasiyotekelezeka?

(b) Je, ni lini huduma hiyo itafikishwa kwa wananchi wa Buchosa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina nia ya kuwavunja moyo wananchi wa Buchosa. Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) inaendelea na zoezi la kufanya utafiti kuhusu uwezekano wa kupata biashara ya simu kwenye maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na kama itaonekana kuna biashara maeneo hayo yataingizwa kwenye mpango wa maendeleo ya Kampuni. Lakini hata hivyo, kwa upande wa simu za mkononi, Kampuni ya *Celtel* hivi sasa inatoa huduma katika Wilaya ya Sengerema. Kijiji cha Nyehunge kitapata huduma za *Celtel* kabla ya mwaka huu wa 2003 kwisha. *Celtel* nayo pia inaendelea na kufanya tathmini ya soko katika maeneo mengine katika Wilaya ya Sengerema na Mikoa ya Ziwa kwa ujumla. (*Makofi*)

Na. 124

### **Uuzwaji wa *Shares* za *TTCL***

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inao mpango wa ama kubinafsisha au kuuza baadhi ya mashirika yake na kwa kuwa moja ya mashirika yaliyouzwa ni *TTCL* kwa hisa (*shares*) 35 na kwa kuwa mara nyingi hao wanunuzi hawalipi kikamilifu kwa mujibu wa makubaliano na hata wanapopewa maelekezo ya kuweka line hawaweki na kwa kuwa Menejimenti ya wanunuzi hao hulipwa hela nyingi kutokana na mapato yanayopatikana na kwa kuwa mara nyingi wanunuzi hawa huwapunguza wafanyakazi baada ya kununua shirika husika:-

(a) Je, Serikali inaweza kutueleza *shares* hizo 35 za *TTCL* zimeuzwa kwa kiasi gani?

(b) Je, katika mwaka 2002 wanunuzi hao walitakiwa waweke line ngapi?



(c) Je, Menejimenti hulipwa *fee* ya kiasi gani kutokana na mapato yanayopatikana?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hisa 35 yaani 35% za *TTCL* zimeuzwa kwa kiasi cha dola za Kimarekani milioni 120. Dola milioni 60 zimekwishalipwa na 60 zilizobaki zitalipwa baada ya mahesabu ya mwaka 2000 kukubalika.

(b) Takwimu tulizonazo zinaonyesha kuwa wanunuzi hawa walitakiwa kuhakikisha zimewekwa line mpya 41,000 kwa mwaka 2001 na njia 60,500 kwa mwaka 2002 katika mtandao wa simu za kawaida za *TTCL*. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la menejimenti kulipwa *fee* ni suala la mkataba au maridhiano ya kibiashara kati ya muuzaji na mnunuzi suala ambalo si vema kimkataba kutaja hadharani maslahi ya upande mmoja bila ridhaa ya upande wa pili. Hivyo haitawezekana kutaja ni kiasi gani Menejimenti hulipwa kama *fee* kutokana na mapato.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninalo swali moja dogo tu. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba hao jamaa wanaonunua *TTCL* watalipa madeni yote?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, malipo yatafanyika baada ya kukubaliana mahesabu na itategemea mahesabu yanasema nini.

Na. 125

### **Ujenzi wa Barabara Kati ya Babati na Simanjiro**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa mpya wa Manyara ulitangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali *GN. No. 367* la tarehe 2 Agosti, 2002 na kwa kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kwa wananchi hapo tarehe 31 Julai, 2002 alieleza azma ya Serikali ya kugawa maeneo kuwa ni kutaka kuboresha Utawala, Huduma za Jamii, Kiuchumi na Miundo mbinu:-

(a) Je, ile ahadi ya Serikali ya kujenga barabara ya kudumu kati ya Babati na Simanjiro sasa imefikia hatua gani?

(b) Je, Serikali ina mipango gani ya kujenga barabara za lami angalau kilomita 5 tu kwa kila upande kuelekea barabara kuu ya Singida, Arusha, Dodoma na kuelekea hospitali ya Wilaya kutokea katikati ya Mji wa Babati ili kuleta sura mpya itakayofanana na Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' Mbunge wa Babati Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Serikali ya kujenga barabara ya kudumu kati ya Babati na Orkesumet/Kibaya ipo pale pale. Katika mwaka wa fedha wa 2002/2003 jumla ya shilingi milioni 120 zilitengwa kwa ajili ya kazi za kubaini eneo muafaka la kupitisha barabara, kuandaa nyaraka za zabuni na kufanya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 300 kwa kazi ya kuanza ujenzi wa barabara hii. Taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga barabara hii utanza mara baada ya kukamilika kazi zilizotajwa hapo juu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za kutoka katikati ya Mji wa Babati kuelekea barabara kuu ziendazo Singida, Arusha na Dodoma zitajengwa chini ya mpango wa kujenga barabara kuu za Dodoma - Babati na Singida - Babati - Minjingu. Maandalizi ya miradi hiyo yameshaanza ambapo mkataba wa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa barabara ya Singida-Babati-Minjingu umetiwa saina tarehe 26 Mei, 2003 na kazi inatarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja. Baada ya hatua hii kukamilika Serikali itatafuta fedha za ujenzi. Hivyo ujenzi utanza kutegemea upatikanaji wa fedha.

Aidha, Serikali inaendelea na mawasiliano na wafadhili mbalimbali kuhusu upatikanaji wa fedha za ujenzi wa barabara ya Babati-Dodoma hadi Iringa kwa kiwango cha lami.

Hata hivyo, kabla ya utekelezaji wa miradi mikubwa iliyotajwa hapo juu, Serikali kwa kupitia Bajeti ya fedha za Mfuko wa Barabara ya mwaka 2003/2004 imetenga jumla ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya uwekaji lami nyepesi (*OTTA SEAL*) katika kilomita 2.4 za barabara za mji wa Babati. Matengenezo hayo yataanza mwezi Januari, 2004 na kukamilika Juni 2004.

**MHE. OMAR S. KWAANGW'**: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa mpango wowote wa Serikali unaohusu maendeleo, unao muda wa kuanza na kumalizika. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuniambia kwamba barabara hii ambayo inatoka Babati kwenda Wilaya ya Simanjiro na Kiteto inatarajiwa kumalizika lini?

Pili, kwa kuwa barabara hii ya kutoka Babati kwenda Wilaya ya Simanjiro na Kiteto ni mpya, je, mali ambazo ni za wananchi zitakazoathirika wakati wa ujenzi wa barabara hiyo zitafidiwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa kuanza na kumalizika kwa barabara hii itajulikana baada ya usanifu kukamilika na mkataba kufikiwa na utakapotywa mkataba Mheshimiwa Mbunge tutakukaribisha ili ujue mwanzo na mwisho wa barabara hii itakuwa lini.

Mali ambazo zitakutwa humo ndiyo maana tunafanya *feasibility study* na usanifu ili tujue nini kinachotakiwa Serikali kuwajibika. Kwa hiyo, kujibu kulipa ama kutolipa ni wakati huo ambapo tutakuwa tayari tuna taarifa mkononi. *(Makofi)*

Na. 126

### **Wizara zilizopanga kwenye Majengo Binafsi**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa mpaka sasa bado zipo Wizara ambazo hazina majengo yake ya kudumu badala yake hufanyia shughuli zake kwenye majengo ya mashirika na ya watu binafsi na kusababisha Wizara hizo kulipa fedha nyingi sana za pango:-

Je, Wizara ya Viwanda na Biashara inalipa kodi ya jengo kiasi gani kwa mwaka kwa wamiliki wa jengo ambamo wamepanga?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara, inalipa kodi ya pango ya Shilingi milioni 295.49 kila mwaka kwa Ofisi zake zilizopo katika jengo la washirika, Mtaa wa Lumumba na Jengo la Shirika la Bima *(NIC)*, lilipo Mtaa wa Samora na Urambo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa inaonyesha kwamba Serikali inalipa pesa nyingi sana katika Mawizara yake kwa kupanga. Je, Serikali inapata faida gani kukaa Dar es Salaam badala ya kukaa Dodoma? Kama inapata hasara, je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kukodisha majengo hapa Dodoma nusu ya pesa ambazo inalipa na Ofisi nyingine ikaendelea na ujenzi hapa Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba inalipa pesa nyingi Dar es Salaam na ndiyo maana sasa kuna msukumo mkubwa wa kuhamia Dodoma ambapo majengo yetu wenyewe tutajenga na kuyatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya kuja Dodoma na kukodi majengo. Majengo ya kukodi Dodoma hayapo. Yangukwepo tungekwishaingiza Wizara nyingi, ndiyo maana tunajenga sasa nyumba za kuhamia Dodoma. Dar es Salaam zipo ndiyo maana tumepanga.

Na. 127

### **Bei na Vinu vya Kuchambulia Pamba - Kilosa**

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Mikumi Kata za Kilangali, Mabwerebwere, Masanze, Zombo, Ulaya na Kisanga zimeamua kulima pamba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati na kuboresha mitambo ya jineri ya kuchambulia pamba iliyoko Kilosa ili kuondoa usumbufu wa kupeleka pamba Morogoro kwa ajili ya kuichambua?

(b) Kwa kuwa wananchi wamekuwa wakiambiwa kuwa, pamba yao italipwa mara wanapouza na kwamba bei itapanda kufikia shilingi 250/= kwa kilo ili kuwaondoa hofu ya kukopwa tena pamba yao na kulipwa bei ndogo kama miaka ya nyuma, je, sasa Serikali kwa kilimo cha mwaka huu inawatamkia nini wananchi kuhusu usumbufu huo ili waondoe wasiwasi wa kulipwa bei ndogo na kusafirisha pamba yao mbali?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher S. Wegga, Mbunge wa Mikumi, pamoja na masahihisho lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha kuchambulia pamba cha Kilosa kilikarabatiwa na Bodi ya Pamba mwaka 2001 kwa lengo la kuwezesha uchambuzi wa pamba iliyozalishwa Wilaya Kilosa katika msimu wa 2001/2002. Hata hivyo, Kiwanda kilikabiliwa na deni la umeme la miaka ya nyuma la takribani shilingi 12,366,000. Tatizo hili la deni lilisababisha kiwanda kukatiwa umeme na hivyo kikashindwa kuchambua pamba katika msimu wa 2002/2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa zao la pamba kwa wananchi wa Wilaya ya Kilosa, Serikali kupitia Bodi ya Pamba imelipa deni lote la umeme ili kiwanda kiweze kuchambua pamba msimu huu wa 2003/2004. Kwa hiyo, pamba yote ya Wilaya ya Kilosa ikiwemo pamba ya jimbo la Mikumi hivi sasa inachambuliwa katika kiwanda cha Kilosa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo wa soko huru Serikali haipaswi kupanga bei ya mazao ya wakulima, isipokuwa bei hizo hupangwa na wadau wa zao husika kwa kuzingatia mwenendo wa bei katika soko la dunia na gharama za uzalishaji. Kwa upande wa zao la pamba, umoja wa wadau wa Pamba yaani *Tanzania Cotton Association*, hupanga bei ya chini ya kuanzia majadiliano yaani *low price* kabla msimu wa ununuzi kuanza. Kwa kuwa wanunuzi wote wa pamba ni wanachama wa chombo hiki ambacho hujadili na kukubaliana bei ya chini, wanunuzi wote wanapaswa kuheshimu maamuzi yaliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2003/2004 dira ya bei ya zao la pamba kwa nchi nzima ilikuwa shilingi 225/= kwa kilo ya daraja la kwanza na shilingi 100/= kwa daraja la pili.

Katika Kanda ya Magharibi ambapo ununuzi ulianza mwezi Julai 2003, bei ya wastani iliyopatikana kwa wakulima ilikuwa shilingi 280/= kwa kilo ya daraja la kwanza. Ununuzi katika kanda hiyo umekamilika. Katika kanda ya mashariki ambapo msimu wa ununuzi ulianza tarehe 30 Septemba, 2003 wanunuzi wa zao la pamba wanunua pamba kwa wastani wa shilingi 300/= kwa kilo ya daraja la kwanza na shilingi 100 kwa daraja la pili.

Serikali inapenda kuwaondolea wasiwasi wa kulipwa bei ya chini wakulima wa zao la pamba wa kanda ya mashariki kwa kuwa tayari wanunuzi wamekubali kununua pamba kwa shilingi 300/= kwa kilo ya daraja la kwanza bei ambayo iko juu kuliko bei ya dira.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupata jibu zuri kutoka kwa Naibu Waziri. Je, sasa Waziri anaweza kuwahakikishia watu wa Kilosa kwamba madawa na mbegu yatafika mapema kutokana na mwaka huu mvua ni kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Christopher Wegga, kuridhika na jibu tulilotoa hapa. Lakini nataka nimhakikishie kwamba nia ya Serikali ni kuwasaidia wakulima katika shughuli zote zinazohusiana na ukulima wa mazao pamoja na yale yanayohusiana na ununuzi.

Kwa hiyo, suala la mbegu pamoja na madawa, Serikali imeshasikia na itaifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 128

### **Kero ya Ushuru wa Aina ya Kodi**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imedhamiria kupunguza na hata kuondoa kabisa kero ya ushuru wa aina ya kodi ambazo ni kero kwa wananchi; na kwa kuwa kutozwa ushuru au kodi zinazojirudia rudia ni kumdidimiza mlengwa na hivyo kumwongezea umaskini:-

Je, Serikali itafuta ushuru na kodi mbalimbali zinazojirudia rudia ili kumpa unafuu wa bei mkulima wa kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imedhamiria kufuta kodi, ushuru na ada mbalimbali zinazotozwa na Serikali za Mitaa ambazo ni kero kwa wananchi. Utekelezaji wa dhamira hii umejidhihirisha ambapo katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali imefuta baadhi ya kodi, ushuru na ada za Halmashauri na kuziwekea viwango maalum kodi nyingine. Uamuzi huu unahusisha pia ushuru na kodi zinazohusiana na mazao ya kilimo likiwemo zao la kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali kuchukua hatua hii ni kufanya marekebisho katika mfumo wa kodi za Serikali za Mitaa na kuwapunguzia kero wananchi kwa kodi zilizoonekana kusababisha kero na usumbufu. Ni dhahiri kuwa baadhi ya kodi hizo zilikuwa zinakwamisha jitihada za kukuza uchumi pamoja na jitihada za kupunguza umaskini. Kwa mfano, badala ya kumwinua mkulima, kodi hizo zilikuwa zinamdidimiza na kumwongezea umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma hii Serikali imetoa mwongozo unaobainisha kodi, ushuru na ada zitakazoendelea kutozwa na Serikali za Mitaa pamoja na kuainisha maeneo na huduma ambazo hazitatozwa. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2003 mwongozo huo umebainisha kwamba, Serikali za Mitaa haziruhusiwi kutoa ushuru wa mazao kwa mnunuzi zaidi ya asilimia tano ya bei ya shambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kufuta baadhi ya ushuru na kodi ambazo ni kero kwa wananchi inatarajiwa kumpatia mkulima bei ya kuridhisha kwa mazao yake, kumwongezea kipato na kumpunguzia umaskini.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa kuwa gharama za uzalishaji wa kahawa na mazao mengine ya biashara ni kubwa sana na Serikali inalifahamu hilo; na kwa kuwa bei anayopata mkulima baada ya kuwa amezalisha zao lake ni ndogo, haiwezi kurudisha gharama zake alizotumia katika kuzalisha zao hilo; je, Serikali ina mpango gani wa

kuona ya kwamba inafuta kodi zote na ushuru kwa mkulima ili aweze kupata bei inayomtosheleza kurudisha gharama zake na kuendesha maisha yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa nchi zinazoendelea zimeanza utaratibu wa kutoa ruzuku kwa wakulima wa mazao ya biashara katika nchi zake; na kwa kuwa Tanzania ni nchi inayoendelea na ina wakulima wengi na ambapo mazao ya biashara ndiyo msingi; je, Serikali ina utaratibu gani sasa wa kuhakikisha ya kwamba inatoa ruzuku ya kilimo kwa mkulima moja kwa moja siyo katika utafiti wala katika kongamano na *workshop*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufuta kodi ya mazao kama kahawa na pengine siyo zao la kahawa tu ambalo bei ya uzalishaji, gharama za uzalishaji ni kubwa kuliko bei anayopata mkulima pengine kuna mazao mengine vile vile, hilo litahitaji kufanyiwa utafiti wa kina na kufikia uamuzi hapo baadaye kama itaonekana kwamba hivyo ndivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili juu ya ruzuku. Kama tulivyosema ya kwamba mwaka huu tumeanza kwa mbolea tu na kwa baadhi ya Mikoa, Serikali kama itakavyoendelea na kama hali itakavyoruhusu, tutaangalia namna ya kiasi gani cha ruzuku kwa kila zao kulingana hasa na uzalishaji wa mkulima ili kuweza kuzalisha zaidi na kuweka mapato zaidi kutokana na zao analolilima na hasa kuangalia gharama zinahusika za pembejeo ili kuweza kumfidia mkulima huyo kwa ruzuku.

Na. 129

### **Michango Mikubwa kwa Sekondari za Bweni za Serikali**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kutumia busara zake imeamua kufuta michezo ya UMISHUMTA; na kwa kutambua pia uwezo mdogo wa wazazi wa kulipa ada, imeweka viwango vya ada kwa shule za sekondari ili wazazi waweze kusomesha watoto wao:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba zipo shule za sekondari za Serikali hasa za bweni ambazo wazazi wanalazimika kulipa michango mikubwa kuliko ada iliyowekwa na Serikali?

(b) Kwa kuwa michango hiyo mikubwa inaondoa nia ya Serikali ya kuwapa wazazi uwezo wa kusomesha watoto wao; je, Serikali inakabiliana vipi na michango hiyo mikubwa?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya michango hiyo iliyo kinyume na mapendekezo ya Serikali katika hotuba yake ya Bajeti

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haijapata taarifa kama zipo shule za sekondari za Serikali hasa za Bweni ambazo wazazi wanalazimishwa kulipa michango mikubwa kuliko ada iliyowekwa na Serikali. Wizara yangu ilitoa maagizo kwa Wakuu wa Shule zote za Sekondari na Vyuo vya Serikali kwa Waraka wa Elimu Na. 2 wa mwaka 1999, kuwa michango inayoweza kuchangishwa kwa hiari ya wananchi kupitia Bodi ya Shule isizidi shilingi 15,000/= kwa mwaka kwa kibali cha Mkaguzi Mkuu wa Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu bado inasisitiza kwamba hakuna ruhusa ya kuwatoza wazazi wa wanafunzi wa shule za sekondari za Serikali michango ya fedha taslimu bila kibali cha Afisa Elimu Kiongozi ambaye kwa kiwango cha hadi shilingi 15,000/= amekasimu madaraka hayo kwa Mkaguzi Mkuu wa Kanda. Bodi ya shule ya sekondari inaweza kuamua yachangiwe maendeleo ya shule yao kwa makubaliano yao wenyewe katika Jumuiya ya Shule ambayo yatafikishwa katika vikao vyao na kupewa kibali cha Afisa Elimu Kiongozi kwa madaraka aliyomkasimu huyo Mkaguzi Mkuu wa Kanda. Michango ya aina hii haitakiwi kuwa kikwazo cha kuandikisha au kikwazo cha mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

Kwa hiyo, Bodi za Shule za Sekondari zinatakiwa kuwa makini sana katika kuweka viwango vya michango ya aina hiyo ambayo kwa vyovyote vile isizidi hiyo shilingi 15,000/= . *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nampongeza kwa kweli kwa jinsi Wizara ya Elimu na Utamaduni inavyofanya kazi yake vizuri. Ningependa kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa michango hiyo ikishaidhinishwa na mamlaka mbalimbali inakuwa ni sehemu ya ada; na kwa kuwa sasa hivi upo utaratibu ambao umeanza kujitokeza katika shule za sekondari kwamba mwanafunzi anapokuwa hakumaliza michango hiyo, anapomaliza kidato cha nne ananyimwa fomu zinazoitwa *Sel form* au fomu zile zinazomfanya achague elimu ya kidato cha tano, ananyimwa kuzipata fomu hizo au hata akijaza katika shule yake hazipelekwi, hivyo kuwezesha kwamba wapo vijana huko Vijijini daraja la kwanza, *division one* wameshindwa kupata nafasi ya kuchaguliwa kidato cha tano kwa sababu ya kunyimwa fomu hizo.

Je, hilo ni agizo la Serikali, Mamlaka ya Bodi za Shule au ni *Management* tu ambayo inatoa maamuzi makali hayo ambayo kwa kweli yanawaathiri sana vijana wetu wa Taifa hili? *(Makofi)*



**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nisisitize kwamba michango inayoruhusiwa ni kiwango hicho nilichokitaja kisichozidi shilingi 15,000/=.

Napenda nikubaliane naye kwamba mchango wa sura hiyo ukishakuwa umepangwa kwa kweli unakuwa kama ni sehemu ya ile ada kwa sababu ni fedha inayotakiwa ilipwe ndiyo maana Serikali imepanga ada kwa ajili ya sekondari kiwango kidogo sana, kwa sekondari za kutwa ni shilingi 40,000/= na kwa sekondari za bwani ni shilingi 70,000/=. Kwa hiyo, Serikali isingependa hata kidogo kwamba ibandikwe juu ya hapo michango mikubwa zaidi kwa sababu itakuwa kikwazo kikubwa hasa kwa watu ambao mapato yao ni ya hali ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaratibu unaowekwa wa kukusanya, ni kweli mimi nafahamu kabisa ya kwamba baadhi ya shule kama mtu hajalipa huzuia asipate *Sel form, School Leaving Certificate* au yale matokeo, mimi nafikiri huu ni utaratibu uliowekwa kwa kujaribu tu kuhimiza makusanyo.

Mimi napenda kuahidi kwamba kama kuna mchango uliowekwa zaidi ya hii shilingi 15,000/= halafu kuna mwanafunzi anazuiwa kupata matokeo, ningependa nitaarifiwe ili niweze kutoa maagizo apewe hayo matokeo. (*Makofi*)

Na. 130

### ***Greenbelt* katika Upimaji wa Viwanja**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Je, kwa nini Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi haizingatii dhana ya *greenbelts* katika upimaji wa viwanja vya majengo kwenye Miji yetu ili kuifanya ipendeze?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa dhana ya kijani kibichi katika upangaji wa Miji hapa nchini. Juhudi zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kupitisha Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. Aidha, Sheria zimetungwa na miongozo mbalimbali imetayarishwa na kusambazwa kwa wahusika ili kufanikisha utekelezaji wa sera hizo.

Serikali inazingatia maelekezo ya Sera na Sheria za upangaji wa Miji katika hatua za Uandaaji wa Michoro ya Mipango Mji (*Town Planning Drawing*) na ramani za upimaji wa ardhi (*survey plans*) ambazo zinapatikana katika Ofisi za Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya nchini kote. Katika vielelezo hivyo, maeneo ya wazi (*public*

*open spaces*), maeneo ya hifadhi ya kijani kibichi (*green areas*) na ukanda wa kijani kibichi (*greenbelt*) yameonyesha kuwa yametengwa au yatatengwa na kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi wa kupima viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam, Wizara yangu imezingatia dhana ya maeneo ya kijani kama ifuatavyo:-

- Viwanja vya wazi (*public open spaces*) vya ukubwa mbalimbali kwa ajili ya michezo, burudani na mapumziko vimetengwa katika maeneo yote ya makazi ya watu.
- Mabonde ya mito na vijito yamelipiwa fidia na kutengewa ukanda mpana wa hifadhi (*conservation*) ambao umepimwa na utatumika kwa kupanda miti.
- Maeneo yenye miinuko na miteremko mikali yamelipiwa fidia na kupimwa kuwa maeneo yasiyostahili kujengwa nyumba na badala yake yatapandwa miti kuzuia mmomonyoko.
- Ardhi yote ya maeneo tete au oevu (*wetlands*) imezungukwa na ukanda wa kijani (*greenbelt*) kwa ajili ya kuhifadhi ardhi na maji kupendezesha mandhari.
- Maeneo ya miundombinu kama vile njia za umeme, mabomba makubwa ya maji, mafuta na gesi, barabara kuu na reli yametengwa kuwa maeneo ya kijani (*green areas*) kwa sababu ya usalama na kupendezesha Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na Sera na Sheria nzuri ni muhimu na ni vitendea kazi vya lazima, lakini havijitoshelezi bila usimamizi na utekelezaji makini.

Hivyo, ili kuzifanya Sera na Sheria zilizopo kutekelezwa ipasavyo, natoa wito kuimarisha usimamizi na ushirikiano baina ya Waheshimiwa Madiwani, Watendaji katika Halmashauri zote na wananchi kwa lengo la kuzuia uvamizi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na maeneo ya kijani katika Miji yetu yote.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu lakini ningependa kuuliza swali la nyongeza lifuatalo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wote tunaona hali ya pale Jangwani Dar es Salaam, natumaini ni kwa sababu ya kutosimamia. Lakini kwa jibu lile la nyongeza kwamba katika kupanga upya, katika mpango wa viwanja 20,000 Dar es Salaam wamezingatia masuala hayo; je, katika kufanya hivyo haoni kwamba chini ya mpango wa

viwanja 20,000 kujenga nyumba ndogo ndogo yaani siyo maghorofa, Jiji la Dar es Salaam litafika Tanga mpaka Morogoro na nchi nzima itakuwa nyumba tu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tusipoangalia maghorofa yatafunga hata Mji wa Kibaha lakini hatuna Sheria inayomfunga mtu kujenga nyumba anayoitaka, iliyobaki ni kujenga kwa mpango, afuate taratibu za Sheria ambazo zinatawala Mpango Mji na pia afuate jinsi ambavyo tumetenga maeneo kama ambavyo nimesema greenbelt, mahali pa burudani, wasiharibu Mpango Mji kama ambavyo Sheria zinatawala. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi utakwenda kwa matakwa lakini kwa utaratibu uliopangwa na Sheria. *(Makofi)*

Na. 131

### **Uhaba wa Maji - Nzega**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Nzega wanakabiliwa na uhaba wa mara kwa mara wa maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo:-

(a) Je, ni lini wananchi hao watasaidiwa kupata visima na malambo?

(b) Je, kuna mpango gani mahsusi unaoandaliwa wa kusaidia kutatua tatizo hilo la maji hasa kwa Mikoa ya Tabora na Shinyanga?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maji inaelekeza kwamba wananchi ambao ndio walengwa wa miradi ya maji washirikishwe kikamilifu katika hatua zote ikiwa ni pamoja na kubuni, kupanga, kujenga, kugharamia matengenezo na uendeshaji wa miradi yao. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wahisani inaweza kusaidia juhudi za wananchi kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha. Wananchi wanao wajibu wa kuunda vyombo vya usimamizi wa huduma za maji yaani Kamati za Maji ama Jumuiya za watumiaji maji na kufungua mifuko ya maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wahisani, Halmashauri za Wilaya na wananchi imechimba visima virefu 10, visima vifupi 56 na kuvifunga pampu za mkono ili kupunguza tatizo la uhaba wa maji katika Wilaya ya Nzega. Ukarabati wa lambo la Kijiji cha Ibako nao umefanyika katika mwaka wa fedha 2002/2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa malambo mengine Wilayani Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya kupunguza tatizo la uhaba wa maji linategemea sana mwamko wa wananchi katika kuanzisha Kamati za Maji na kufungua mifuko ya maji. Hadi sasa, kati ya Vijiji 133 vilivyopo Wilayani Nzega ni Vijiji 47 tu vilikwishaunda Kamati za Maji na kuanzisha mifuko 46 ya maji yenye jumla ya shilingi 5,391,000/=. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kama kawaida yake, aendelee kusaidia kutoa elimu kwa wananchi wa Wilaya ya Nzega ili waone umuhimu wa kujiunga na kuanzisha Kamati za Maji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa muda mrefu wa kutatua tatizo la maji hasa kwa Mikoa yenye ukame ikiwemo Shinyanga na Tabora ni kuchimba visima virefu na ujenzi wa mabwawa. Tangu mwaka 1985 Mkoa wa Shinyanga umekuwa ukitekeleza mpango wa usambazaji wa huduma za maji Vijijini kwa ufadhili wa Serikali ya Uholanzi.

Hivi karibuni Serikali imeanzisha mpango mpya ambao umezinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Machi, 2003 wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji. Mpango huu unatekelezwa kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga. Tofauti na ule wa awali, mpango huu upo huru kutumia teknolojia yoyote ile ambayo wananchi wana uwezo wa kuiendesha. Kiasi cha shilingi bilioni 8.9 kitatumika kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Tabora, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za kuanzisha mpango utakaohusu Wilaya zote za Mkoa. Katika mwaka 2002/2003 Serikali ilikamilisha mradi wa maji wa Kijiji cha Chibiso Wilayani Igunga kupitia mradi uliofadhiliwa na nchi ya Japan.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wilaya ya Igunga ina maandalizi ya utekelezaji yanayoendelea kwa miradi ya maji katika Vijiji kumi chini ya Mradi wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (*RWSSP*) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Kadhalika Wilaya ya Nzega, Sikonge na Urambo nazo zimeongezwa kwenye orodha ya Wilaya 38 zitakazonufaika na mradi uliotajwa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na pia napenda kuipongeza Wizara yake kwa kazi waliyoifanya, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora pamoja na Shinyanga wako karibu sana na Ziwa Victoria ambalo hupeleka maji katika nchi za nje na kuwaacha wananchi wa Wilaya hizi, Mikoa hii wakiwa na hali ya ukame; je, Serikali ipo tayari kuyashawishi mashirika, watu binafsi na wananchi kwa ujumla kuyatumia maji ya Ziwa Victoria ili kuondoa ukame wa maji ya watu pamoja na maji ya mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora na wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni wafugaji wazuri sana wa mifugo; na moja ya sababu ambayo imewafanya wananchi hawa wahame maeneo hayo ni kwa sababu ya kufuata maji kwa sababu malambo hayatoshi; je, Serikali ipo tayari kuongeza

kasi ya uchimbaji wa malambo katika maeneo haya ya Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Shinyanga na hasa Wilaya ya Nzega? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya Ziwa Victoria *catchments area* yake ni pamoja na maeneo mengi ya Mkoa wa Shinyanga, hivyo kwa kuanzisha utaratibu wa kuchimba malambo sehemu za Mikoa ya Tabora na Shinyanga, itasaidia sana badala ya kusubiri maji yafike *Lake Victoria* halafu tunayachukua tena kurudisha umbali huo ambao uliopo, mfano kama Nzega ni karibu kilomita 300.

Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema katika miradi hii mipya ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia, tutazingatia uchimbaji wa malambo ili kukidhi matumizi ya binadamu na wakati huo huo kukidhi matumizi ya maji kwa ajili ya mifugo.

Na. 132

### **Ukarabati wa Bwawa la Nyumba ya Mungu**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitenga shilingi milioni 150 katika mwaka wa fedha 2001/2002 kwa ajili ya ukarabati wa Bwawa la Nyumba ya Mungu; na kwa kuwa kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ya kuchimba kisima cha kutoa maji safi kwa wananchi wa Kijiji cha Kisangara katika Bajeti hiyo lakini hakuna utekelezaji wowote uliofanyika hadi sasa:-

(a) Je, fedha za ukarabati wa bwawa hilo zitapatikana lini ili kazi hiyo iweze kuanza?

(b) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuchimba kisima cha maji safi kwa wananchi wa Kisangara?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Bwawa la Nyumba ya Mungu linamilikiwa na Wizara yangu, hivyo utunzaji wake ikiwa ni pamoja na ukarabati wa bwawa hili ni jukumu ya Wizara yangu. Bwawa hili hutumika kuhifadhi maji kwa ajili ya mitambo ya umeme na mahitaji mengine ya kiuchumi.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa katika mwaka wa fedha 2001/2002 Wizara ilipanga kukarabati Bwawa la Nyumba ya Mungu kwa gharama ya shilingi milioni 150. Kutokana na kutokupatikana kwa fedha hizo, kazi hiyo haikufanyika. Hata hivyo, Wizara yangu ilipanga tena kutekeleza kazi hiyo katika mpango wa mwaka wa

fedha 2002/2003 ambapo kiasi cha shilingi milioni 80 zilitengwa. Nafurahi kumuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizo zimepatikana na kutumwa katika Ofisi ya Bonde la Pangani kwa ajili ya kazi iliyokusudiwa. Taratibu za kumpata Mkandarasi wa kufanya kazi hii zinaendelea.

(b) Kuhusu ahadi ya Serikali ya kuchimba kisima cha maji katika Kijiji cha Kisangara, nakiri kusema kwamba Wizara yangu haijaweza kutimiza ahadi yake kutokana na kutopatikana fedha zilizotarajiwa kwa kazi hiyo. Hata hivyo, Wizara yangu inafanya juhudi kuhakikisha kuwa ahadi hiyo inatekelezwa mara fedha zitakapatikana.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa magugu ya Ziwa Jipe yamejijenga na yanasambaa kwa kasi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na hasa maeneo ya Handeni na Lang'atabora; je, ukarabati wa bwawa hilo utakuwa pamoja na kuondoa magugu hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa Kijiji cha Kisangara kwa sasa kinategemea maji ya Mradi wa Chanjale ambayo hayatoshi kwa sababu hakuna tanki la kuhifadhia maji hayo; je, Serikali iko tayari kufikiria kujenga tanki la kuhifadhi maji ili mradi huu utosheleze? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Bwawa la Nyumba ya Mungu, lakini pia kwa kupitia Mheshimiwa Mbunge ambaye ninafahamu ana uwezo mkubwa wa kuwashawishi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungejaribu kutumia utaratibu ambao ulitumika kupunguza magugu katika Ziwa Victoria kwa kuwashirikisha wananchi walio kando kando ili kuyavuna kwa kuyatoa *physically* kutoka kwenye eneo la maji, kitu ambacho nina hakika wananchi wa Jimbo lake ni watu ambao wana uwezo mkubwa, wanaweza kusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tanki la maji la Chanjale, la Mradi wa Maji wa Chanjale, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tukipata fedha na maombi rasmi ambayo yataonyesha ni kiasi gani Kijiji chenyewe kimechangia katika mradi huo ili kutekeleza sera zetu za maji, nina hakika ya kwamba Wizara iko tayari kutoa utalam na ushauri mahala ambapo patahitajika. Hii ikizingatia ya kwamba Mheshimiwa Mbunge anakazana sana kusaidia upatikanaji wa maji Jimboni kwake.

Hata hivyo, napenda pia ashukuru ya kwamba Serikali imejitahidi sana kuisaidia Wilaya yake kupatikana kwa maji na kupunguza matatizo ya maji kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yote tuliyoyapanga yamekwisha na muda nao umekwisha. Sasa tuna matangazo ya vikao. (*Makofi*)

Ile Tume ya Huduma za Bunge pamoja na Kamati ya Uongozi inayoendesha shughuli za Bunge, tukutane Saa Saba na Nusu pale tunapokutana, tukutane wote, Kamati ya Huduma za Bunge na Kamati ya Uongozi, kuna suala muhimu ambalo ni vizuri wote tukawepo ili tulitatie.

Pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 8.00 mchana, chumba Na. 133, *Wing C*, hawa wanakutana saa 8.00 mchana. Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawatangazia Wajumbe wake kwamba kesho tarehe 15 Novemba, 2003 kutakuwa na semina, masuala ya *Unit Trust of Tanzania*, chumba Na. 428, ghorofa ya nne kuanzia saa 3.00 asubuhi.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anawatangazia wajumbe wa Kamati hii kuwa kutakuwa na kikao leo saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 107, ghorofa ya kwanza. Kwa wale ambao pengine hawajafika hapo ni ofisini kwa Mheshimiwa Mwenyekiti Simpasa.

Matangazo mengine, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mwenyekiti wa Chama cha Idadi ya Watu na Maendeleo, anawaarifu wanachama wa chama hicho kukutana muda mfupi leo mara baada ya kuahirisha Bunge jioni, baada ya ile hotuba ya kufunga Bunge ya Waziri Mkuu, humu humu ndani, anasema ni maelezo mafupi tu.

Kwa wanamichezo, tangazo ni kwamba wote mnaombwa kukutana leo saa 9.00 alasiri katika chumba namba 231 ghorofa ya pili.

Nadhani mlipokea ile barua ambayo niliwaandikia kuwataarifu msiba wa mtoto wa mwenzetu, Mheshimiwa Martha Wejja. Sasa nina taarifa hapa kutoka kwa Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba mazishi ya marehemu yatakuwa siku ya Jumamosi tarehe 16 Novemba, tarehe 16 ni Jumapili, sasa sijui maana ni jambo muhimu hili ni Jumamosi au tarehe 16?

**MBUNGE FULANI:** Jumapili.

**NAIBU SPIKA:** Jumapili, kwa hiyo, Jumapili tarehe 16 Novemba, 2003 saa 5.00 asubuhi mjini Dar es Salaam. Usafiri utakuwepo hapa nje, Ofisi ya Bunge kuanzia saa mbili na nusu asubuhi. Sasa sina uhakika saa mbili na nusu Jumamosi au Jumapili hiyo hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Jumamosi.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Jumamosi saa mbili na nusu asubuhi kutakuwa na usafiri hapa kuwahi mazishi yatakayofanyika Jumapili saa tano na nusu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza shughuli zinazoendelea, naomba kuwataarifu kwamba wote mmeona order paper kazi iliyopo leo ni nini. Kuna Kauli ya Waziri, hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Muswada wa *Microfinance* lakini pia hoja ya kuahirishwa Bunge itasomwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kufunga Bunge. Ni kazi nyingi na muda tulionao ni mdogo.

Kwa taarifa tu, ule Muswada wa *National Micro Finance Bank* walioomba mpaka wakati napeleka orodha kwenda kuchapishwa walikuwa 16 kabla hata ile orodha haijarudi wakaongezeka wengine wanne kwa hiyo, 20. Sasa muda tuliona nao ni huo.

Mimi nitawapa nafasi mpaka pale ninapoono muda huu sasa umetosha tuendelee na shughuli nyingine. Kwa hiyo, hawatapata wote na ili kusaidia kwa wale watakaopata badala ya napongeza na nini tukifupisha muda tunaweza ku-*accommodate* wengi zaidi. Sasa orodha hiyo nimechapa kwa kadri ombi lako lilivyofika hapa. Kama umeniletea sasa hivi wewe ujue utakuwa wa 20 aliyewahi asubuhi kabla hata kusoma dua wa kwanza. Naomba hiyo ieleweke. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo, Katibu, *agenda* inayofuata.

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **TAMKO KUHUSU MALIPO YA UZEENI KWA WASTAAFU WALIOKUWA WATUMISHI WA SERIKALI NA KULIPWA PENSHENI KWA MKUPUO**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa tamko na taarifa kuhusu malipo ya uzeeni kwa wastaafu waliokuwa wa Serikali ambao walilipwa pensheni kwa mkupuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 11 Novemba, 2003, niliahidi kwamba nitawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tamko rasmi la Serikali kuhusu watumishi wastaafu wa Serikali ambao walilipwa pensheni kwa mkupuo kwa mujibu wa Sheria ya Pensheni Sura Na.371 na Kanuni za Pensheni, Sehemu ya Tano, Kifungu cha 23 ikisomwa pamoja na *Pension Laws Miscellaneous Amendment Act* Na.4 ya mwaka 1989. Hatua hii imefuatia maelezo binafsi ya Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, aliyotoa hapa Bungeni tarehe 11 Novemba, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake binafsi, Mheshimiwa Dr. Kamala, alipenda kufahamu hatua ambayo Serikali imefikia katika kutekeleza ahadi yake ya kuwasaidia wastaafu wa Serikali waliolipwa pensheni kwa mkupuo na ambao wamekuwa hai zaidi ya miaka ambayo Serikali ilitumia kuwalipa kwa mkupuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda ninukuu yale niliyosema hapa Bungeni tarehe 20 Juni, 2003 wakati wa majumuisho ya hotuba ya Bajeti. Nanukuu: “Mheshimiwa Spika, Serikali itaifanyia kazi ombi na kilio cha wastaafu ambao walichukua mkupuo miaka ya nyuma na mpaka sasa bado wako hai. Hawa idadi yao ni 33,700. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie kwanza *financial implications* za watu hawa lakini Serikali inalifikiria



na natumaini baada ya muda si mrefu pengine nitakuja na jibu sahihi.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa malipo ya pensheni kwa mkupuo yalizingatia sheria hatua ya kuwarudisha wastaafu hawa katika daftari la pensheni itahitaji marekebisho ya sheria husika. Aidha, gharama za kuwarudisha wastaafu hao na uwezo wa Bajeti ya Serikali wa kumudu gharama hizo vinahitaji kufanyiwa kazi kwa makini. Vile vile kuna kazi ya kuweka utaratibu utakaoweza kuwatambua wastaafu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko katika hatua za mwisho za kuifanyia kazi ahadi yake hiyo ya kuwarejesha wastaafu hao kwenye daftari la malipo ya pensheni. Inatarajiwa kwamba mapendekezo ya marekebisho ya sheria husika yatawasilishwa katika Bunge lako Tukufu mwaka huu wa fedha 2003/2004 ili zoezi la kuwaingiza wastaafu hao katika daftari la malipo ya pensheni lianze Julai, 2004. Aidha, utaratibu utakaotumika kuwatambua na nini wastaafu hao wafanye utaelezwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **MAAZIMIO**

#### **Azimio la Bunge la Kuruhusu Kuwasilishwa Siku ya Uteuzi Wagombea katika Chaguzi Ndogo za Majimbo Yaliyowazi ama Yatakayokuwa Wazi kati ya mwezi Novemba, 2003 na mwezi Oktoba 2004**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi Na.1 ya mwaka 1985, naomba kutoa hoja mbele ya Bunge lako Tukufu kuomba Bunge lipitishie Azimio litakaloruhusu kuwahishwa siku ya uteuzi wa wagombea Ubunge ili kuwezesha kufanyika kwa uchaguzi ndogo katika Majimbo yote ambayo viti vyake viko wazi na vitakavyokuwa wazi kati ya Mwezi Novemba, 2003 na mwezi Oktoba, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa yapo Majimbo mawili ya uchaguzi ambayo yapo wazi kutokana na Wabunge wa Majimbo hayo kupoteza sifa zao kuwa Mbunge kwa mujibu wa Ibara ndogo ya (1)(e) ya Ibara ya 71 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inataka Mbunge awe mwanachama wa Chama cha Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, uteuzi wa wagombea Ubunge katika Majimbo yaliyo wazi kwa ajili ya uchaguzi mdogo unatakiwa ufanyike katika muda usiopungua miezi ishirini na minne au usiozidi miezi ishirini na mitano tokea kiti cha Ubunge kiwe wazi au

mapema zaidi kama itakavyoamuliwa na Bunge baada ya Serikali kuwasilisha Azimio Bungeni.

Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 76(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano uchaguzi mdogo hauwezi kufanyika katika kipindi chote cha miezi kumi na miwili kabla ya Bunge kuvunjwa. Kwa kuzingatia masharti hayo ya Sheria ya Uchaguzi, 1985, uteuzi wa wagombea katika Majimbo yaliyo wazi unatakiwa ufanyika kati ya mwezi Aprili na mwezi Mei, 2005 na hivyo kuangukia katika kipindi ambacho Katiba ya nchi hairuhusu chaguzi ndogo kufanyika isipokuwa kama Bunge litakubali uteuzi wa wagombea Ubunge ufanyike mapema zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali inatekeleza programu nyingi katika sekta mbalimbali chini ya Mkakati wa Kuondoa Umaskini Nchini ambazo zinahitaji usimamizi wa karibu wa viongozi wote pamoja na Wabunge ili kuchochea kasi ya maendeleo nchini.

Serikali imeridhika kwamba ili kuwepo kwa usimamizi wa karibu wa harakati hizo, ipo haja ya kujaza viti vya Ubunge ambavyo viko wazi na viti vingine vyovyote vitakavyokuwa wazi kati ya sasa na mwezi Oktoba, 2004 mapema zaidi kuliko muda uliopangwa ili wananchi katika Majimbo hayo wapate wawakilishi wao Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili azma hii ya Serikali iweze kutekelezwa, kwa mujibu wa kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, naomba niwasilishe Azimio kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985, uteuzi wa wagombea Ubunge katika chaguzi ndogo unatakiwa kufanyika katika muda usiopungua miezi ishirini na minne na kwa vyovyote ndani ya muda usiozidi miezi 25 tokea kiti cha Ubunge kinapokuwa wazi au mapema zaidi kama itakavyoamuliwa na Bunge baada ya Serikali kuwasilisha Azimio Bungeni kupunguza muda huo;

NA KWA KUWA taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Spika kwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya 1985 inayoonyesha kwamba baadhi ya Majimbo ya Uchaguzi hivi sasa yako wazi;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 uteuzi wa wagombea katika chaguzi ndogo za Bunge kwa Majimbo yaliyo wazi au yatakayokuwa wazi zinapaswa kufanyika kati ya mwezi Novemba, 2003 na mwezi Oktoba, 2004 ili kuzingatia masharti ya Ibara ndogo ya (3) ya Ibara ya 76 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 inayokataza kufanyika kwa uchaguzi kwa muda wowote usiozidi miezi kumi na mbili kabla ya Bunge kuvunjwa na kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu;

NA KWA KUWA uchaguzi Mkuu unaofuata utafanyika katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2005 isipokuwa kama patatokea dharura itakayolazimu vinginevyo;

NA KWA KUWA utekelezaji wa programu mbalimbali za maendeleo unaofanywa na Serikali hivi sasa chini ya Mkakati wa Kuondoa Umaskini Nchini umeungwa mkono na wananchi na unahusisha rasilimali nyingi ambazo zinahitaji usimamizi wa karibu wa Serikali na viongozi wote ikiwa ni pamoja na Wabunge;

NA KWA KUWA Serikali imeridhika kwamba ipo haja ya kuwahisha siku ya uteuzi wa wagombea katika chaguzi ndogo za Majimbo yote yaliyo wazi na yale ambayo viti vya Ubunge vinaweza kuwa wazi kati ya sasa na mwezi Oktoba, 2004 ili chaguzi hizo zifanyike mapema zaidi;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985, Serikali inaweza kuliomba Bunge lipitisha Azimio litakaloruhusu kuwahisha kwa siku ya uteuzi wa wagombea katika chaguzi ndogo kwa Majimbo yaliyo wazi au yatakayokuwa wazi kati ya sasa na mwezi wa Oktoba, 2004;

KWA HIYO BASI, Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu linaazimia kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 muda wa uteuzi wa wagombea katika chaguzi ndogo za Bunge katika Majimbo ambayo viti vya Ubunge viko wazi na vile vile kwa Majimbo mengine yatakayokuwa hayatatimiza au hayatakuwa yametimiza masharti ya kifungu cha 37(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya 1985, uwahishwe ili uweze kufanyika wakati wowote kati ya mwezi Novemba, 2003 na mwezi Oktoba 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia hoja hiyo, ooh haikwenda kwa Mwenyekiti!

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - KIONGOZI WA UPINZANI BUNGENI NA MSEMAJI MKUU OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nikushukuru kwa kunipa nafasi kutoa maoni kuhusiana na Azimio ambalo limewasilishwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(c), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Azimio la Bunge lililowasilishwa na Mheshimiwa Waziri la kuruhusu kuwahishwa siku ya uteuzi wa wagombea katika chaguzi ndogo za Majimbo yaliyo wazi ama yatakayokuwa wazi kati ya mwezi Novemba, 2003 na Oktoba, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge ni chombo ambacho kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63(2) chenye madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 89(1) pia imelipa Bunge uwezo wa kutunga kanuni zake zitakazosaidia kutekeleza kazi zake. Kanuni Na. 91 ya Kanuni zetu za Bunge inatambua kuwepo Kamati ya Uongozi ambayo kimsingi ndio humsaidia na kumshauri Spika kuhusu mambo na mpangilio wa shughuli zinazopaswa kushughulikiwa na Bunge katika vikao vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, umekuwa ni utaratibu mzuri wako wewe na Mheshimiwa Spika mwenyewe wakati wote kuitisha Kamati ya Uongozi ambayo pia Kiongozi wa Upinzani au mwakilishi wake ni wajumbe ambapo shughuli zinazopaswa kushughulikiwa na Bunge hili katika kikao husika huwasilishwa na kujadiliwa na kisha kuamuliwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali kulileta kwapani Azimio hili bila hata kuwahi kugusiwa katika vikao vyote viwili vya Kamati ya Uongozi vilivyokaa tarehe 2 Novemba, 2003 na 11 Novemba, 2003 vinaitia wasiwasi Kambi ya Upinzani juu hasa ya madhumuni ya Serikali kama kweli hakuna hila ndani ya Azimio hili. Kama ulivyobainisha wewe mwenyewe hapa Bungeni hata Kamati husika haikuwahi kuletewa jambo hili kulijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtindo huu wa Serikali kuleta mambo kinyemela pamoja na kuliaibisha Bunge na kulidharau kwamba linaweza kupelekewa chochote na wakati wowote na likapitisha bila tatizo lakini pia ipo siku ambapo Serikali kwa tabia yake hii ambayo inaonekana kuendelea kukomaa itafanya kituko ambacho kitawaathiri hata hao wanaofikiri kwamba hayawahusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mabadiliko ya Sheria ya Uchaguzi yalipoletwa hapa Bungeni na kufuta sheria iliyokuwepo kabla, Kambi ya Upinzani ilieleza bayana kwamba Bunge liache tabia ya kutunga sheria au kufanya marekebisho ya sheria kwa minajali ya kulenga matakwa fulani ya kisiasa au manufaa ya kundi fulani la watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulieleza bayana kabisa kwamba mabadiliko hayo yalikuwa yamelenga Majimbo 15 ya Pemba ambayo Wabunge wake walikuwa wamekataa kuja Bungeni kutokana na vitendo vya dhuluma vya kuharibu makusudi uchaguzi wa mwaka 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ilieleza bayana pia kwamba mabadiliko hayo ya sheria yalikuwa yanawanyima haki ya uwakilishi wananchi wa Majimbo husika kwa muda mrefu katika vyombo vya kutunga sheria na kufanya

maamuzi mbalimbali. Kipindi hicho tulionekana majuha wa Abunuwasi, tulibezwa na hatukusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ambazo Serikali inazileta katika Azimio hili ni zile zile tulizozieleza hapa Bungeni na nanukuu sehemu ya *paragraph* ya pili, ukurasa wa pili wa Azimio unaoeleza kwamba nanukuu: “Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali inatekeleza programu nyingi katika sekta mbalimbali chini ya mkakati wa kuondoa umaskini nchini ambazo zinahitaji usimamizi wa karibu wa viongozi wote pamoja na Wabunge ili kuchochea kasi ya maendeleo.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunatoka wapi tunakwenda wapi? Sababu zilizoielezwa na Serikali hapa Bungeni wakati wa kuleta marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ni masuala ya gharama kubwa za uchaguzi jambo ambalo Serikali ilisema ingeweza kuathiri bajeti ya Serikali mara kwa mara. Hivi Serikali inataka kutuambia nini, sababu hizi hivi sasa zikoje?

Je, Serikali inatambua kwamba uko vijijini wananchi wengi hivi sasa wanaathirika kwa balaa la njaa na wengine wanakufa? Je, vipi wafanyakazi wa mashirika mbalimbali wanaodai mafao yao wanaoshinda kwenye magati ya Hazina na *PSRC*? Je, vipi tatizo la umeme ambalo tulielezwa hapa Bungeni linalotegemea kutukabili katika kipindi kifupi kijacho kutokana na kupungua kina cha maji na hivyo kuigharimu Serikali si chini ya bilioni 17 kila mwezi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufa na kuishi au mambo kubadilika kila siku ni jambo la kumwachia Mwenyezi Mungu. Hivi humu ndani Mwenyezi Mungu akituita kama Wabunge 24, Serikali italetwa Azimio lingine la kuondoa Azimio hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukawa tunafanya marekebisho ya sheria kwa kutanguliza maslahi ya Taifa na sio maslahi ya mtu fulani? Hali hii inaashiria matumizi mabaya ya madaraka. *Favour* kamwe isitumike kama kigezo cha kutunga sheria au kuleta maazimio hapa Bungeni huu ni ubinafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili linaletwa wakati ambapo kuna Mbunge wa Kambi ya Upinzani na Madiwani ambao wamejiunga na Chama fulani hii isije ikawa ni mbinu ya kutimiziana ahadi na makubaliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani bado inaamini mabadiliko ya sheria hii yaliletwa kwa ajili ya kukidhi haja ya yale yaliyotokea mwaka 2001 huko Pemba. Hata hivyo kama tulivyoshuhudia sisi sote hali hiyo haikusaidia kubadili dhamira na maamuzi ya wananchi wa Pemba. Hata pale palipowekwa mizengwe na mbinu hapakuzuia maruhani kupata kura na hivyo kuujengea Upinzani sifa ambayo haitafutika kamwe katika historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina imani kuwa kwa kuwa waamuzi wa mwisho daima ni wapigakura, mbinu na mikakati inayofanywa hapa au inayoweza kufanywa, ni matukio tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka kulipa Bunge hili heshima zake, ni vizuri tukarejesha sheria ya awali ili shughuli za uchaguzi zitegemee na zifuate sheria kuliko zikaendeshwa kwa kutegemea Maazimio tu yanayotegemea maslahi ya watu fulani au kundi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hapa sina mwingine aliyeomba kuchangia, sasa namwita Mheshimiwa Waziri amalizie hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kujumlisha hoja hii ambayo nimewasilisha Bungeni bahati nzuri ameongea mtu mmoja tu, Kiongozi wa Upinzani.

Sitaki niingie katika malumbano ambayo Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, anataka tuingie lakini nataka kusema kwamba Azimio hili sio la kwanza kuja hapa Bungeni na Azimio kama hili limesaidia pia Kambi ya Upinzani kuwa na Wabunge wengi.

Kwa hiyo, nafikiri Wapinzani wangemlaumu sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kwamba hataki Maazimio haya yaje hapa ili Wapinzani wawe wengi Bungeni. Lakini nafikiri nia yetu katika azimio hili ni nzuri. Tumepata Wabunge wengi sana kutoka *CUF*, tumepata Wabunge wa *CCM* kwa hiyo madhumuni yetu kwa kweli ni kuimarisha demokrasia ndani ya nchi yetu. Waamuzi wa mwisho ni wapiga kura, tusiwaseme hapa wapelekewe Wabunge wataamua nani kama *CCM*, *CUF*, *CHADEMA* kwa hivyo waamuzi wa mwisho ni wapiga kura tusiwanyime haki yao hiyo. Iko ruksa kabisa kama chama hakitaki kushiriki kiache, kisishiriki na Chama changu kitaweka wagombea pale. Kwa hiyo, tutafurahi sana kama Wapinzani watagoma ili Chama changu kipite bila shida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme madhumuni makubwa ya Azimio hili ni kuimarisha demokrasia ili kuwapatia wananchi wawakilishi halali katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili Wabunge watakachaguliwa waje watetee maslahi ya wapiga kura wao.

Sasa hivi kuna miradi mbalimbali ya *TASAF*, *MMEM* na kadhalika nani atawasemea kama sio Wabunge? Sasa hivi kuna upungufu wa chakula kwa hiyo lazima Wabunge wawe mstari wa mbele kuwasemea ili kupata chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwamba tatizo letu na Kambi ya Upinzani siku zote wanapinga tu hata kama ni jambo jema wao wanapinga tu, hili ni jambo jema kwa Upinzani kwa sababu Wapinzani wamefukuzwa nafasi ipo waingie hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoomba Wabunge wote pamoja na Upinzani muunge mkono hoja hii ili Watanzania wapate haki yao ya demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Azimio la Bunge Kuruhusu Kuwahi kwa Siku ya Uteuzi wa Wagombea Ubunge katika Chaguzi Ndogo za Majimbo yaliyowazi ama yatakayokuwa wazi kati ya Novemba 2003 na Oktoba, 2004 lilipitishwa na Bunge)*

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya National Microfinance Bank wa Mwaka 2003 *(The National Microfinance Bank Limited Incorporation (Repeal) Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya *National Microfinance Bank (The National Microfinance Bank Limited Incorporation Act, 1997* na marekebisho yake, sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kwa niaba ya Serikali, kutoa shukrani zangu za dhiti kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, tumezingatia maoni, ushauri, mapendekezo na maudhui ya Kamati na kwamba baadhi yake tumeyaaanisha katika jedwali la marekebisho *(Schedule of Amendment)*, ambalo naamini Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kulisoma. Aidha, mapendekezo mengine yatafanyiwa kazi ipasavyo katika hatua za kukamilisha ubinafsishaji wa Benki hii hususan katika matangazo ya kukaribisha wawekezaji *(The Information Memorandum)*, katika Mikataba ya mauzo na Mikataba ya wanahisa. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, ambao kwa nyakati tofauti wametoa ushauri na mapendekezo yao ambayo yamesaidia sana katika kuukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada, mapendekezo ya Muswada huu pamoja na marekebisho yake ninayoleta mbele yenu yana nia ya kuweka mkakati thabiti wa kubinafsisha Benki ya *NMB* na hatimaye kuwezesha wananchi wa Tanzania kumiliki hisa katika Benki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati unaoambatana na Muswada huu ninaouwasilisha mbele yenu una malengo makuu yafuatayo:-

(a) *NMB* inahitaji mtaji mpya wa kutosha ili iweze kuwa na uhimili wa kutoa mikopo mingi kwa wakulima na wafanyabiashara hasa wadogo wadogo. Benki inahitaji kufikia mtaji wa shilingi bilioni 27 kama nguzo ya amana za takriban shilingi 395 bilioni zilizomo.

(b) *NMB* inahitaji kupata wawekezaji wenye utaalam wa kileo wa kibenki wenye kuaminika na waadilifu.

(c) Wawekezaji wenye uzoefu wa uongozi wa kibenki na watoaji wa mikopo midogo midogo (*Microfinance*) na pia uendeshaji wa Benki ya Biashara (*Commercial Bank*) yenye matawi mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja kubwa ya kuendelea kuwa na uongozi imara katika Benki hii utakaobuni njia mpya za kuongeza mapato ya matawi 37 yanayotoa faida ndogo na yale 15 yanayopata hasara hivi sasa. Aidha, uongozi huo utatakiwa kuwa na utaratibu mzuri wa utendaji na udhibiti wa hasara inayoweza kutokea kutokana na hali ya biashara au misukosuko mbalimbali, kuna umuhimu wa kupata wawekezaji wenye uwezo wa kuweka na kuongeza mitaji mara utokeapo mtikisiko wa aina hiyo, jambo ambalo ni rahisi sana kutokea kwenye benki kwa mfano wizi, uporaji kwenye biashara za nje au fedha za kigeni. Inajulikana duniani kote kuwa biashara ya kukopesha wateja wadogo ni ghali na nyeti (*risk*) na ndiyo sababu ya riba kubwa zinazotowza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NMB* bado ipo katika harakati za kutafiti njia bora za kutoa na kudhibiti mikopo hasa Vijijini. Hadi mwisho wa Septemba 2003, *NMB* ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. 18.7 bilioni kulinganisha na amana zake za Sh. 395 bilioni. Hivyo basi, mtaji mkubwa, teknolojia ya kisasa na utaalam katika masuala ya utoaji wa mikopo hasa midogo midogo, ni muhimu sana ili kuwezesha Benki kuwekeza kiasi kikubwa cha amana zinazoshikilia sasa kwa faida na wakati huo huo kudhibiti hasara inayoweza kutokea endapo baadhi ya mikopo hiyo haitalipwa, jambo ambalo linaweza kutokea kwa Benki yoyote. Aidha, *NMB* ina mtihani (*challenge*) wa kubaini aina nyingi za mikopo inayoweza kutoa zaidi ya ile ya *Microfinance* kwa vile ina kiasi kikubwa cha amana ambacho kinahitaji kuwekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki zinazotoa mikopo kutokana na amana za wananchi, yaani watu na makampuni mbalimbali zinahakikisha kila senti inayotolewa kama mikopo ina uwezekano wa kurudishwa au kutorudishwa. Kama sehemu kubwa ya mikopo isiporudishwa na wakopaji Benki inaweza kuanguka. Ili kuwa na kinga ya kutosha kuhimili uwezekano wa mikopo kutorudishwa Benki yoyote inahitaji mtaji wa kutosha. Ili kuzuia mikopo mibovu isitolewe ambayo itashindikana kurudishwa, inahitajika menejimenti yenye uelewa na uzoefu wa kutosha na teknolojia ya kisasa. Menejimenti hiyo inapaswa pia iwe na uchungu na Benki inayoiongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NMB* inatakiwa iweke mkazo kwenye shughuli za *Microfinance* ili kuiwezesha Benki kuwa mahiri na kubuni aina mpya ya mikopo kwa wateja wa *Microfinance*. Kwa kuwa *NMB* inatoa huduma kwa kutumia matawi 108



ambayo yapo katika takriban Wilaya zote nchini na kwa kuwa katika baadhi ya Wilaya, *NMB* ndiyo taasisi pekee inayotoa huduma za kibenki, Benki hii inatarajiwa kutoa huduma za kibiashara na zile za *Microfinance* hususan katika maeneo yasiyo na Benki nyingine. Wajibu huu wa *NMB* unailazimu iboreshe teknolojia yake na utaalum wa kutoa huduma za Benki za Biashara kama vile huduma ya akaunti za hundi (*Cheque Accounts*), huduma ya fedha za kigeni (*Forex Account*) na huduma ya biashara ya nje (*Letters of Credit Facilities*).

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma hizi ambazo zipo zaidi katika Miji mikubwa zitachochea maendeleo ya wananchi kwa kuwa *NMB* ipo karibu nao kuliko Benki nyingine yoyote hapa nchini ukiondoa Benki chache za wananchi. Wafanyabiashara wadogo na wakulima watawezesha kupata huduma za Benki kwa ajili ya biashara zao. Kwa kuwa *NMB* ina amana nyingi na inakusudia kutoa mikopo mingi kwa wateja wadogo na wakubwa, inahitaji mtaji wa kutosha, teknolojia ya kisasa na menejimenti endelevu ambayo itakuwa na uchungu na Benki hii. Aidha, wananchi wamesubiri kwa muda mrefu sasa kupata huduma ya *NMB* kama walivyoahidiwa, kwa hiyo, Serikali inaamini kwamba, sasa ndiyo wakati muafaka wa kuibinafsisha *NMB*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, Serikali kupitia Muswada huu inapendekeza kwamba, mkakati wa kubinafsisha Benki hii uwe kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iuze asilimia 49 ya hisa zake katika *NMB* kwa muungano wa wawekezaji (*Consortium of Investors*) wakiongozwa na Benki ya Biashara kama *strategic investor* lakini ziwemo pia Benki au Taasisi za *Microfinance*. Aidha, katika tangazo la kukaribisha wawekezaji, itamkwe bayana kwamba, wawekezaji watakaokuja na mkakati mahiri unaoshirikisha Watanzania, watapewa kipaumbele. (*Makofi*)

(b) Asilimia 51 ya hisa zinazobaki zigawanywe kwa Watanzania tu kama ifuatavyo: Kwanza, asilimia 21 ziuzwe kwa mwananchi mmoja mmoja au katika vikundi. Aidha, wafanyakazi wa *NMB* watapewa fursa ya kununua hisa kama watataka. Pili, asilimia 30 itabaki Serikalini mpaka hapo itakapoamuliwa kuwauzia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa namna ya pekee kuishukuru Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa *NMB*, kwa kazi kubwa na nzuri waliyofanya ya kuifikisha Benki hii katika hatua hii muhimu. Serikali inaamini kwamba, mkakati huu ni mzuri na unatekelezeka (*doable strategy*), umezingatia mahitaji ya mtaji wa kutosha kwa *NMB*, umuhimu wa kuwa na wawekezaji mahiri wenye utaalum na menejimenti endelevu ya kuendesha mtandao mkubwa wa Benki itakayotoa hasa mikopo midogo midogo na watakaoboresha teknolojia na unaiweka Benki mikononi mwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine za mkakati huu ni kwamba, unazingatia umuhimu wa kuwapa wananchi wakiwemo wafanyakazi wa *NMB*, fursa ya kuwekeza katika Benki hii kwa kupitia mkondo wa *Public Offer* mapema iwezekanavyo baada ya kuuza hisa kwa muungano wa *strategic investors*. Aidha, mkakati huu unazingatia umuhimu wa Serikali kuendelea kushikilia sehemu kubwa za hisa za *NMB* ili iweze kuwa

na ushawishi katika uendeshaji wa shughuli za Benki kwa lengo la kuhakikisha kwamba, matawi hayafungwi bila sababu za msingi na huduma za *Microfinance* zinaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, lengo la Muswada huu ni kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha *NMB* kubinafsishwa ili wananchi hasa wa Vijijini waweze kupata huduma muhimu za kibenki ili kujiondolea umaskini. Kwa maneno mengine ni kusema kwamba, Serikali katika Muswada huu inaomba kitu kinachoweza kufananishwa na daraja ili iweze kuvusha *NMB* hapa tulipo na kuipeleka ng'ambo ya pili ya mto tunaovuka. Kwenye ng'ambo ya pili *NMB* itakuwa kampuni iliyoandikishwa kwa utaratibu wa Sheria za Makampuni (*Limited Liability Company*). Hapa ilipo inaendeshwa kwa sheria mbili, sheria iliyoitunda *Microfinance* ambayo tunaomba ifutwe na sheria iliyounda *National Bank of Commerce* ya mwaka 1997 ambayo pia tunaomba irekebishwe. Sheria hizi zikisharekebishwa *NMB* itabaki ni *Limited Liability Company*, ambayo sasa itakuwa tayari kuuzwa kwa utaratibu ambao nimeeleza wa asilimia 49 kwa wawekezaji mahiri (*Strategic Investors Consortium*) na asilimia 51 kati ya hizo, kuchukua asilimia 21 kuuzia wananchi na asilimia 30 kubaki Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. NJELU E.M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Ubinafsishaji wa *National Microfinance Bank (NMB)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati kuhusu ubinafsishaji wa *The National Microfinance Bank* kwa kufuta sheria iliyoanzisha *NMB (The National Microfinance Bank Incorporated Limited, Act No. 22 of 1997)* ili *NMB* ibakie chini ya Sheria ya Makampuni (*Companies Act*) na kufanya marekebisho katika Sheria ya *The National Bank of Commerce, Reorganization and Investing of Assets and Liabilities Act, 1997* ili hisa za *NMB Limited* sasa ziweze kumilikiwa moja kwa moja na msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge ambao siyo Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kuhudhuria na kushiriki katika kujadili Muswada uliotajwa hapo juu na kwamba naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Idd Simba, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa

Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Omar J. Omar, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Dr. Deodorus Kamala, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Hasnain Murji, Mheshimiwa Mosi Suleiman Musa, Mheshimiwa Issa Mohammed Salim, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa Nazir Kalamagi, Mheshimiwa George Francis Mlawa, Mheshimiwa Henry Shekiffu na Mheshimiwa Ibrahim Marwa. Wote nawashukuru kwa michango yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati haina kipingamizi na hoja ya Serikali ya kubinafsisha *NMB* kwa kuzingatia mabadiliko yaliyofanywa katika sheria zilizoanzisha katika sehemu ya utangulizi hapo juu na pia kwa kuzingatia mashauriano na maoni mbalimbali yaliyokuwa yakitolewa toka hoja ya kubinafsisha *NMB* ilipoanzishwa. Aidha, kusudio hili limefika katika wakati muafaka sambamba na kutekeleza sera mbalimbali za kiuchumi na fedha za kufufua uchumi wa nchi katika kuleta maendeleo ya watu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kamati kutokuwa na kipingamizi na hoja hii kwa Serikali, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

Kamati imesisitiza kuwa pamoja na nia nzuri ya kubinafsisha *NMB*, kwa kuwa Benki hii ina matawi yake nchi nzima na ndiyo Benki pekee inayotegemewa na wananchi wengi walio wafanyabiashara wadogo wadogo na wakubwa, basi azma hii iwekwe wazi katika sheria hii kuwataka hao watakaowekeza katika Benki hii kuifahamu vema dhana ya *Microfinance*. Serikali imeshauriwa na imekubali kuhakikisha kuwa malengo na madhumuni ya *Microfinance* yanadumishwa na kuendelezwa. Kwa kuzingatia hili, Serikali imeshauriwa isijitoe upesi katika umiliki wa *NMB* ili kuona kuwa uwekezaji unaendeleza malengo ya Benki hii kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesisitiza pia Serikali iwe karibu sana na Benki hii kwa kuhakikisha kuwa mtaji wa kutosha unawekezwa, kunakuwepo uongozi wa kibenki wenye uzoefu mkubwa, yaani *management* na Benki iweze kuendesha shughuli zake kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Aidha, Kamati imesisitiza itamkwe wazi kuwa wawekezaji watakaopatikana kutoka nje washirikishe vikundi mbalimbali kama vile *SACCOS*, *Community Banks* na Benki nyingine ambazo zinamilikiwa na Watanzania na wawekezaji wengine wa ndani katika umiliki wa hisa zinazotengwa kwa upande wa mwekezaji binafsi yaani hizo asilimia 49. Kwa kuwa Serikali ina nia ya kuleta Muswada wa uwezeshaji na pia ina mkakati wa kupunguza umaskini, Kamati imeitaka Serikali kueleza wazi ni jinsi gani sera ya uwezeshaji na mkakati wa kuondoa umaskini vitafanikiwa bila ya kuwa na Benki kama *National Microfinance Bank*. Sera ya uwezeshaji na mpango wa kuondoa umaskini hauwezi kupata mafanikio makubwa bila kuwa na chanzo cha upatikanaji mikopo kwa wenye sifa za kukopa na ambao ni wahusika wa programu hiyo ili waweze kuendesha shughuli zao kama ambavyo Serikali inakusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshauri pia mara baada ya ubinafsishaji kwa *NMB* lengo liwe la kukuza mtaji kwa kuelekeza kwamba kusiwe na gawio litakalotokana na faida ili baadaye benki iweze kuwa na mtaji mkubwa na kutoa mikopo kwa wingi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo katika nyanja zote za kiuchumi. Kwa kuwa wafanyakazi waliopo katika *NMB* ni wale wale waliotoka katika iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara na baadhi wameshaajiriwa na ndiyo waliyoifikisha *NMB* hapo ilipo. Hivyo, Kamati imeshauri wafanyakazi hao wapewe fursa ya kumiliki kiasi fulani cha hisa mara taratibu za ubinafsishaji zitakapokamilika na nashukuru kwamba, Waziri amelitaja hilo na kwamba wafanyakazi watapewa fursa ya kununua hisa hizo mara taratibu zikikamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa *NMB* katika matawi yote nchini kwa kuwa watulivu na kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi licha ya malumbano yaliyokuwa yakiendelea juu ya hatma ya ubinafsishaji wa *NMB*. Aidha, Serikali inashauriwa kusaidia wafanyakazi wafanye makubaliano ya Mkataba wa hiari na menejimenti ya *NMB* ili kuboresha mafao yao, ajira yao itakapokoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ilivijadili vifungu vyote vya Muswada vinavyokusudia kubinafsisha *NMB* na kuupitisha Muswada huo baada ya majadiliano ya kina na magumu ingawa yote yalilenga katika kuboresha mgawanyo wa umiliki kati ya atakayekuwa mwekezaji binafsi na zile za upande wa Serikali. Hapa ningependa kusema ilifika mahali katika majadiliano tukatumia na busara ya Mfalme Solomon katika maandishi matakatifu. Mfalme Solomon nasikia kuna akina mama wawili walikuwa wanagombea mtoto, walifika mbele yake kila mmoja akidai kwamba yule mtoto ni wa kwake na yeye katika kuamua kwa kuwa alikuwa hajui nani mwenye mtoto, basi akaamua kwamba mtoto yule akatwe vipande viwili na kila mwanamke abebe kipande chake. Mama mmoja akakubali kwamba kweli akatwe tugawane, lakini yule aliyekuwa ndiye mwenye mtoto alikataa, akasema ni bora aende akiwa hai kwa mama wa kambo kuliko kuona anakatwa vipande vipande. Kwa hiyo, Kamati ya Fedha ilifika mahali baada ya Serikali kusema kwamba Benki hii isipobinafsishwa itakufa, basi Kamati iliona ni vema ipone ikiwa mikononi mwa mama wa kambo kuliko kufa mikononi mwa Kamati ya Fedha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauri kuwa Serikali iendelee kuwa na kauli katika *NMB* ama kwa kuwa na hisa nyingi au kuwa na hisa ya turufu (*Golden Share*). Utaratibu wa kutumia *golden share* umefanyika vizuri tu katika nchi nyingi kama vile Uingereza, Marekani, Urusi, Uchina na kadhalika. Kwa hiyo, tulifikiri kwamba nchi yetu katika masuala kama haya, inaweza kuendelea kuwa na nguvu katika *NMB* kwa kutumia *golden share* na kwa maana hiyo hizo hisa asilimia 30 inaweza kuziua kwa wananchi mapema zaidi na yenyewe ikabakia na hisa ya turufu na kwa hiyo kupanua umiliki wa wananchi ndani ya *NMB* kama ambavyo tunakusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kukubali kuwa wakati wa kuuza hisa zinazomilikiwa na Serikali zitauzwa kwa wananchi na taasisi zinazomilikiwa na Watanzania. Hii itapanua umiliki wa Watanzania katika *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutamka kuwa Kamati inakubaliana na madhumuni ya Muswada huu. Ahsante sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya *National Microfinance Bank* ya Mwaka 1997 na kufanya marekebisho katika Sheria iitwayo *The National Bank of Commerce Reorganization and Investing of Assets and Liabilities* pia ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo nayafanya kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge Toleo la mwaka 2003, kifungu cha 70(4). Kabla ya yote napenda kuwasilisha masikitiko ya Kambi ya Upinzani jinsi Serikali ilivyoshinikiza ubinafsishaji wa *National Microfinance Bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa ni msingi wa demokrasia kwa makubaliano kufikiwa baina ya Bunge na Serikali, ni vema ieleweke kuwa *NMB* imeathirika sana kutokana na malumbano ya muda mrefu baina ya vyombo hivi viwili. Matamko mbalimbali mengine yakiwa hayajapata ridhaa ya Kamati mbalimbali na vikao mbalimbali vya Bunge yameathiri *National Microfinance* kwa kiwango kikubwa na yameongeza hasara kwa Benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, shinikizo hili la Serikali kwa upande wa pili linaashiria Serikali kutoshauri ushauri wa Wabunge na kama siyo hivyo, basi kunajengeka hisia kubwa miongoni mwa Wabunge na hata wananchi kwa ujumla kwamba, pengine kubinafsisha Benki hii ya *National Microfinance* kunatokana na shinikizo na msukumo wa ziada kutoka nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma sababu mbalimbali zilitolewa na Serikali kuhusu kwa nini imepania kubinafsisha Benki hii muhimu ambayo imekuwa ikitoa huduma kwa Watanzania wengi kuliko Benki nyingine yoyote ile hapa nchini. Sababu za msingi zilizotolewa nyuma ni pamoja na:-

- (a) Suala la ubinafsishaji ni sera ya nchi.
- (b) Benki yenyewe haina mtaji au utaalum au teknolojia ya kutosha.
- (c) Benki hii inaendeshwa kwa hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na kitendo hiki cha kuitelekeza Benki ambayo imekuwa na mtandao mkubwa na ulioingia zaidi Vijijini kuliko Benki nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya nchi ya ubinafsishaji ambayo vile vile inalenga kuiondoa kabisa Serikali katika biashara na kuendesha moja kwa moja shughuli zote za kiuchumi katika siku si nyingi, itaiingiza nchi yetu katika utegemezi usio na kifani hususan katika huduma za kibenki. Aidha, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuwa suala la *NMB* lisiangaliwe kibiashara zaidi ila mtazamo uelekeze zaidi kwenye huduma za kibiashara kwa wananchi wenye kipato cha kati na kipato cha chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema vile vile ikaeleweka kuwa kwa ujumla wake Kambi ya Upinzani haina tatizo na sera ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma yanayoendeshwa kwa hasara na hata pengine kwa faida. Hata hivyo, tunapinga kwa nguvu zote tabia au sera ya kubinafsisha kila kitu vikiwemo vile ambavyo vinaonekana wazi kwa kufanya hivyo wananchi walio wengi wataathirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya kubinafsisha *National Microfinance Bank* ni kuwa huduma za Benki nchini kwa zaidi ya kiwango cha asilimia 75 zitakuwa zinamilikiwa na Benki za kigeni au wanahisa wa kigeni. Hali hii si ya hatari kwa usalama wa uchumi wetu tu bali ni hatari kwa wananchi wengi wa Mikoani, Wilayani na Vijijini, ambao kwa sasa wanatumia huduma za *National Microfinance Bank*. Wawekezaji wa nje wana kusudio moja tu nalo ni faida, nao hawana huruma na Mtanzania yeyote asiyeweza kuwapatia faida iliyowaleta Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waziri kutupa maelezo kuwa Serikali inakusudia kubinafsisha Benki hii ili iweze kutoa huduma ikiwepo mikopo midogo midogo na mikubwa nchini ikiwemo huko Vijijini. Aidha, vile vile kupata utalam wa kisasa na vile vile kupata uongozi wenye uzoefu wa kibenki, tunapenda kuishauri Serikali kuwa azma hii inaweza kutimia bila hofu yoyote kama kimsingi Serikali haitajivua wajibu wake wa kuwahudumia wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la Serikali kumiliki asilimia 51, nikizungumzia hapa nazungumzia Serikali kwa ujumla kwamba, Serikali na wananchi wa Tanzania ambao watauziwa hisa hizi kwamba pendekezo hilo kwamba asilimia 51 zitabaki Tanzania na pengine wawekezaji wa nje hao *strategic investors* watapatiwa asilimia 49 ya hisa za *National Microfinance* pamoja na tamko kwamba Watanzania vile vile wanaweza kuwa sehemu ya hawa *strategic investors*, ni kigezo tosha cha kuendeleza *NBC* kutumia vigezo hivyo na mgawanyo huo kwamba, ndicho kigezo pekee cha kuweza kuendeleza *National Microfinance Bank*, kwetu Kambi ya Upinzani tunakiona kwamba ni mtazamo potofu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachojitokeza hapa ni Serikali kutafuta mbinu yoyote ili Wabunge wakubaliane na azma ya kubinafsisha Benki hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa ubinafsishaji wa baadhi ya Mashirika muhimu ya umma umedhihirisha kuwa Serikali yetu ama kwa makusudi ama kwa kutokujua, imeruhusu wawekezaji kuchukua miliki ya uendeshaji wa Mashirika haya pamoja na wao kuwa na hisa kidogo. Mfano halisi ambao umekuwa ni kero kubwa na

ninaweza kusema ni *embarrassment* tosha kwa Serikali ni suala la ubinafsishaji wa Kampuni ya Simu (TTCL).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajua wazi kuwa kama Bunge hili litapitisha leo Muswada huu ndiyo utakuwa mwisho wa Waheshimiwa Wabunge kuuliza masuala na mstakabali wa *National Microfinance*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ukipitishwa maana yake ni kuwa sasa *National Microfinance Bank* itatawaliwa na Sheria ya Makampuni kupitia *Memorandum and Articles of Association* ambayo katika mazingira ya usiri wa Serikali hii, Bunge lako kamwe halitaona. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya *Memorandum and Articles of Association*, ukweli ni kuwa hatma ya maslahi ya nchi hii kwenye *National Microfinance Bank* itakuwa kwenye Mkataba wa uuzaji wa hisa yaani *Sale Agreement*. Mikataba hii ya uuzaji imekuwa siri kubwa na kwa maana hiyo ni vyema Waheshimiwa Wabunge leo kwa ujumla wetu bila kuangalia tunatoka Vyama gani, tuelewe kuwa kupitisha Muswada huu katika mazingira yalivyo kwa hakika tumeitosa *National Microfinance Bank* na kamwe hatutakaa tujue ukweli wake tena. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu uzoefu umetuonyesha muda mrefu kwamba, pindi mikataba hii inapoingwa Bunge linatumiwa kutunga sheria na Bunge likishatunga sheria halina tena mamlaka ya kuuona mkataba au kushauri kuhusu dondoo za Mkataba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huu basi nia njema yote iliyoelezwa na Serikali hapa, Bunge hili tangu leo litakuwa halina uwezo wa kujua kama kweli yametimizwa kwa sababu litakuwa halina kikao wala uwezo wa kuita mkataba ambao ndiyo utaonyesha hatma ya *National Microfinance Bank*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa upande mwingine inasikitishwa na kutoshirikishwa kwa *management* ya *National Microfinance Bank* katika hatua hizi za mwisho za ubinafsishaji. Taarifa mbalimbali zilizoletwa zimetoka upande mmoja wa Serikali. Katika vikao vyote vya Kamati ya Fedha vilivyotangulia kabla ya Muswada huu kuwasilishwa leo Bungeni, uwakilishi wa aina yoyote kutoka kwa *National Microfinance* tunasikitika haukuwepo na hili linapelekea Kambi ya Upinzani kuwa na hofu kwamba, Serikali imependa kulibeba hili suala yenyewe na kuwatenga wadau muhimu ambao ni wafanyakazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine taarifa za ndani ya *National Microfinance Bank* zinasema kuwa wafanyakazi ambao ni zaidi ya 1,100 wana wasiwasi hasa kutokana na ukweli kuwa hawashirikishwi kwenye zoezi hili na hawajui hatma yao. Aidha, wafanyakazi wanasikitika kuwa hawajasainiwa mkataba wa hiari na mwajiri wao na wala hawajui watasainiwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejenga hoja kuwa kama siyo kutoa huduma kwa Serikali, *NMB* itakufa pamoja na kutoupinga ukweli huu, nia yetu ni kuikumbusha Serikali kuwa kwa kuipa nafasi *National Microfinance Bank* siyo fadhila bali ni wajibu wake. Hatutegemei Serikali yetu ipeleke biashara kwa Benki za nje wakati kuna Benki zake zenye uwezo wa kutoa huduma hizo sana sana tunategemea Serikali iongeze biashara kwa *National Microfinance Bank*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba, huduma ya Benki ya *National Microfinance* ni muhimu kwa Watanzania wa kipato cha kati na ni muhimu hasa kwa utumishi na wafanyakazi wengine wa Serikali ambao wako katika maeneo mengine ambayo huduma hizi za kibenki haziwafikii. Serikali itastahili na itawajibika kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, itatumia mbinu gani kuwalazimisha wawekezaji hawa ili waweze kupeleka huduma zaidi vijijini na sehemu zingine za Wilayani ambako bado hata hiyo *NMB* yenyewe haijafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba, Serikali iendelee kubeba jukumu la kuisimamia na kuilinda *National Microfinance Bank*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Kambi ya Upinzani inakubali kwamba, *National Microfinance Bank* inahitaji kuongezewa mtaji na vilevile inahitaji kupata teknolojia ya kisasa. Ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba, kama Serikali itauza asilimia zisizozidi 30 kwa wawekezaji wa nje ambao vilevile wanaweza wakapewa jukumu la *management* lakini chini ya uangalizi wa karibu wa Serikali basi Benki hii itaweza kuendelea kufanya lile lililokusudiwa pale ilipoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni maoni ya Kambi ya Upinzani kwamba, asilimia 70 ambayo itabaki kama hisa za Serikali, Serikali itoe asilimia 30 kwenda kwa wadau mbalimbali wa ndani ya nchi zikiwemo Taasisi za Fedha za ndani na Serikali yenyewe iendelee kubaki na asilimia 40 na kwa maana hii, Serikali bado itakuwa na hisa kubwa na uwezo wa moja kwa moja wa kuisimamia Benki hii ili iendelee kutoa huduma kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna imani kabisa kwamba, Serikali kama ingekuwa na nia na dhamira ya dhati ya kuikomboa *NMB*, ina uwezo wa kuiwezesha Benki hii kuimarika na kwamba kufa kwa *National Micro-Finance Bank* leo au kuzorota kwa *National Microfinance Bank* leo ni mkakati wa pengine wa kutokujua ama wa makusudi wa Serikali kuhakikisha kwamba, Benki hii inadhoofika ili iweze kuuzika kama sababu, lakini bado tuna imani kabisa kwamba, Serikali ina wajibu wa kuisimamia *National Microfinance Bank* na Benki hii ama Taasisi hii muhimu iweze kuendelea kutumika katika mkakati mzima wa Serikali wa kuondoa umaskini, sera ambayo tunaisubiri iletwe ya namna Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha wazawa kuweza kumiliki uchumi wao wakati wazawa wenyewe wamepokonywa Taasisi zote za fedha ambazo ni nyeti na muhimu katika kuwawezesha kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyazungumza hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)



**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hapo awali, tunao wachangiaji hivi sasa 20 na muda tulionao ni kuanzia sasa mpaka saa 10.14 jioni ili kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri aweze kuhitimisha hoja yake. Baada ya hapo tutakwenda kwenye Kamati na baada ya hapo hoja ya kuahirisha Bunge itatolewa ili kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kuahirisha Bunge na nimepanga Mheshimiwa Waziri Mkuu apate nafasi saa 11.00 jioni. Kwa hiyo, saa 11.00 jioni tuwe tumemaliza shughuli zote ili Bunge liahirishwe saa 11.00 jioni ili kumpa saa moja Mheshimiwa Waziri Mkuu kumalizia hotuba yake ya kuahirisha Bunge.

Sasa wachangiaji wako 20 kama nilivyosema, tutaishia pale ambapo muda umekwisha. Nawaomba sana sana kila mmoja ajaribu kubana muda na wa kwanza ni Mheshimiwa Jacob Shibiliti, atafuatiwa na Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Musa Lupatu na Mheshimiwa Ibrahimu Marwa. Nimewataja hao 10 ili waweze kujiandaa na kadri muda unavyosogea nitawataja na wengine. Sasa namwita Mheshimiwa Jacob Shibiliti.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Makatibu Wakuu wote, kwa jinsi walivyoweza kurekebisha Muswada huu na kuletwa katika sura ambayo sasa inakubalika katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umefikia hatua hiyo baada ya marekebisho ambayo yamefanyika yanayoleta picha ya kwamba, sasa suala hili linawezekana sasa angalau kutokana na hali halisi. Sera ya Ubinafsisaji ni Sera ya Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo ni vema itekelezwe katika misingi ambayo Chama chetu kwa kweli kimefikia mahali kinaweza kuonyesha picha ambayo wananchi wake wanakuwa na imani na Chama chao na matunda tunayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, kabla ya yote niunge mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja upitishwe. Kwa sababu umesema wachangiaji ni wengi na kila mmoja anaweza kugusa hapa na pale, mimi nigusie machache na wenzangu niwaachie nafasi ili nao waweze kuchangia kwenye maeneo mengine nitakayokuwa nimeyabakiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu mno ndiyo maana umerudi kwa mara ya pili baada ya kuwa na sura ambayo sasa inatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya kwanza Muswada huu ulikuwa na sura ambayo kwa kweli ilikuwa haiwagusi wananchi walio wengi, lakini baada ya kukaa

wataalamu na kuurekebisha na kusema asilimia 51 ni za wananchi wa Tanzania, hapo nawapongeza sana ni sura ambayo inatupa picha ya kwamba sasa tutashiriki kikamilifu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tahadhari ambayo ningependa niitoe kutokana na matawi na mtandao iliyonao Benki hii uendelezwe pasitokee tawi hata moja la kufungwa. Matawi yote yalivyo yazidi kuendelezwa na baadaye ikiwezekana yaongezwe mengine ili angalau wananchi waweze kupata huduma muhimu karibu na maeneo yao ya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia suala la kuongeza matawi kwa sababu ziafuatazo: Kumekuwa na msongamano wa watu wengi hasa katika Wilaya mbalimbali, Vyama vya Ushirika vingi vimekuwa vikihangaika namna ya kuchukua fedha na kuzipeleka kwa wananchi wake. Wanaomba sana wananchi wengi walioko katika maeneo mbalimbali Benki zizidi kuwasogelea ili huduma zao ziende vizuri zaidi. Kwa hali hiyo huduma hii ikiboreshwa wananchi wengi watafaidika na kutokana na hali halisi ya jinsi Muswada ulivyowekwa, nina imani utapata marekebisho yaliyo mengi kutokana na michango tunayoitoa hapa ili wananchi waweze kufaidika na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa niligusie ni jinsi mikopo mikubwa itakavyozidi kutolewa kwa wahusika wengine ambao wana shida ya mikopo kwenye maeneo yako ili waweze kuzalisha. Suala la mikopo kwa wakulima wadogo wadogo linahitajika si mikopo midogo midogo kama ilivyokuwa inatolewa jinsi alivyoweza kueleza Mheshimiwa Waziri kwamba, mikopo inayotolewa sasa hivi na Benki yetu hii ni mikopo kwa kweli ambayo ni midogo midogo, shilingi 50,000/= au Sh. 100,000/=, haitoshi. Sasa tuiboreshe zaidi mikopo hii ili iweze kuwasaidia wakulima wadogo wadogo na wenyewe waweze kuinua maisha yao na itolewe bila matatizo yoyote kwa wahusika hao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kilio changu kikubwa kilikuwa ni hicho, wananchi wakumbukwe katika Benki hii na baadaye nao waweze kunufaika na Benki hii. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Maafisa mbalimbali, walioshiriki katika kuleta Muswada huu hapa ambao nafikiri umekuja kwa muda muafaka. Kwa hiyo, natanguliza kusema kwamba, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulivyofika hapa kwa wakati huu umeshirikisha wadau wote na umehakikisha kwamba matarajio ya kila mdau yake yamefikishiwa. Kwanza, mdau kama Serikali, umehakikisha kwamba umerekebisha Benki hii na kuiwekea mitaji ya kutosha na kuiwekea *management* ya kutosha kusudi kuifanya Benki hii iwe nzuri na *attractive* kwa kuweza kuiuza. Nafikiri kwa kipindi hiki wameweza kufanya hivyo na tunajivunia walipoifikisha Benki hii, la sivyo ingekuwa katika hali mbaya sana. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali inataka kuiua Benki hii,

kama ingekuwa inataka kuiua Benki hii isingeweka mtaji mkubwa na kuweka fedha za walipa kodi kama ruzuku kuifikisha hapa ilipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetangaza waziwazi kwamba, inataka kukaa ndani ya *NMB* kama mwekezaji ili kuhakikisha kwamba huduma na hizo fedha ambazo imeziwekeza kama ruzuku mpaka sasa hivi hazipotei, kwa njia hiyo Serikali inaonekana kwamba, ina nia nzuri kama mdau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watarajiwa wengine ambao ni wawekezaji. Matarajio ya wawekezaji ni kupata faida na ili wapate faida lazima wafanye hii Benki ifanye kazi kwa ufanisi, kwa hiyo lazima wataweka *capital*, wataweka teknolojia nzuri na wataweza kufungua matawi mengi, kwa sababu bila ya kufanya hivyo hawatapata ile faida ambayo inatakiwa kupatikana. Kwa hiyo, kwa kuleta *management* nzuri na teknolojia nzuri na mtaji, nafikiri hii Benki itakuwa ni nzuri kwa Kitaifa lakini itakuwa inawahakikishia wale wawekezaji wa nje na hata wa ndani kwamba, hii Benki itapata faida kusudi na wenyewe waweze kupata gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja imetokea ya kutopata gawio, sijawahi kuona *investor* yeyote hapa duniani labda *donor* ama Serikali tunaita ruzuku unaweza kuwekeza usipate faida ama gawio, usipopata gawio sijui hiyo utataitaje, siyo *investor*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu ambacho kinatugusa sisi Waheshimiwa Wabunge wote tulioko hapa kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi kwa hiyo tunawasemea wananchi kwa ujumla. Hicho ni kitu cha huduma kuhakikisha kwamba, huduma inapatikana kwa urahisi na kote nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutumia nafasi hii kuwaambia nimesoma ama nimeangalia mahali fulani kwamba, *NMB* ina matawi 108, matawi 37 yanapata faida kidogo na matawi 15 yanapata faida kidogo. Lakini tunajua kwamba kwa kuweka *capital*, *management* nzuri, teknolojia inaweza kuwa *turn around*. Nina nataka kuwaambia tunazungumzia wananchi, mimi katika Jimbo langu la Bukoba Vijijini, hakuna tawi hata moja la *National Microfinance Bank*, matawi yapo katika miji midogo na miji mikubwa. Sasa kwa kufanya matawi yakaweza kusambaa vijijini na sisi Waheshimiwa Wabunge tunasema yafike vijijini kwa sababu kwa sasa hivi hayapo tunataka yaende vijijini, naona itakuwa ajabu kama sisi wawakilishi wa wananchi kama tutakataa hili la kuyasambaza matawi ya Benki mpaka yafike huko vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo inabidi tuangalie sisi Waheshimiwa Wabunge, Benki maana yake nini na inafanya nini? Benki ina-*mobilize resources* katika sehemu mbalimbali na kuziwekeza. Sasa kitu cha muhimu tulichopaswa kuangalia hapa hizo *resources* ambazo ziko *mobilized* zinawekezwa wapi na tumefurahi wameshatuambia kwamba, katika hizo *MEMAT* na katika *Sales Agreement*, wataweza kuweka vifungu bayana vya kuhakikisha kwamba, hizi *resources* ambazo zitapatikana kipaumbele cha kwanza wanapewa wakulima, wavuvi, wafugaji na hao watu wadogo wadogo ndiyo shughuli ya *Microfinance Bank*. Sasa tusiweze kuinyima huu uwezo wa ku-*mobilize* na utaalumu wa kuziweka katika hii shughuli ambayo ni ngumu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nataka kuzungumzia juu ya *timing*. *Timing* ya kubinafsisha ni sasa hivi tusingoje kwa sababu ushindani wa kibenki sasa hivi ni mkali sana na teknolojia. Kwa sababu *National Microfinance Bank* watu wengi tunaikwepa kwa sababu inakuwa na watu wengi wa kuhudumia kwa gharama kubwa kwa hiyo Benki nyingi huwa zinapata hasara kwa kufuata watu. Lakini teknolojia ya sasa hivi inayoendelea ya *out banking electronic payments*, inafanya kazi ya kuwafikia watu wengi kwa njia rahisi. Sasa tukikosea wakati huu mbele ya miaka miwili, mitatu, hiyo teknolojia itakuwa kubwa sana kiasi kwamba haya majengo tuliyonayo, ambayo tunasema ndizo *assets* yatakuwa hayana faida yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa ufupi labda niishukuru tu Serikali kwa kuzingatia mambo yafuatayo katika hizo *Sales Agreement*: Wataangalia kwamba hii *NMB* itaendelea kufanya shughuli za *National Microfinance Bank* hata ikichanganya nyingine lakini lililo juu kubwa litakuwa ni *Microfinance* na pili katika *consortium* ile ile itahakikisha katika ile asilimia 49 itakayokuwepo kwamba wale wataokuwa katika *consortium* iwapo makampuni ya Kitanzania yatajitokeza na *lobbying* ipo kwamba zina sifa tosha, yale makampuni ambayo yatakuwa na *consortium* ya Watanzania na wa nje ama Watanzania watupu yapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nawashukuru sana kwa kuokoa muda.

**MHE. THOMAS S. NYIMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kukushukuru wewe uliyenipa fursa hii ya kuongea leo katika Muswada wa *NMB*. Kwanza, mimi nawapongeza sana viongozi, watumishi na watendaji wa *NMB*, wamefanya kazi nzuri, yenye heshima hata imetuwezesha kuwa na muda mrefu wa kujadili kuhusu Benki hii kwa niaba ya Watanzania. Nawapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hapa hakuna anayekataa hata mmoja lengo la Serikali la kutaka kuongeza mtaji, kuingiza teknolojia na *management*, hakuna anayeweza kukataa maana ni dhahiri masuala haya ya kibenki si maeneo ambayo Watanzania wengi wameboba humo, kwa hiyo, huo uamuzi wa Serikali ni wa msingi na ni bayana. Mahali panaponipa shida sasa ni mahali ambapo tunakuwa na malengo mawili ambayo kimsingi hayawezekani kwa maamuzi tunayoendelea nayo. Ni wakati tunashauriwa na Serikali tuweke sheria ili *percent 70* ziuzwe na *percent 30* zibaki kwa umma kupitia Serikali yao, ndiyo chombo kinachotunza umma. Sasa ukishauza *percent 70* huna kauli tena, unaweza ukaongelea mambo mengi sana kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, lakini tusingahau katika shughuli za makampuni kuna kitu kinaitwa *Shareholders Agreement*, ambao wataifanya wao wanaomiliki ile Benki bila sisi wala yeyote asiyemiliki ile Benki na kwa utaratibu wa sheria tulizonazo, *Shareholders Agreement* ita-*over rate* Sheria ya Makampuni katika maeneo yale ambayo *Shareholders* wamekubaliana kinyume na Tume ilivyotangaza, wala hilo halina mjadala. (*Makofi*)

La pili, Mheshimiwa Waziri anasema ni nia yake njema *NMB* iuzwe, ikishauzwa ndipo ipeleke matawi mengi vijijini ambako Serikali imeshindwa. *That is a serious statement.* Hilo ni *miracles and I wish I leaved to see that* kwamba, siku hizi wafanyabiashara walioko Tanzania badala ya kufanya *Commercial Banking* watafanya *Development Banking*, hapo sasa na mimi nitafurahi kwamba, katika uhai wangu Mungu akinijalia nitapata nafasi ya kuyaona yale yaliyoshindikana kwa wenzetu walioendelea lakini sisi tutaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata matamshi kwamba itawezekana ili kujenga uwezo wa kuhudumia wanavijiji wa Benki hii eti aliyenunua asilipwe gawio lake, hii nayo ni mpya katika ukurasa wa biashara, lakini duniani mambo yanabadilika tunaweza Tanzania tuka *invent a new system* na dunia iliyoendelea ikatufuata sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kama nia ya Serikali ni kuondoa umaskini, kama nia ya Serikali ni kuwawezesha Watanzania *percent 85* walioko vijijini wanahangaika hivi sasa basi hatutaelewana, lakini kama nia ya Serikali ni kuboresha uchumi wa nchi na marekebisho ya *NMB* ni katika hilo hakuna shaka ni kweli na ni dhahiri. Sasa ninasikia Serikali ina nia, *I am not sure*, italetu Muswada wa Uwezeshaji. Mimi sijui haya yote ni mapya, *I stand to learn.* Hivi baada ya kuwa hatuna Benki yoyote ambayo inamilikiwa na Serikali, hii *mechanism* ni *natural mechanism* itakayoweza kushughulikia haya masuala kati ya Taifa, Mkoa, Kata, Kijiji, sijui itakuwa kitu gani! *THB* ilileta matatizo tukaifuta, *we have never been able to replace it in the decade.* Tuliifuta na kama ilivyo desturi kufa ni kawaida. Kufa ni kawaida lisilo la kawaida ni kufufuka, *I hear there is one claim, a person who did that and that is the end of it, he was Jesus and don't.* Kufufuka si jambo la kawaida na ukifufuka nina uhakika ndugu zako waliokulilia ulipokufa watakukimbia kwa nini umefufuka!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi wakati wote nilikuwa natarajia jitihada itakuwa Benki hii imilikiwe na Serikali, lakini lengo la kupata mtaji, teknolojia na *management* liwepo. Ndiyo maana jana kwenye Kamati nilisema Serikali imiliki *percent 60* na hao wenye teknolojia na mtaji wamiliki asilimia 40, hiyo haikupendeza. Baadaye kwa sababu napenda kujifunza nilimwuliza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Waziri unapata tabu kueleza mengi sana, kwa nini usinielimishe ubaya wa kuwa asilimia 60 *government* na asilimia 40 wawekezaji ni nini? hakuwa na jibu.

Sasa nasema naomba mnielewe wanaosema Mheshimiwa Thomas Nyimbo anapinga si kweli hiyo ni tabia kusema uongo. Mimi sipingi nawaeleza ninalolijua, ninaloliamini na ninaloliona. Kupinga siyo kazi yangu, Bunge letu lina watu wenye kazi ya kupinga, watapinga wao kama wanapinga mimi siwezi kupinga. Mimi nitaelimisha, nitawashauri wenzangu na nitasema ili tuelewane au angalau ieleweke kwamba tunaloamua haliko *consistent* na lengo, ni hiyo tu. Hata mengi yanayoelezwa hapa haiwezi kuwa ni Sheria ya Makampuni halafu hiyo Kampuni ikawa inaamuliwa na Serikali. Kuna mwenzetu mmoja kwa busara kubwa aliongelea *golden share.*

*Golden share* napenda muelewe ina maana tu kwa nchi yenye watu wastaarabu, waadilifu na waaminifu. Maana *Golden share* haiji kwenye sheria. *Golden share* inakuja kwenye makubaliano, kwenye *memorandum article of association*, ndiyo inavyokuja. Hapa uzoefu wetu hakuna sheria hata moja ambayo Bunge liliipitisha ambayo itaiumiza Serikali au wananchi, hakuna. Inafanya utekelezaji kila mara hayo yametokea tu. Sasa nilifikiri ni vizuri tuyaweke mambo sawia kwenye kuziweka sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya kuna mwanafalsafa mmoja atakayetaka karatasi hii nitampa, amewa-analyse Waafrika. Ameanza kusema “*It comes as something of surprise to many Africans. To discover that all Africans look the same to non-Africans*”. Naomba nimalize. “*Africans, Tanzanians in particular are very good at agreeing to agree when they differ vehemently*”. Sasa haya ndiyo matatizo ninayoyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimalize kwa kusema kwamba, ushauri wangu haupingi, hoja iendelee, ila tukubali kwamba lengo la kuhudumia wanavijiji wa Tanzania hilo halipo. Kama tutaendelea kulieleza kwa kweli tutaonekana hatuna mantiki. Hakuna biashara ambayo haitatawaliwa na nguvu ya soko au uchumi, haiwezekani. Hakuna atakayefungua matawi vijijini ya kumpa hasara. Leo tunavyoongea *NBC* imefungwa. Kibaha wamefunga ni Makao Makuu ya Mkoa lakini bado kibiashara ni padogo, wengi wanashinda, Dar es Salaam wamefunga *NBC*. Wala huwezi kuwalaumu, ukitaka kuwalaumu peleka fedha za kufanyia kazi pale, ndio utaratibu wa biashara. Sasa unapomiliki asilimia 30 ndio umma huo. Maana ukitamka umma lazima utamke nyuma yake Serikali. Sasa ukisema wananchi watamiliki kwa maana ya kumuuzia Nyimbo, Juma, Hussein, Abdallah, *you are wrong, the concept is wrong*. Sisi ni *individuals* na tuna hulka zetu na tuna matakwa yetu katika kununua kitu. Hakuna anayenunua kwa nia ya mtu mwingine, si kweli. Hakuna mtu wa namna hiyo anayeweza kufanya kazi usiku na mchana kwa maendeleo ya umma ni Serikali. Ubinafsishaji ni sera mimi sikatai, ni Ilani mimi sikatai, turudi Ilani ya mwaka 1995 mpaka 2000 hatukuimaliza. Turudi kwenye Mataifa makubwa mengine yana miaka 200, 300 na kadhalika. Lakini mpaka leo bado vitu vya msingi viko *owned* na Serikali hizo kwa faida ya wananchi wa nchi nzima. (Makofi)

Sasa labda niombe kwa siku nyingine sio leo akipenda hata leo hivi aniambie lipi ambalo Serikali inadhani ni la msingi kwa maendeleo ya Watanzania katika maeneo yao na uchumi wao, Serikali italishikilia kama ni njia muhimu ya kuwaendesha Watanzania kiuchumi. Angalau tujue tusipigepige kelele na *NMB* tu kumbe Serikali imeandaa jambo lingine ambalo ni kubwa na ni zuri zaidi na ni busara kuua mtoto wa miaka 10 ili uzae wa mwezi mmoja. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa moyo wangu wote nakubali ni hekima na busara kwa mwanao kukaa na baba wa kambo akiwa hai ukawa unamwona kuliko akifa. Ndiyo usemi tuliousema jana na ninaurudia tena. Kwa hiyo, nakubali hoja iliyoletwa na Serikali iendelee, ila inabadili mwelekeo wetu wa *NMB* na yale tuliyoyaaahidi tunapovunja *NBC*. Ahadi kwa mwungwana ni deni, ada ya mja ni vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia na hasa katika hizi dakika za maombolezo kwa ajili ya hiki chombo cha wananchi ambacho kuanzia leo kinatokomea katika mazungumzo rasmi ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na hoja ya kuwashirikisha wadau. Ni utamaduni wa Bunge hili kwa muda mrefu tumeshirikisha wadau wote katika hatua zote kwa kuwa na wao pia ni sehemu muhimu ya jamii ya Tanzania. Imeelezwa hapa kwamba, wadau wameshirikishwa na baadaye akatajwa tu Serikali. Sasa nashangaa kama Serikali peke yake ndiyo mdau. Naomba nikumbushe kwamba, Mashirika haya yakiwemo *NMB* ni jasho la Watanzania na yametengenezwa yakaundwa na yakaonekana yanaelea kwa sababu yaliundwa na Watanzania wote. Sasa leo yanapokuja kumomonyolewa ni vizuri tukajua kwamba, wadau wote wana haki ya kushirikishwa, nasikitika kwamba, hawakushirikishwa. Kwa kuwa hawakushirikishwa kuna mambo mazito katika taarifa ya Waziri yananiwa wasi wasi. Ninamshangaa Daktari Bingwa, ambaye ni mwema sana anakaa hospitali anamwambia mgonjwa mwenye kansa kaa huko huko mimi nitakutibu huko huko halafu anamweleza kansa yake inafananaje. Hii ndiyo hali tuliyofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea juu ya watalamu kwamba, *NMB* hatuna. Wabunge wote ni mashahidi *NMB* kwa kutumia Bodi yao iliyoondolea, walileta ushahidi wa maandishi kwamba wataalamu tunao. Watalamu wenye Shahada za Uzamili wako zaidi ya 75. Hata Benki zingine za nje zilizopo hapa hawana. *NMB* imewafunza hao Wabunge wote wamegawiwa hiyo *document*. Wataalamu wenye *Diploma* ya mambo ya Benki wako zaidi ya 375, Wabunge wote tumegawiwa. Wataalamu wetu wa Tanzania tunajua wanatoka nje ya Tanzania wanafanya kazi sehemu zingine sina hakika wa Benki kama wapo sijafanya utafiti, lakini sitashangaa kama wapo. Leo tunaambiwa hatuna wataalamu, hivi ni vipi Tanzania tunazidi kudharau wataalamu wetu ambao watoto wetu tumewafunza sisi wenyewe kwa kodi zetu kwa jasho la Watanzania tunafika hapa tunasema hatuna wataalamu. Serikali itupe taarifa na ninamwomba Waziri kwa wakati muafaka, tungependa kujua idadi ya wataalamu wa nchi hii tuondokane na hili janga la kusema Tanzania haina wataalamu kiasi kwamba lazima kila siku twende nje kutafuta wataalamu.

Benki Kuu inaendeshwa na nani, sasa basi tubinafsishe na Benki Kuu kwa sababu hatuna wataalamu kama hiyo ndiyo *head*. Hatuwezi kuelewa sura ya aina hii kila siku tunapewa hoja ambazo kwa kweli hazina ukweli. Tungependa kujua ni kwa nini Bodi ile ambayo ilileta taarifa rasmi ndani ya Bunge kwa Kamati ya Bunge ikaondolewa siku chache tu baada ya kutoa taarifa kama sio Serikali kuudhika na ile taarifa ambayo ndiyo ilikuwa taarifa ya ukweli. Pili, Wabunge wote ni mashahidi na nilifikiri ni vizuri Wabunge wote tukasimama na ukweli. Aidha, Serikali inadanganya au *NMB* inadanganya na yule mwenye kudanganya anatakiwa kuchukuliwa hatua. Kama ni *NMB* imetudanganya kwa zile *documents*, wale wote wanatakiwa washtakiwe sio kufukuzwa tu. Lakini kama ni Serikali imedanganya, Serikali nayo inatakiwa ichukuliwe hatua. Huku kubembelezana ndio kumeua nchi hii. (*Makofi*)

Huko nyuma iliyoua haya Mashirika ni Serikali hii hii. Tulikopa Mabenki taarifa zile tuliziona, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha tulikwenda mpaka ndani ya *NBC* ile ya zamani tukakuta ni madeni yaliyokopwa na Serikali kwa shinikizo za Serikali, Mabenki yamekufa tunasema yamekufa hayafanyi faida. Sasa nani ameuua kama sio Serikali? Serikali iue halafu iseme tena yameuawa sijui na nani! Ni sawa na mtoto mdogo anakaa nyumbani anasema sahani imevunjika. Imevunjwa na nini imeteremka kutoka kwenye kabati peke yake. Sasa Serikali lazima iwe makini hatuwezi kuendelea na sura ya aina hii. Kwa taarifa tuliyonayo ndani ya Bunge hili kutoka kwa *NMB* ni kwamba, *NMB* ina vifaa vya kisasa imefunga kwenye matawi yake zaidi ya 75 katika matawi 108 kama sikosei. Sasa ni Benki gani nyingine imefunga vifaa na vifaa gani vingine tutaletewa, Waziri atuambie ni vipi atatuletea nje ya hivi na taarifa ile *NMB* ni Benki ya tatu hata kwa kushindana na hizi Benki nyingine za nje zilizoko nchini. Mimi ningependa tunapozungumzia tuwe wakweli na tuweze kueleza kama tunazungumzia nini isiwe ubinafsishaji unageuka tu kuwa *fashion* na *fashion* pia inachoka ikifika mahali fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vile vile tunapozungumzia suala la kubinafsisha tukapata fedha. Mimi bado najiuliza, jana kwa bahati nzuri tuligawiwa kitabu kile cha *PSRC* na nashukuru kwamba, tulipewa bila taarifa. Kwa Wabunge ambao ningependa tuwe wadadisi na tusiwe tunajaribu kuitetea Serikali kwa sababu ni Serikali yetu, wajaribu Wabunge kuwashawishi wasome kile kitabu cha jana kwenye fedha zilizopatikana kutokana na Mashirika tuliyobinafsisha. *ABSA* ambayo ndiyo imenunua *NBC 1997 (Limited)* ilitupa fedha za nje kiasi gani. Wengine wote wameandikwa wameleta fedha kwa dola. *NBC* imeleta fedha yake kwa Sh. 15 bilioni ambazo zimelipwa ni Sh. 12 bilioni tu. Mimi nafikiri ni vyema tukafanya utafiti. Nimetafuta siku pata majibu yale ya jana bahati mbaya nimeomba sikupewa hata muda. Lakini ninajaribu kujiuliza kama shilingi 12 bilioni zile zilipatikana kwa *system* ya ndani na bahati mbaya zikapelekwa Manhattan kama sikosei. Sasa najaribu kujiuliza hizi fedha tunazotafuta kutoka nje ni zipi wakati Watanzania hawa hawa hata ungewaomba shilingi elfu moja moja, shilingi bilioni 15 ungezi-raise hapa hapa kama *season capital*. Lakini tuna mambo mengi.

Nashukuru Mheshimiwa Waziri amesafiri sana na anatembea huko nje kama sisi wengine tulivyotembea, ukifika huko nje hata kwenye ndege tu unakuta magazeti yanatangaza *positions* zilizo wazi. Siku hizi sio lazima ubinafsishe unaweza hata ukaajiri utaalumu tu. Kama tatizo letu ni *Management* utaajiri *Managers*. Mbona Muhimbili tunaajiri, mbona *Net Group* tumewaajiri. Inafika kwa chombo kinachohusu kwa nini tunashindwa kuajiri. Ni kitu gani hiki ambacho kinatusukuma kama Muhimbili mahali pazito tumemwajiri tena kile ni chombo chetu na tunaamini kwamba tutapata. Tunaamini kabisa kwamba, *Net Group* tunawalipa tena fedha nyingi na wanatufanyia kazi na tuna uwezo wa kuwaamuru tunataka nini. Leo unatoa na kwa taarifa ya Wabunge ukizungumzia asilimia 70 kwa maana ya 49 percent ya *strategic investors*, unazungumzia Kampuni ambazo zinachukua na zita-manage. Kwa hiyo, huna madaraka tena ya kuingilia ni *Corporate Board*. Imeongozwa hiyo Kampuni kwa Sheria za Makampuni.



Sasa sisi tutaingia kama nani, wale wenye *Limited Company*. Ikiandikwa *Limited* maana yake ni *Limited*.

Unapozungumzia *21 percent to citizens of Tanzania* tujiulize Wabunge tuna *shares* wengi hapa za *TBL, Oxygen*, hivi tuna kauli gani na ni lini tumekwenda kupiga kura ndani ya Bodi ya *TBL, Oxygen* au sijui ya *TATEPA*. Hatuwezi kwa sababu sisi kama mmoja mmoja hatuna mamlaka na hatuna sauti na mimi bahati nzuri ni *member* wa *TBL*. Ninakumbuka tulipata barua tukaambiwa basi mjiunganishe ili muwe na mtu mmoja ndiyo mpate sauti hatukufika hata ile idadi iliyotakiwa. Kwa hiyo, hatuna sauti ndani ya *TBL*. Leo unasema unauza asilimia 21 kwa maneno mengine tunapoteza nafasi yetu, hiki kitu kimeondoka na hii ni njia ya chombo hiki kuondoka. Kama kitaondoka basi kiondoke. Lakini katika historia sisi tumeyasema yale tunayofikiria kwa niaba ya wananchi na sheria tutakuja ku-*judge* na tutaona ni kitu gani kitatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina zaidi naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika na mimi ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu. Kwanza kabisa, ningependa kuungana na wenzangu kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu. Vile vile naungana na wenzangu kuwapongeza wafanyakazi wa *NMB* kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya hasa ukizingatia kwamba, kama wasingekuwa waaminifu wangeshakata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nirudi tena katika jambo hili kwamba, dunia ya sasa ni tofauti kidogo na miaka 20, 30 iliyopita. Dunia ya sasa ni moja, tunaishi katika dunia moja. Ili tupate maendeleo suala la kutokushirikiana, kwa mfano mimi nimeona hata hapa Tanzania Mikoa ambayo ina watu, Tanzania nzima wamechanganyika wanafanya maendeleo makubwa sana kuliko wale waliobakia wenyewe tu peke yao. Mimi nafikiri suala la dunia ya leo hatuwezi kukwepa kufanya kazi na watu wengine, hili halikwepeki utake usitake. La kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka niishukuru Serikali maalum kwa sababu kwa bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nilikuwepo tangu mwanzo kwenye Kamati zetu zote na tulipokuja Bungeni na hasa tulipokutana hata Wabunge wa CCM, mapendekezo tuliyokuwa tunaleta wakati ule kila wakati ilikuwa ni kuiomba Serikali ikubali Tanzania kwa maana ya Serikali na Watanzania tubakize asilimia 51. Sasa leo Serikali imekubali na mimi nataka kuipongeza Serikali kwa kukubali mapendekezo yetu na huu ni uungwana. Sasa hivi najaribu kufanya *research* hapa na ikikamilika nitakuja kutoa, lakini mpaka sasa inavyoonekana ni kwamba, asilimia kubwa sana ya mambo yanayoamuliwa katika Bunge na kutekelezwa na Serikali mengi sana yanatokana na ushauri wa Wabunge. Kwa hiyo, Serikali haipuuzi Wabunge. Nina mifano hiyo nitakuja kuiwasilisha nitakapomaliza utafiti wangu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, labda sasa kidogo nielezee tofauti ya hisa za *DSE* na hii inayozungumzwa. Hisa zinazozungumzwa hapa ni zile ambazo wanaotamkwa hapa itabidi wazinunue mara inapokuwa inatakiwa. Sio zile zinazotangazwa kwa *DSE* ni

tofauti. Serikali itakapofika wakati ule pengine kuuza zile hisa zake ni jambo lingine. Lakini kwa mfano tukisema *consortium* maana yake nini? Maana yake ni kwamba, PSRC atakapokuwa anauza itabidi watoe maelekezo kwamba, waombaji hawaji mmoja mmoja, wanakuja *in a form of consortium*, wanakuja zaidi ya mmoja na wenye ujuzi wa *commercial banking* na *micro*. Hilo ni sharti. Lakini vile vile *consortium* hii haisemi kwamba, lazima wawe *foreigners*, haisemi awe kutoka nje ya nchi wanaweza hata kutoka humuhumu. Lakini sisi kwenye Kamati ya Fedha, jambo ambalo tulisema na likakubaliwa na Wizara na Serikali ni kwamba, watakapotangaza kwenye masharti yale mojawapo liseme endapo waombaji wanatoka nje washirikishe Watanzania wengine kuwa kwenye *consortium*. Sasa hayo pia ni mafanikio. Kwa hiyo, ndiyo kusema kwamba, katika *participation* ya 49 uwezekano wa kuwemo Watanzania pia ni mkubwa pamoja na ile asilimia 21. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana kwa maana ya vile tulivyokuwa tunashauri Serikali yetu kwa upande wa Wabunge.

Moja ambalo limesemwa na mimi nalikubali lakini lazima vile vile tukubaliane kwa mfano ukisema Watanzania haiwezekani ukawa unasema Watanzania wote na wa Sumbawanga na wa Kwera wakulima wa kijijini kwangu. Tunaposema Watanzania maana yake ni kusema angalau wakiwepo hata Watanzania 50, 60 kwenye *participation* ni Watanzania hao, ndiyo maana yake. Hata ukienda nchi za nje ukisema Waingereza kwani kila Waingereza wapo kwenye Kampuni ya Ndege au kwenye Benki. Hapana lakini sisi tunasema kwa kuwa tunaanza angalau Watanzania wapatikane wanaoweza kushiriki huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa mfano zinauzwa hisa za TCC, ni sera zetu na tumekubaliana wote na hii ni dunia nzima wananunua hisa katika Makampuni, sio wale wote watanunua ni wale wenye uwezo na wanaotaka. Ila tulichosema katika Muswada huu ambacho Wabunge tulishauri na imekubaliwa ni kwamba, ile asilimia 21 inazungumzia mtu mmoja mmoja na *Community Banks* pamoja na SACCOS za wananchi. Kwa hiyo, kama Rukwa tutakuwa na *Community Bank* tutaomba yenyewe ije inunue hisa. Lakini wasi wasi wangu ni kusema kuwa hivi tumejiandaa kiasi gani kwa kushirikisha vyombo hivi. Maana Iringa wana *advantage*, Mufindi wana Benki, wenzetu kule Same wana Benki, kwa hiyo, ni rahisi wao kusema wenye SACCOS. Kwa hiyo, nataka niseme kwa tafsiri ya kifungu zile *share* 21 mimi naridhika kwa sababu zimetaja mtu mmoja mmoja pamoja na *Community Banks* na kadha wa kadha. Hata SACCOS zetu vile vile hata wafanyakazi waliokuwa katika Benki hii wametajwa. Kwa hiyo, naridhika kabisa ningepomba wote tuunge mkono mapendekezo haya. (Makofi)

Sasa nilisema hivyo pia tulipata wazo moja mtaalamu, labda mmoja alileta wazo labda nimseme Dr. Kamala na akatuletea na *evidence* kwenye *internet* akatueleza wote tuliridhika pale hii ya *Golden Share*, huwezi kupuuza kwa sababu inatumika duniani. *Golden share* hii itaingia kwenye *memorandum* inaipa Serikali nguvu ya kusema hili ninyi wenye Kampuni hamtafanya, hili mtafanya. Hii imetumika dunia nzima na ndiyo maana tulikubaliana na wenyewe Serikali wamekubali kwa hiyo sioni kama kuna tatizo tena kwa sababu hiyo itakuwa kinga ya Serikali ya kusema kwamba hii msifanye, hii mtafanya, kwa sababu ya wasi wasi huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kumalizia hapa ni kuwa hili suala la *participation* nimeshaeleza, sitaki kurudia kwa sababu tumekubaliana wote. Lakini wazo alilotoa Mheshimiwa Dr. Slaa, naomba niliunge mkono. Lakini pia nielezee kwamba, naona kama tunajiandaa hivyo. Serikali ya CCM naona inajiandaa hivyo. Sisi kwenye Kamati yetu ya Fedha na Uchumi tulizungumza na Serikali na tumekubaliana kwamba, kwa sababu ya hali ya soko inawezekana baadaye tukagundua kwamba, Makampuni yaliyomo Tanzania hawayatumii Watanzania. Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba, iwepo sheria ambayo itasaidia kulinda na kuhakikisha kuwa, Watanzania waliosoma wanatumika katika Makampuni hayo. Kwa sababu bila ya hilo tutapata matatizo. Kwa hiyo, nataka *Law Doctor* ajue kwamba CCM tuko mbali kutazama hilo na tunakuja huko, hatuko nyuma katika wazo hilo. Ni wazo zuri na ndio maana mko hapa ili tusaidiane mawazo. Lakini nataka ijulikane kama Serikali inajiandaa kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa nataka niseme tu kwamba, sisi Watanzania maana kumekuwa na maneno yanasemwa Benki ya Kabwela, mimi nataka nikubaliane kwamba, ukizungumza kabwela Tanzania anza kuzungumza Rais mwenyewe na Serikali yote, wote ni makabwela tu hawa. Hakuna mtoto wa Waziri au Rais ambaye baba yake ni milionea, wote ni makabwela, watoto wa makabwela hawa. Waziri Mkuu anatoka kule tena ukifika kule Babati watu wanaishi kwenye mashimo, ni mtoto wa kabwela huyu. Sisi wote Wabunge ni watoto wa kabwela na hawa wananchi tunaowaongoza ni makabwela wenzetu, kwa hiyo sisi ni Wabunge wa makabwela kwa hiyo hatuwezi kupuuzwa maslahi ya kabwela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba, Muswada huu na tulivyokubaliana jana ni kwamba, baadhi ya mambo kwa mfano ndani ya *memorandum* yaongezwe. Kwa mfano, tunataka kwa mwanzo vile vile *memorandum* maana hatunayo hapa lakini tulisomewa. Yako mambo mazuri sana ambayo tulisomewa mazuri kweli yanazingatia hili. Lakini tulisema waongeze na wamekubali. Kwa mfano, tuna *consultant* mmoja hapa Ndugu Iddi Simba, Wizara ilisema kama ana mawazo mengine kwa uzoefu wake anaweza akawapa kule na kama kuna mwingine kati yetu ana mawazo mazuri alete Wizarani ili waboreshe ile *memorandum*.

Kwa mfano, mimi nimesema waongeze kilimo, waendeleze ufugaji na vile vile waendeleze na uvuvi ili Benki iwepo kwa sababu hatujawa na Benki ya Wakulima. Benki hii ndiyo ianze kwa Watanzania wote pamoja na wafugaji na wakulima na wengine wote wanaohangaika na shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe machache.

Kwanza, nimuunge mkono Msemaji wa Kambi ya Upinzani amezungumza vizuri sana na nafikiri ni ya kuangalia. Pili, namuunga mkono wajina wangu Thomas Nyimbo amezungumza mambo muhimu na ya msingi katika hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka tu niwakumbushe Wabunge wenzangu kuhusu mwenye kuanzisha Benki hii ya *Microfinance*, ambaye leo ni marehemu, Mwalimu Julius K. Nyerere. Kwa kweli leo akifufuka akiona haya tunayoongea hapa hatakubaliana. Kwa sababu Benki hizi zina mtandao sehemu zote Vijijini. Tilitumia fedha nyingi kujenga Benki hizi huko Vijijini na hakuna Benki nyingine yenye mtandao wa kiasi hicho. Kwa hiyo nia yetu ilikuwa ni kumiliki Benki yetu na kumiliki fedha yetu na ni siri ya nchi. Wakati tunauza *NBC* ilikuwa moja, kulikuwa hakuna *Microfinance Bank*. Sasa tukakubaliana kwamba hii Benki tuigawe tutoe kidogo iingie kwenye *Microfinance* imilikiwe na Watanzania na hii kubwa tuwauzie hawa wageni na tukafanya hivyo. Sasa leo wakati tuna Mabenki mengi zaidi ya Mabenki 16 makubwa *CRDB* na kadhalika tunang'ang'ania kabenki haka kadogo sasa sijui kamemuumiza nani. Wakati kabenki haka tumeambiwa kwamba kanatoa faida. Ina matatizo gani hii Benki ya *Microfinance* kwa ajili ya wananchi na inamsumbua nani? Kama ni maendeleo ya nchi tunayo hiyo kubwa *National Bank of Commerce* ambayo inamilikiwa na *South Africans*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tujirejeshe, tuangalie ugomvi tulioufanya sisi mapema wakati inabinafsishwa hii Benki (*NBC*) na hawa *Wa-South Africa*, Makaburu hawa kuhusu ugomvi na *NBC*. Ugomvi huo tulikwenda kuamua kule *South Africa*. Walizuia fedha na wakataka tukubaliane. Kwa hiyo, watu wetu walikwenda kule ikabidi wafanye muafaka kwa sababu mkataba ulishapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme ni kwa nini hasa nimemkumbuka Marehemu Nyerere, kwa sababu hawa makaburu wanataka kuturudisha kwenye *monopoly*, wanataka kuhodhi hii Benki tunayoiuza leo ya *Microfinance* tunasema eti Serikali itapata asilimia 30, hawa *strategic investors* watapata asilimia 49. Wao ndio wenye fedha na watakaonunua ni hao Makaburu wa Afrika ya Kusini wala tusidanganyane hapa, watainunua, wataihodhi, hakuna watu wengine watakaonunua hii Benki zaidi ya hao. Sasa sisi kabla hatujatoa hii asilimia yetu 30 Sheria ya Makampuni inasema aliyetoa fedha nyingi ndio mwenye sauti, hata kama wewe una asilimia 51, lakini hujazipata hizo fedha zenyewe. Yeye amekuja ameweka fedha zake pale kwa hiyo yule mwenye fedha nyingi ndio mwenye "say", ndiyo Sheria ya Makampuni inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bado hao watasimamia na watahodhi hizi Benki kama walivyohodhi Kiwanda cha Bia, kwenye bia tunapata kodi kubwa lakini wamefunga Kiwanda cha *Kibo Breweries* na hakuna wa kuwasemesha.

Si wamenunua bwana na watanunua hii na watafunga kama walivyofunga Benki za Kibaha na nyingine. Wanasema sisi tunafanya biashara na mlituuzia. Hata juzi hapa tumesikia watu wa madini wanatuambia, sisi tunafanya biashara bwana, tumekuja kibiashara tunataka kuchuma, siyo kuwaendeleza ninyi. Sasa leo hii tunavyowauzia hawa, hayo tumeyaangalia ndugu zangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubali hii ni Sera ya Chama Twawala (CCM), kuuza kila kitu na sina tatizo na hilo kwani ndiyo Serikali inayotawala. Mimi ni

mpinzani, sina tatizo na hilo, lakini nawaasa ndugu zangu, nawaasa kwa kweli. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa kwenye Kamati ya Fedha, tulipokuwa tunafanya mahesabu kuhusu hii Benki ya *Microfinance*. Tulikataa hapa na mkarudisha na kusema: “Tumeongeza hizo asilimia 2.” Lakini hizo asilimia 2 kutoka asilimia 49 ambayo walikuwa nayo ili iwe asilimia 51 ni maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ni nani atakataa kwamba tulivyotaifisha nyumba za Wahindi kule Dar es Salaam tulisema Wahindi wabaki na vyumba viwili katika *room* kama 20 au 30 ya yale maghorofa! Tujifunze hapo, leo ni Mwafrika gani yuko pale? Wale Wahindi kusema wabaki na vyumba viwili tu na ndiyo itakayotokea hapa katika hili, kwa sababu hatuna hizo fedha, hata hizo asilimia 21 hatuna. Kwa hiyo, wao watatoa fedha, watakuwa ni wasemaji na watafunga hayo Mabenki. (Makofi)

Ndugu zangu, napenda kusema kwamba, Sera ya Ubinafishaji tuwe nayo, lakini kuuza kila kitu, kila kitu, kila kitu, ningependa hebu tuangalie ni nini kilichotututiza, je, ni *Banking System*? Kuna Benki nzuri kama *CRDB*? *What is the problem*? Ni nini hasa tunachofuata huko kwenye *Microfinance Bank*? Imeomba hela Serikalini? Inawahitaji muwape hela? Hapana! (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hii inanipa uchungu sana. Siku hiyo tunajadili katika Kamati ya Fedha, tulipewa taarifa na Bodi ilikuwa nzuri kabisa na ilikuwa inaendeshwa na Mwenyekiti anaitwa Kaduma. Wakati tunajadili siku hiyo hiyo usiku taarifa ya habari ‘Kiongozi wa nchi avunja Bodi ya *NMB*.’ Jamani, tunakwenda wapi? Ni demokrasia gani hiyo, ndiyo kulinda haki za mtu? Sisi tunasema kwamba, tuna nchi ya demokrasia ya wengi wape. Sasa, Bodi imevunjwa, maskini ya Mungu yule mtu amejikalia Chuo Kikuu pale, basi hana Bodi. Sasa tutaamini lipi hapa, kwamba hata wenzangu waliokuwa wananiunga mkono kwenye hoja hii na wao wametishwa kuwa usiposema sawasawa wewe utafanyiwa hivi na hivi. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunapendekeza kwamba, kwa kuwa mmeamua kuuza na sisi hatuwezi kutia neno hapo kwa sababu nyie ndiyo wenye Serikali yenu, tunasema hivi basi hawa *Strategic Investors* wawe na asilimia 30. Kuna Wawekezaji kutoka Marekani na sehemu nyingine, *why only this South Africa*?

**MBUNGE FULANI:** Kaburu.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Huyu Kaburu wa *South Africa*, *why*? Anatutesa ni kwa nini tusichanganye Wawekezaji wengine? Ni kwa nini huyu? Tumekwishamwona tumuache. Tukumbuke mateso aliyotufanyia mpaka Viongozi wetu wakaenda *South Africa* kufanya kesi ya *NBC*, mimi najua. Walizuia fedha yetu. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nataka niwaeleze na Wabunge ambao hawajui, ukitaka ku-*draw* hela ya *National Bank of Commerce*, kama mashine haija-*click*

kule kule *South Africa* hauwezi ku-*draw* hapa. Mashine kama zile unazo-*draw CRDB* ni lazima i-*click Dar es Salaam*. Sasa, hii ya *NBC* ni lazima i-*click South Africa*, kwa kuwa wameona kwamba, Benki ya *Microfinance* italeta ushindani katika *NBC* na ina *potential* kubwa, watahodhi. Hebu tuangalie, zile nyumba zilizokuwa za *NBC* sasa hivi ziko wapi? Wameuza nyumba, wameuza viwanja wanajumlisha kwenye mtaji na hizi wataanza kuuza nyumba na vitu vingine maana nyumba ziko nyingi. Watasema hii haifai uza, hii haifai uza, weka fedha. Fedha zinaingia, *control South Africa*. Hebu tuchanganye basi hawa Wawekezaji halafu tuwape asilimia 30 na asilimia 70 ziwe kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Wawekezaji, tuna Benki ya Ushirika imeomba kununua, wauzieni ni wenzetu. Kuna *CRDB* nayo imeomba kununua, wauzieni ni wenzetu. Lakini haya mambo ya kubanana na huyu M-*South Africa* ndiyo kitu ambacho ninakipiga vita zaidi na zaidi na zaidi na ninaomba chonde, chonde, chonde, hatusaidii sana huyu. Kama tunataka atusaidie, basi tayari tumeshampa ile Benki kubwa, tumeshampa *National Bank of Commerce*, si akae nalo atuachie hii ndogo. Sipingi sana mambo yenu, lakini nawashauri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba, haina Wataalam, kila mahali tunapobinafsisha hatuna Wataalam! Sasa na Serikali yote itakavyokuwa haina Wataalam; je, mtaachia ngazi na ninyi tuwabinafsisha? Kwa sababu sasa kila mahali hakuna Wataalam, hakuna Wataalam, hakuna Wataalam, mnabinafsisha na nyie mbinafsishwe? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba, hiki kitu wanachosema kwamba, ni *golden share* hakitusaidii. *TTCL* wamewapa hiyo *golden share*, lakini leo hii tunalia nayo. Sasa, haina maana sana kwa kutuambia ni *golden share* ndiyo itakuwa muafaka, haitatusaidia sana. Kwa hiyo, tunafahamu hilo na tunafanya utafiti wa kina kujua ni nini tunakuja kusema hapa. Tuangalie sana wakati tunabinafsisha vitu vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake wote, kwa kutayarisha hoja hii na kuileta mbele yetu. Pia, ninampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri waliyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana tukaelewa kwamba, Watanzania wanao uwezo wa kununua hizo hisa. Mfano ulitokea wakati tunauza *DAHACO*, iliuzwa kwa fedha nyingi sana, mpaka ikabidi Wananchi warudishiwe fedha zao. Kwa hiyo, huu ni mfano mzuri sana wa kuwauzia Wananchi asilimia 21. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, tunadhani kwamba, uamuzi huu wa kuwauzia Wananchi asilimia 21 na asilimia 30 zibaki Serikalini, kwa kweli inatungezea nguvu kabisa na hasa Wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Maneno mengi yatazungumzwa

na Wapinzani, lakini wao walitaka tushindwe kuuza ili waweze kusema zaidi, lakini tunashukuru kwamba tumeweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kabla ya kuuza hizo *shares* tujaribu kuangalia mifano mingine kwenye Mashirika tuliyouza. Tuna *accounts* za mwaka 2000 za *TTCL* ambazo hazijakamilika mpaka leo, tunaomba hilo nalo lisije likatokea hapa, kwamba *accounts* zote ziwe *up to-date*. Unaambiwa kwamba, Kampuni hii haijasajiliwa, haina hati ya kufanya kazi ya kibenki, tunaomba hilo lirekebishwe kabla hatujauza. Vile vile, maslahi ya Wafanyakazi na hasa Mikataba ya Hiari ya Wafanyakazi yote ikamilishwe, tusingependa kuona mlolongo wa Wafanyakazi wanakwenda *PSRC*, wanakwenda Hazina na vitu kama hivyo. Yote hayo yaandaliwe kwanza, wakubaliane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hizo asilimia 30 ambazo zitabaki Serikalini iwekwe wazi kwenye mkataba kwamba, watauziwa Wananchi na kama Serikali itabaki na *Golden Share* ni vizuri ikajulikana. Pia, tuna mifano mingi kuhusu masuala ya Wafanyakazi ambayo kwa kweli inasikitisha. Tunadhani huu ni wakati mzuri, Serikali ikachukua hatua kuhakikisha kwamba, matatizo ya Serikali na Wafanyakazi yanakwisha, kwa mfano, *Elimu Supplies* na *NASACO*, kwa kweli inatuchafua. Ni watu wachache, lakini bado wanatuhangaisha, ni vizuri Serikali ikamaliza haraka sana matatizo hayo. Tunachohitaji ni mtaji, menejimenti nzuri na teknolojia mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wapinzani wanasema tunao Wafanyakazi waliosoma na wana vyeti na kadhalika. Suala siyo Wafanyakazi, unahitaji menejimenti yenyewe na mfumo wake mzima, siyo mfanyakazi kuwa na *degree*, hapana. Tunaposema teknolojia mpya inakwenda na Wafanyakazi ni lazima wajue teknolojia mpya. Tunapozungumzia mtaji, sasa unataka mtaji uendeshwe na watu ambao hawana teknolojia? Ni vizuri tukaelewa haya mambo na ndiyo maana tumetafuta menejimenti mpya kwa ajili ya *TANESCO* na mapato yameongezeka mara mbili. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri mkalielewa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwekezaji atoe utaalam wa kutosha na kufundisha watu wetu, siyo kwamba, atakuja na watu wengine, hawa hawa tulionao atawafundisha. Vile vile, nadhani hizi fedha ambazo tutauza hisa zetu asilimia 49 na asilimia 21 ni vizuri zikarudi tena kuongeza mtaji wa Benki ili Serikali iweze kupata kodi mapema zaidi na wananchi walionunua zile hisa waweze kupata gawio mapema zaidi. Lakini ukisema zichukuliwe na Serikali, itachukua muda mrefu sana kuhakikisha kwamba tunazipata hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu ni hayo machache. Ahsante sana.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu kidogo kuhusu Muswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya *National Microfinance Bank* ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda sana kuishukuru Serikali kwa kukubali ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika kushughulikia suala hili. Nadhani hiyo ni hatua nzuri sana ya kutekeleza majukumu yetu baina ya Serikali pamoja na Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siyo mfanyabiashara, lakini ninasoma *magazines* za *African Business*. Nilipokuwa *Air Tanzania*, kila mwezi nilikuwa naletewa *Airline Business Magazine*. Kwa hiyo, tunajifunza mambo haya ya kuendesha shughuli za uchumi na biashara, hivyo isifikiriwe kwamba wanaojua haya mambo ni wafanyabiashara tu. Pengine hawaelewi zaidi kuliko wale wengine ambao hawafanyi biashara, maana wamechukua *for granted* kwamba, wako kwenye hiyo shughuli, wanajua kuliko sisi ambao hatuko kwenye biashara. Tunapenda kujifunza na ni vizuri tuendelee kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoona katika *Global Business* sasa hivi *trend* ni kwamba, watu wanakwenda kushirikiana kwa njia ya usawa (*Equal Partnership*), ndiyo inayokuja. Sidhani kama tunaweza kupata Mwekezaji yeyote wa maana kama tunamuuzia hisa tatu au nne, hatakuja! Kwa hiyo, ni lazima tuitazame hii katika *Global Business*. Wewe unataka kufaidika na yule anayekuja kuingia kwenye *partnership* na yeye anataka kufaidika. Sasa, muweke utaratibu ambao wote mtafaidika, lakini yule ambaye ana hisa nyingi atafaidika vizuri zaidi. Katika kugawanya *shares* hujafanya kazi kubwa, kazi kubwa ni kwenda kuweka taratibu za usimamizi na za kuweka kanuni za kufanya *business* hiyo. Kwa hiyo, kubadilisha sheria kwa kweli ni kazi ndogo sana tuliyofanya hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri nilipata nafasi ya kushirikishwa katika *privatisation* ya *Air Tanzania Corporation* na ninaishukuru Serikali kwa sababu waliniteua kuwa *Interim Chairman* wa kusaini *documentation* kwa niaba ya Serikali. Kulikuwa na *document* kama sita, ambazo zinaweka nini kifanyike, wewe unatakiwa ufanye nini, wewe usifanye nini na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, si mambo rahisi rahisi ukiyatazama hivi kwamba, unagawanya hisa 49 wanachukua halafu na wewe unakaa, hapana. Kuna taratibu ambazo Serikali inazifanya. Ninasema hivyo kwa sababu nilishiriki kwenye kusaini kwa niaba ya Serikali makaratasi ya kuiuzia *South Africa Airways* asilimia 49 ya *ATC* na asilimia 51 ziko kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Serikali katika utaratibu huu uliowekwa wa kuwa na hisa 51 kwa maana ya *Majority Shareholding*, halafu hizo katika wakati muafaka, 21 ziuzwe kwa Wananchi, hizo nyingine katika wakati muafaka ziuzwe, halafu baadaye Serikali ibaki na Hisa ya Heshima (*Golden Share*). Nilikuwa nashangaa, hili wazo lilipotokea jana ilionekana kama ni wazo jipya, siyo jipya hili, someni Ripoti za Kamati ya Mashirika ya Umma. Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa tunalisema humu ndani hili suala, siyo la leo, lakini tatizo la Tanzania jambo likitoka nje linasomeka vizuri. Jana tuliletewa ile *Computer printout* ya mtu mmoja anazungumzia umuhimu wa *Golden Share*. Naona wameniheshimu, lakini ile tuliandika kwenye taarifa nyingi za kila mwaka umuhimu wa *Golden Share*, zimo. Kwa hiyo, ninasisitiza kwamba, haya



mambo mengine ambayo ni ya ki-*international* tuyatumie ili tuweze kunufaika zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali na ningependa Wabunge wenzangu muelewe kwamba, unapouza hisa chache utapata mtaji mdogo. Kwa hiyo, kwa kuuza hisa 49 Serikali itapata mtaji zaidi na hili ni jambo zuri, kwa sababu mtaji ule ndiyo utatumika kubadilisha na kuimarisha kazi za *NMB*. Hizi haziingii kwenye kodi, zinakwenda kwenye kuimarisha mtaji wa *NMB*. Kwa hiyo, ni hatua nzuri sana. Kama nilivyosema, kwa kweli hakuna mtu yeyote ambaye ni *Serious Investor* au *Strategic Investor* atakuja umuuzie hisa 25 achukue. Hawezi, haji kubembeleza, mna-*negotiate*. Kwa hiyo, unakwenda kwenye *position* ambayo ni *negotiable*, yaani mnazungumza kitu *close to equal partners*, lakini *you are not equal* kwa sababu hisa zile umejiwekea ili zikupe nafasi ya kuweza kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusisitiza kwa Serikali kwamba, *National Microfinance Bank* ibaki na kazi yake iliyoanzishwa (*The Core function of Microfinance Bank*). Kwa hiyo, tungetaka tuone kwamba kuna taratibu zilizowekwa za kuwahudumia wakulima wadogo, wafanyabiashara wadogo, wavuvi wadogo na wafugaji wadogo. Haya ndiyo madhumuni ambayo tunataka kwa kweli yaende na hii Benki. Sasa, anayepewa jukumu hilo, hili ndiyo jukumu la kusimamia, liwekewe taratibu za kusimamia kwamba hii azma inasimamiwa na inatekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa jinsi ambavyo ameshirikisha Wabunge wengine na kuheshimu mawazo yao na baadaye kutoa taarifa ambayo ninakubaliana nayo kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na *Attorney General* kwa jinsi walivyojibu hoja za Wabunge kwa kina na kuelewa nini ambacho kinatakiwa. Kwa bahati nzuri eneo langu ambalo nimelikalia sana ni eneo la *Policy Management and Policy Analysis*. Ukishatunga sera, ukishaipitisha, *stand by it*, eah. *Stand by it* mpaka ufike wakati utakaposema, sasa hii haifai. Lakini mtu mwingine asikusumbue hapa katikati ili utoke, hakuna sababu. Mpaka uridhike kwamba kwa kweli hapa ulipo ni lazima uibadilishe sera hii maana haikusaidii. Sasa, Sera ya Ubinafsishaji ni Sera ya Chama cha Mapinduzi na tutaisimamie na tutafanya marekebisho yote muhimu yanayostahili na wenzetu nitashangaa kama hawatatukosoa, maana ndiyo kazi yao hapa Bungeni. Lakini tungetaka tupate constructive criticisms ili tujenge nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafsi hii na ninaunga mkono hoja hii kabisa. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie katika hoja hii muhimu ambayo inahusu ubinafsishaji wa *National Microfinance Bank*. Niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu ukiwa

sasa umeangalia marekebisho ambayo tumekuwa tukiyazungumza kwa muda mrefu na sitasita kuunga hoja hii mkono kwa sababu ni hoja muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono, katika kuchangia hoja hii ninataka kutoa tahadhari tu kwamba, sasa hivi kama Serikali ilivyotoa mapendekezo ni kuwa asilimia 51 inabaki kwa umma pamoja na Serikali na 49 percent ya hisa inachukuliwa na hii *consortium* ambayo itapata nafasi ya kushinda. Sasa, ni vizuri kabisa kwenye ile asilimia 51 inayobaki katika *Sales Agreement*, Serikali ikawa wazi kueleza ni jinsi gani zile hisa zinazobaki, asilimia 30 ambazo hazitanunuliwa kwa wakati wa kwanza na Wananchi ama Watanzania zitakuwa *exposed* namna gani wakati wake ukifika, badala ya kuacha tu wazi kwamba, Serikali itafikiria jinsi ya kuzi-*dispose* wakati utakapofika. Nadhani ingekuwa ni vizuri iwe wazi kabisa ni jinsi gani hisa hizi zitatolewa. Hiyo itatupa nafasi Watanzania kuwa na uhakika wa miliki ya Benki hii ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia na shabaha ya kubinafsisha kama ilivyoielezwa na Serikali na imeelezwa katika Mashirika yote yanapobinafsishwa kwamba, ni kutaka kuongeza mtaji, ni kutaka kuleta menejimenti ya kisasa na kuleta teknolojia ya kisasa. Hii nakubaliana nayo na kwamba wakati huu ambapo dunia iko wazi, mtandao uko wazi kila mahali, ni vizuri tukawa na teknolojia ya kutosha na ya kisasa kwa sababu kama hatuna teknolojia ya kisasa ina maana kwamba Benki hizi ambazo matawi yake yatakuwa yako mbali (matawi 108) bila kuyaunganisha na mtandao wa kisasa na teknolojia ya kisasa kwa kweli huwezi ukayatawala matawi haya na yakapata faida. Ni muhimu sana kuleta hii teknolojia. Kwa hiyo, ni vizuri kabisa katika *sales agreement* Serikali ikawa wazi ni jinsi gani, ni teknolojia ya kiwango gani ambayo inahitajika, siyo kuiacha wazi tu kwamba itakuja teknolojia bila kusema teknolojia inayotakiwa inatakiwa ifike kwa kiwango gani. Nadhani katika *Sales Agreement* ingewekwa hiyo ingekuwa ni jambo muafaka. Angalizo la pili, ambalo napenda kulitoa ni juu ya wenzetu hawa hasa watakaokuwa *consortium*, ambao kwa kweli ndiyo watakuwa na uamuzi mkubwa katika utendaji wa Benki hii. Sasa, iko mifano ambayo ninaweza nikaeleza. Kwa mfano, *NBC* ilisema haitafunga matawi, lakini ikafunga matawi. Sasa ni vizuri tuwe na uhakika kwamba kweli matawi hayatafungwa, kwa sababu matawi haya ya Vijijini yatakapofungwa, maana yake Wananchi wetu hawatapata nafasi ya kupata *banking facilities* na kwa maana hiyo, mikopo haitakuwepo kwa Wananchi wetu ambao ndiyo tunaowatarajia wafaidike kutokana na *Microfinance Bank*.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo la tatu, ni juu ya uamuzi wa Benki hii kwamba, inawakopesha watu wa namna gani. *NBC* tumeiona, kwa mfano unapotaka kuchukua mkopo *NBC* licha ya kutimiza masharti yote, lakini hawakubali u-*finance* biashara mpya, hata kama umekuwa ukifanya *investment* tayari, unahitaji tu *working capita*, lakini kama ni biashara mpya, *NBC* wanasema hawawezi kufundisha mtoto kutembea. Kwa hiyo, ningependa nitoe angalizo hilo kwamba, katika *Sales Agreement* hizi ambazo Serikali itazifanya ni vizuri mambo yote haya yakawekwa sawa, ama sivyo tutakuwa tumeiua Benki na haitasaidia asilimia 80 ya Wananchi wanaoishi Vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli shabaha yangu ilikuwa ni kusimama kueleza haya machache, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge waliosimama wamekwishaeleza mengi kuhusu umuhimu wa kuibinafsisha na jinsi ya kuisimamia ili angalau iweze kutoa huduma inayotakiwa kwa Wananchi. Kwa hiyo, napenda nisipoteze muda mwingi na muda wenyewe umekwisha. Niishie tu kwa kusema kwamba, naiunga hoja hii mkono ambayo sasa imeiva kwa wakati wake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwanza nawashukuru sana wale waliochangia, wamejitahidi sana ku-*save time*, maana tayari tumepata wachangiaji tisa ambao wameshazungumza. Sasa, tutakapokutana tena mchana ataanza Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, halafu na Mheshimiwa Mlolwa pia ajiandae. Napenda kuwakumbusha lile tangazo la Mheshimiwa N'hunga la wana-CCM kwamba wabaki. Napenda pia kuwakumbusha wale Wajumbe wa Tume ya Bunge na Kamati ya Uongozi, tukutane saa 7.30 mchana.

Baada ya hapo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa 10.00 jioni.

*(Saa 06.59 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika hoja ya Muswada huu wa Sheria ya *National Micro Finance Bank*. Kwanza kabisa niseme nina-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, niseme moja kwa moja kwamba ninaunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Pia ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru sana Serikali kwa utaratibu ambao imetumia hatimaye tukafikia muafaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge walikuwa na wasiwasi mkubwa hasa katika muundo na mgawanyo wa hisa za benki hii. Lakini sasa sura ambayo hatimaye imefikwa ya asilimia 51 kwa Serikali na Watanzania asilimia 49 kwa kikundi cha wawekezaji mahiri huo nadhani ni muafaka mzuri. Kwa hiyo, napenda nishukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na mimi nisisitize kuhusu ule wasiwasi ambao kwa namna moja au nyingine Serikali imeshachukua hatua. Jambo la msingi katika Benki hii ni kutoa huduma za kibenki ikiwa na pamoja na mikopo, ku-*mobilize services* kwa wananchi wadogo wadogo huko vijijini na mijini, kukuza biashara zao, kuhudumia masuala ya elimu, ujenzi wa nyumba hayo ndiyo mambo ya msingi kwa kupitia *Macro financing*. Kwa hiyo, swali na wasiwasi uliokuwepo ni ile *Central Mission* ya *Micro Financing* kwa kiasi gani Serikali na hili zoezi ambalo linaendelea sasa la kubinafsisha NMB itaweza kulindwa hiyo *Central Mission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu ambazo tulipewa za mwenendo wa ufanisi na uendeshaji wa benki hii, ulikuwa unaonyesha dhahiri kwamba matawi mengi takribani 50

hayafanyi vizuri. Sasa kwa mwekezaji yeyote wa kibenki ambaye msukumo wake anasukumwa na kutengeneza faida inaweza kuwa ni vigumu sana kuyaacha yaendele matawi kama hayo. Kwa hiyo, hili duku duku la kufanya Serikali na wananchi kwa ujumla wawe na hisa nyingi linapelekea kwamba haya matawi hayafungwi.

Kwa hiyo, hilo ni suala la msingi kabisa. Mimi napenda niseme kwamba Serikali isijivue katika jukumu lake la kuendeleza *Micro Financing* kwa kupitia benki hii. Uzoefu tunao ambapo benki za nje ambazo zimeingia hapa nchini zimeanza kufunga matawi. Kwanza zinafungua matawi mengine, lakini hata kule vijijini baadhi ya matawi zinafunga kwa mfano *City Bank* imefunga tawi huko Mwanza sembuse *NMB* kwa hiyo, Serikali haiwezi kujivua katika kusimamia benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi bila kupoteza muda napenda kusema kwa mara ya mwisho kwamba naunga mkono hili pendekezo la *NMB*. Nimalizie kwa kusema kwamba kwa ufanisi ambao ulikuwepo mwaka 2002 ambapo katika mabanki matawi 108 ya *NMB* Tawi la Wilaya ya Kahama limekuwa namba 10.

Kwa hiyo, ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza *Management* ya Tawi la Benki Kahama na wafanyakazi wa huko kwa ufanisi mzuri. Kwa hiyo, katika kubinafsisha Benki ya *NMB* kama alivyosema Waziri uzoefu na *track record* ambayo sasa hivi imekwisha kufikiwa na *NMB* lazima ilindwe na iendelezwe. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache kuhusu Muswada ulioko mbele yetu. Kwanza kabisa nataka kusema kuwa mimi naunga mkono Muswada huu moja kwa moja. *(Makofi)*

Pili, tunavyoona mambo ya kubinafsisha nchi na Serikali yetu ina uzoefu mkubwa sana. Imepata kubinafsisha mashirika mengi, mengine yaliyobinafsishwa yanafanya vizuri sana. Lakini kuna mengine yanaboronga au yameboronga. Sasa yale mazuri ambayo tumejifunza katika mashirika ambayo tuliyabinafsisha basi yatumike katika kuiongoza hii *NMB* mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu *Micro Finance* ni sekta ambayo ni *very sensitive* na kama itakuja kuboronga maana yake uchumi mzima na *monitorisation system* ile ambayo kuingiza uchumi fedha utaharibika.

Kwa hiyo, Serikali isijivue majukumu yake baada ya kubinafsisha *NMB*. Labda ningesema kuwa hii *NMB* mpya ambayo itazaliwa baada ya kupitishwa Muswada huu ni kama mtoto aliyezaliwa, lakini baada ya mtoto kuzaliwa kawaida wazazi na jamii wanaanza kufikiria jinsi ya kumlea mtoto huyu.

Sasa mimi ninavyoona kwa kuwa *NMB* mpya inazaliwa wakati wa utandawazi na ushindani mkubwa katika biashara ya kifedha na biashara katika sekta zingine, itakuwa vizuri Serikali kama itaelekeza nguvu zake katika kuweka mazingira mazuri kule vijijini.

Kwa mfano, kuna matatizo ya miundombinu huko vijijini na wale walengwa wakubwa wa *NMB* watakuwa ni wananchi, wakulima na wafanyabiashara ndogo ndogo walioko vijijini. Leo tunavyoona umaskini umezidi kuongezeka sasa wale ndiyo walengwa na wale ni wateja wakubwa wa *NMB*. Sasa hawa wasipopatiwa mazingira mazuri ya kukuza uchumi au kukuza shughuli zao kwa kweli utakuwa huo ndiyo mwanzo wa *NMB* kudorora. Kwa hiyo, Serikali ina jukumu la kuweka mambo sawa kuhusu mazingira ya vijijini. (*Makofi*)

Kwa mfano, mimi ninavyoona Serikali na *NMB* wataendelea kufanya kazi pamoja na hasa katika kuongeza matawi. Matawi sasa yamekomea tu kwenye Makao Makuu ya Wilaya na siyo kote kuna Matawi ya *NMB* katika Wilaya. Sasa wananchi walio wengi wako kwenye tarafa, vijijini na kata, kufika kule kwa kweli lazima kuwepo njia za mawasiliano. Lazima barabara zijengwe vizuri, madaraja yajengwe kusudi hata ikiwa kuna *operation* za *NMB* zifike kule kwa sababu ya mawasiliano yakiwa ni mazuri. Pia kuna tatizo la maeneo vijijini, hasa hasa tunazungumzia kuwa *NMB* itakuwa na mtandao mzuri ambao utaunganishwa na *headquarters* zake.

Lakini sasa pasipokuwa na umeme hili halitawezekana na *banking activities* za sasa zinategemea sana mambo ya mawasiliano. Kwa kweli suala hili la kuelekeza nguvu kupeleka umeme vijijini liwe mojawapo ya maeneo ambayo yatasaidia sana kukua kwa *NMB*. Ningeomba pia Serikali ione uwezekana wa kuishauri *NMB* kukopesha kwa masharti nafuu. Hiyo, nasema hivyo kwa sababu kuna taasisi nyingi mojawapo ni *International Monetary Fund* ambayo ilipata kufanya *studies* nchi za America ya Kusini na ikaanza kukopesha hata pasipo kuweka dhamana.

Sasa suala kama lile kwa wakulima wetu na wananchi wa vijijini kwa kweli ukisema wakopeshwe kwa masharti ya sasa hawakopesheki. Kwa hiyo, tutapanua *operations* za *NMB* labda ingewezekana basi *NMB* iwe na *special windows* za kutoa mikopo kwa masharti nafuu.

Kwa sababu hawa ndiyo walengwa, *NMB* isizingitie tu kupata faida kubwa lazima iwalee hawa wananchi mpaka wafike hatua ambayo wanaweza kusema kuwa wanakopesheka kwa masharti ya kibenki ambayo tunayaelewa sasa. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Serikali sasa ipalilie njia kwa *NMB* hasa kwa wananchi walio wengi vijijini ambao ni asilimia 80 ambao wananchi wa vijijini itakuwa vigumu sana kufikia benki zingine ziondoke mijini ziende vijijini.

Kwa hiyo, mzigo wa kusogeza wananchi vijijini katika uchumi wa kifedha bado limebaki ni mzigo wa Serikali. Itumie mbinu zote kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na uchumi wa kifedha kwa sababu kipimo kikubwa kimojawapo cha maendeleo ni kutumia takwimu za kifedha. Sasa tukiwaacha wananchi katika hali hii pasipo kuwasaidia na tusiposaidia *NMB* kufika kule kwa walengwa wakubwa kwa kweli

itakuwa ndiyo tutaionyesha njia ambapo itakuwa vigumu sana kusema kuwa inaweza kushamiri ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningemaliza tu kwa kusema kuwa katika Bodi ya *NMB* iwe na uwezo wa kuelekeza hata kama kutakuwa na *management* mpya kwa sababu tumeona *NBC* miezi miwili iliyopita palikuwa na *crisis* ambapo tulisoma kwenye vyombo vya habari Bodi *I think* ilisambaratika kwa sababu ya kushinikizwa management ya *NBC*. Sasa hapa ningomba Bodi ya *NMB* kwa sababu itakuwa na Mwenyekiti ambaye anatoka kwa wenye hisa walio na hisa nyingi zaidi waweze kuelekeza kwa maslahi kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa labda tungeomba pia bodi katika kutekeleza kanuni zake waweke (*clause*) kipengele ambacho kitawezesha kama wageni wataamua kuondoka au kuuza hisa zao *reference* iwe kwa wananchi, wasiwauzie wenzao nje. Hii ndiyo itakuwa mwanzo wa *localization of NMB*. Kwa hiyo, sisi hatusemi kuwa hatuwataki wageni, hatusemi kuwa waondoke mapema, lakini kama siku ya kuamua kuwa wanataka kuuza hisa zao hii iwe ndiyo mojawapo uwezekano wa kuongezea hisa zetu katika *NMB* kwa kuweka *reference* kwanza kwa kuwauzia wananchi au taasisi za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tena naunga mkono Muswada huu ni mzuri tuiletee *NMB* mpya sisi wote pamoja na Serikali ione kuwa mzigo wake ni kupalilia na kuweka mazingira sawa kule vijijini kusudi *NMB* iwafikie wale walengwa ambao ni wananchi wa vijijini. Ahsante sana nakushukuru. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na wataalam wake kwa kuutayarisha Muswada huu kwa subira kubwa sana. Baada ya pongezi, ninaunga mkono hoja asilimia mia moja.

Hatua ya kubinafsisha *NMB* ni hatua inayohitaji ujasiri mkubwa kwa upande wa Serikali na inafurahisha kuona jinsi ambavyo Serikali yetu imeonyesha uvumilivu na ujasiri mkubwa katika kushughulikia suala hili. Napenda kutoa mapendekezo yafuatayo.

(i) Ni vema Serikali ikahakikisha kwamba matawi madogo hayafi kwani wateja walio wengi katika matawi haya ni vikundi vya wanawake ambao wamechukua mikopo midogo midogo kutoka kwa taasisi za mikopo. Hii ni kweli kwa matawi ya *NMB* yaliyo Morogoro, Kilombero na Mahenge.

(ii) Uhakika wa kulinda wakopaji wadogo hususani wakulima na wanawake wanaofanya biashara ndogo ndogo vijijini na miji midogo. Tafadhali Serikali isimamie sana rai hii kwani bila mikopo midogo umaskini hautaondoka nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga tena mkono hoja nikitumaini kwamba Serikali itaendelea kulinda maslahi ya wanyonge wa Tanzania baada ya kubinafsisha Benki ya *NMB*.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono Muswada wa Sheria ya *NMB* hasa kwa kuzingatia marekebisho yaliyofaywa na Serikali ya mgwanyo wa hisa za Benki hiyo kwa uwiano wa asilimia 51 - Serikali na asilimia 49 kwa muungano wa wawekezaji mahiri.

Pamoja na kuunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha yapo masuala kadhaa ambayo Serikali budi kuzingatia wakati wa kusimamia uendeshaji wa *NMB* iliyobinafsishwa.

La kwanza, ni kwamba Serikali isijivue jukumu la kuendelea kuisaidia Benki hii hasa kwa kuzingatia *mission* yake ambayo ni *micro-financing*. Ukirejea takwimu zilizowasilishwa na Waziri kuhusu utendaji wa *NMB*, utaona kwamba pamoja na mapato ya *NMB* kuendelea kuboreka bado Serikali imeendelea kuisaidia kwa namna moja au nyingine ili iweze kuhimili majukumu yake na kupata faida. Ninakubaliana na Serikali kwamba si vema kuendelea kuipatia *NMB* ruzuku ili ifanikiwe kujiendesha. Lakini huu muungano wa wawekezaji mahiri watawezaje kuendesha matawi zaidi ya 50 ambayo ama yanapata faida ndogo au yanapata hasara; kama Serikali haibuni mikakati ya kuendelea kuisaidia *NMB*? Kwa kuwa kwa kawaida, malengo ya muungano wa wawekezaji mahiri katika shughuli za Benki ni kupata faida, Serikali itabidi iendeleo kuisaidia *NMB*.

La pili, nashauri muungano wa wawekezaji mahiri wowote watakaokuja kuendesha *NMB*, waendeleze mazuri ambayo mpaka sasa yamekuwa yakifanywa na *NMB* hasa faida ambayo imekuwa ikiongezeka. Hapa, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza Meneja na wafanyakazi wa *NMB*, Tawi la Kahama kwa kushika nafasi ya 10 na kupata faida ya Sh.183,320,075.79 mwaka 2002 kati ya Mabenki 108 yote yaliyopo nchini. Wafanyakazi kama hawa wa Tawi la Kahama na wafanyakazi wote wa *NMB* wasiachishwe kazi washirikishwe kikamilifu katika umiliki wa Benki. Ninafurahi kwamba kwa hili Mheshimiwa Mramba atalizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono kwa dhati mfumo wa mgawanyo wa hisa wa asilimia 51 kwa Serikali na wananchi na asilimia 49 kwa muungano wa wawekezaji mahiri. Kwa mfumo huo, Serikali itakuwa na kauli ya turufu kuhakikisha *central mission* ya *micro-financing* ya *NMB* inalindwa na kuendelezwa kwa vyovyote.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri kwa kuleta hoja hii wakati huu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ambayo ni vizuri yakaangaliwa wakati wa utekelezaji wa sheria hii. Suala la kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa nafasi ya kutosha kwanza kuelewa nini tafsiri sahihi ya maamuzi haya tusitoe mwanya kwa wasiopenda maamuzi haya wakapotosha ukweli halisi wa nia ya Serikali. Wawekezaji wapatiwe masharti maalum yenye nia ya kuifanya Benki hii ifanye kazi kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara ndogo ndogo pia itumike kusaidia kuinua kilimo, uvuvi, mifugo na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri apate Bodi imara ya kusimamia Benki hii maana kazi iliyo mbele yetu siyo ya kisiasa tu bali kiuchumi. Mpango wa kuchagua wajumbe wa bodi kwa kujuana tu bila kuzingatia uwezo wao na utaalam wao wa masuala ya Kibenki ni budi uachwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali kubaki na hisa 30 naukubali kwa sababu ni uthibitisho wa Serikali ya CCM kulinda na kusaidia kila mara ili chombo hiki kisitetereke kiuchumi. Ninashauri hisa hizo zisiuzwe nje ya wananchi maana hii ndiyo *thrust* ya nia ya wananchi. Natarajia kuwa maelekezo hayo yatazingatiwa ili siku moja ionekane kuwa Benki hii ni kweli *Peoples Bank*.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya sasa ni budi ikaingizwa kwa nguvu zote ili benki hii iwe mfano isiwe ni Benki itakayoporomoka baada ya muda mfupi. Tukubali kuingiza kila aina ya utaalamu katika Benki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki za wananchi - *SACCOS* na za wanaushirika popote pale walipo, nashauri ziandaliwe taratibu za kujiunga na Benki hii. Mwanzo huo utaleta msukumo mkubwa miongoni mwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashauri Serikali ituambie kwa hivi sasa hali ya *NMB* ikoje kifedha. Ni vizuri tujue kwa kuanzia tuna mtaji kiasi gani. Hili ni muhimu pia katika kuondoa kasoro za kila mtu kutoa takwimu tofauti na za mwenzake kwa nini hili litokee na Serikali inasemaje? Wananchi waambiwe ukweli wa hali ya hivi sasa. Tuanze na sura nzuri kuanzia na hapa tulipo ili Benki hii isituharibikie mikononi mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naipongeza Serikali kwa kuhitimisha awamu ya pili ya Muswada huu na la kufurahisha ni kuongezewa muda *PSRC* kwenye zoezi zima na ubinafsishaji. Kwa sababu uamuzi wa kisera ni Serikali kujitoa kwenye biashara itakuwa kosa kabisa kubakia kuendesha biashara kwenye taasisi za fedha, hii ni kama vile kwenye sera ya ubinafsishaji, sekta ya fedha ilitengewa kipengele kwa mujibu wa kisera, kutoa ruksa kwa Serikali kuendelea kufanya biashara kwenye sekta hii ya fedha hususani Mabenki. Hivyo ni sahihi kabisa kwa kutolewa na *exception clause* kubinafsisha *NMB* sasa. Tubinafsishe sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mtandao wa *NMB* uko nchi nzima hasa vijijini la muhimu basi ni kudumisha mtandao huo na huduma zake nchini. Lakini siyo kwa kujihusisha na Serikali ya Chama Tawala kwenye hatma ya amana za wananchi



zilizowekeza huko ni jukumu la Serikali kuzilinda amana hizo. Kazi hii Kikatiba, kimuundo wa sekta ya fedha ni jukumu la Benki Kuu (*BOT*). Hivyo Serikali kurudi nyuma na kujiingiza kwenye uwekezaji na uendeshaji wa *NMB* ni *duplication of efforts*. Kwa kufanya hivyo na vinginevyo dhidi ya kuuza *NMB* sasa ni kurudisha *parastatal* tena ambazo baada ya makosa itarudia tena kwenye zoezi la uuzaji au ubinafsishaji ili kunusuru hasara zitakazojitokeza. Kama amana ni Sh.395 bilioni na ukopesaji ni Sh.18 bilioni ambayo ni sawa na asilimia chini ya 6 ni dhahiri kabisa kwa shughuli za Benki hii ni kwa kutumia amana zilizowekwa na wananchi na hivyo ni kweli kabisa inaendeshwa kwa hasara. Hili linaashiria umuhimu wa:-

- (a) Kuwekeza zaidi kwenye benki hiyo;
- (b) Kuunda *bank products* zaidi ili waweze kuunda faida;
- (c) Pamoja na undaji huo, bidhaa au *products* hizo mpya za Benki zielekezwe:-
  - (i) Kwa *macro-economy* - wananchi wawekezaji wadogo wadogo; na
  - (ii) Kuwekeza kwenye vyombo vingine vya fedha ili Benki ipate faida kwa amana zilizokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawaje wengi wamezungumzia juu ya *capital structure*, kimsingi mgao wowote ule wa hisa utakaohakikisha utumiaji taaluma sahihi ya Kibenki taaluma itakayotolewa na mwenye uchungu na uwekezaji utakao hakikisha huduma bora na faida utatosha bila shaka yoyote ile. Wazo linalotisha kwenye kugawia hisa nyingi kwa wananchi ni suala la uwakilishi. Nakubali Watanzania wengi wawekeze kwenye benki hii lakini bila kuwa na kikundi maalum *strategic investor* cha kuendesha shughuli za Benki ubadhilifu utatokea. Haitakuwa na tofauti na pale Serikali (kwa niaba ya wananchi) ilipomiliki hisa zote kwenye mashirika ya umma, tukateua Mameneja Wazalendo, Watanzania wenzetu ambao kwa sababu ya:-

(i) Taaluma;

(ii) Kutokuwa na uchungu na uwekezaji tukajifilisi wenyewe mpaka kufikia hatua ya kubinafsisha makampuni haya ya umma. Sipingi *capital structure* ya 51% kwetu na 49% kwa *strategic investor* ila tu hii itakuwa imeifanya Serikali ikiuke lengo la awali la kujitoa kabisa katika biashara. Kwa kuzingatia historia ya uzalendo wa Watanzania kupenda nchi yao, Serikali ya Chama Tawala itaendelea kupenda kwa mgao wowote ule wa hisa kwa kutimiza yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha haki za wafanyakazi zinalipwa na kuepusha kabisa migogoro inayofanana na ile ya *NBC*.

(b) Kudumisha huduma ya kibenki itolewayo sasa na *NMB* kwa wananchi. Nasema haya kwa sababu azma ya kuanza Benki zetu, sera iliyoandaliwa na Serikali ni kuanzisha *Community Banks* benki hizi zikianzishwa sawasawa hofu ya kusitisha huduma haitakuwepo. Naunga mkono Muswada huu kikamilifu.

**MHE. LUCAS L. SELELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *NMB* imerithi kutoka *NBC* iliyokuwa ikiwahudumia Watanzania tangu mwaka 1967 na hivyo ni chombo muhimu mno kwa uchumi wa nchi hii na hata kwa kuhudumia jamii hasa katika maeneo mengi vijijini, Wilayani, naomba uthibitisho wa yafuatayo:-

- Ni namna gani Serikali itasimamia kuendelea kwa matawi yaliyoko Wilayani ambayo yanahudumia wananchi?

- Ni namna gani Serikali itakuwa na sauti hasa pale wawekezaji watakaponunua 49% na pale wananchi watakaponunua 21% kwa sababu mwenye hisa nyingi ndiye mwenye sauti ya kuamua?

- Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha za kilimo katika Benki nyingine kwa mfano *EXIM*, *TIB* na kadhalika. Je, siyo vema tukatumia *Bank* hii yenye mtandao mkubwa?

- Je, ni wakati muafaka sasa Benki hii kupewa leseni?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina kigugumizi chochote na Muswada huu. Kwa maana hiyo, naunga mkono hoja kwa kiwango chote. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, wananchi katika hili, wanakubali kwa masharti yafuatayo:-

- (1) Wananchi na Serikali yao wabakiwe na kauli ya uamuzi wakati wote.
- (2) Benki hii ina sifa ya kutumiwa na maskini waandaliwe dirisha lao, wasitupwe nje.
- (3) Matawi yote yaliyopo yaimarishwe, yasifungwe na tuongeze mengine zaidi.
- (4) Watumishi wa Benki hiyo walindwe na ajira zao ziwe salama.
- (5) Tutumie Benki hii kama nyenzo ya kuondoshea umaskini vijijini/mijini.
- (6) Tuweke dirisha maalum la kutolea mikopo (bila urasimu mrefu)
  - (i) Wakulima wadogo wa vijijini;
  - (ii) Kundi maalumu la wanawake;
  - (iii) Kundi maalum la vijana wetu;
  - (iv) Kundi maalum la wazee.
- (7) Benki hii itumiwe kibiashara na zile:-
  - (i) Benki Kata zilizoanzishwa vijijini;
  - (ii) Vyama vya Kuweka na Kukopa.
- (8) Iwe mfano wa kuigwa na Benki zingine.
- (9) Serikali iwe mlezi mkuu wa Benki hii.

- (i) Isizorote tena;
- (ii) Isife;
- (iii) Isisinzie kishughuli na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo tukiilea vizuri Benki hii, itakua na kuimarika vizuri.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa lengo la kuiboresha lakini zaidi kuorodheshwa katika Wabunge ambao wametoa maoni yao kuhusu hatma ya Benki hii muhimu nchini, *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka wazi kwamba ninaunga mkono hoja hii. Kwa msingi huo, ili kuhakikisha *NMB* imeendelea kuwa ni Benki inayohudumia wananchi wengi katika Wilaya zote nchini, ninashauri yafuatayo:-

- (1) Serikali ihakikishe hakuna tawi la *NMB* hata moja litakalofungwa kutokana na sababu yoyote ile.
- (2) Pale ambapo idadi ya watu ni kubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Arusha pawe na tawi zaidi ya moja yakiendeshwa vizuri yatatoa faida kubwa.
- (3) Pale penye shughuli za uzalishaji mfano Geita, Kahama na Simanjiro wawe na matawi yao.
- (4) Wafanyakazi wote waendeleo na utumishi chini ya Menejimenti mpya bali haki zao zote ziwe wazi.
- (5) Serikali isijitoe hadi itakapothibitisha kwamba wananchi wanaweza kununua hisa zake zote.
- (6) Ikitokea wananchi hawakuweza kununua hisa zote 21, zinazobaki Serikali isisite kuzichukua. Lengo ni kwamba 51% lazima zibaki kuwa ni za Serikali na za wananchi.
- (7) Iteuliwe Menejimenti mahiri yenye moyo wa kizalendo kuiendesha *NMB* kifaida na kuepusha migogoro inayoweza kudidimiza maendeleo yake.
- (8) Taarifa ya *NMB* ni vema ikawa inatolewa mara kwa mara ili wananchi waelewe nini kinachoendelea.
- (9) Benki iendeleo na ipanue utoaji wa mikopo yenye gharama nafuu sana kwa wananchi ambao ni wakulima wadogo wadogo, wafugaji wadogo wadogo na wafanyabiashara ndogo ndogo.
- (10) Uwepo mpango wa kukopesha wananchi wanaojiendeleza kielimu. Elimu nayo sasa ikopesheke toka Benki ya Wananchi. Watu wengi wanapenda kusoma lakini hawana fedha za kulipia karo.

(11) Hisa zigawanywe kwani haiwezekani wananchi kukubali kununua hisa ambazo wanajua hakuna gawio. Hakuna (sio wengi) watakaokubali kununua hisa wakati wanajua kwamba hakuna gawio. Gawio lisipokuwepo, *NMB* itakosa wananchi wa kuinunua. Hii itaua lengo la ubinafsishaji wa *NMB* kwa wananchi kuwa na hisa kubwa.

Baada ya kusema hayo ambayo nataka yaonekane katika kumbukumbu za leo kwamba nilikuwepo na nimetoa mchango wa mawazo yangu katika hoja hii nzito na ya kihistoria. Naiombea *NMB* mpya mafanikio. Narudia kutamka kwamba naunga mkono hoja hii.

**MHE. MUHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake wote wawili kwa kuwasilisha mbele yetu azma ya Serikali ya kuendeleza na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) kwa vitendo. Kutokana na hali iliyoku nayo Benki hii ya *NMB* ni dhahiri kuwa sasa umefika wakati iweze kubinafsishwa ili wananchi walio wengi wa Benki hii ambao wengi wao wako vijijini wafaidike

Kutokana na kuwatakia mema wananchi wa nchi hii, kwa upande wangu naiomba Serikali iheshimu uamuzi wa pamoja kati ya Serikali na Wabunge kwa kufuata mgawanyo wa hisa kama zilivyogaiwa asilimia 21% ziwe kwa Watanzania wenyewe asilimia 30% ziwe mikononi mwa Serikali ambayo ni lazima iwepo kwa muda mrefu katika kushikilia hisa hizo na asilimia 49% ziende kwa kampuni au taasisi za nje hilo ni wazo zuri.

Lakini la msingi ni kuwahusisha zaidi wafanyakazi wa *NMB* katika ununuzi wa hisa na kusimamia kidete haki zao bila kutokea mvutano na usumbufu kama zinavyotokea kwenye taasisi nyingine. Ningeomba huu uwe mfano wa kusoma kasoro zote zile ndogo ndogo ambazo zilijitokeza hapo nyuma. Leo hii sio vema tukaona *NMB* baada ya kubinafsishwa tu ndio mwanzo wa matatizo na mizozo isiyo na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, napenda kutamka wazi naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Aidha, nashauri Serikali ihakikishe inakua na *golden share* ili iweze kuendelea kulinda maslahi ya Watanzania hata baada ya Serikali kuuza hisa zote. Utaratibu wa *golden share* umetumika nchi nyingi duniani kama vile *Malaysia, Singapore, Britain* na kwingineko. Utaratibu huu utaiwezesha Serikali kuwa na kura ya turufu ya kuzuia mambo yasiyokuwa ya maslahi ya Taifa kufanyika. *Golden share* itawaondolea wasiwasi Watanzania na itawahakikishia maslahi yao (Watanzania) kuendelea kulindwa hata baada ya *NMB* kubinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameonyesha nia ya dhali kuhakikisha maslahi ya Watanzania yanalindwa na kwa kuwa Serikali ya awamu ya tatu imefanya kazi kubwa ya kurekebisha uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania, ni matarajio yangu kwamba Serikali itaendelea kusimamia maslahi ya Watanzania hata baada ya *NMB* kubinafsishwa. *Golden share* itaiwezesha Serikali kulinda maslahi ya Watanzania hata baada ya *NMB* kubinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii mia kwa mia kwa manufaa ya nchi yetu na watu wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, *share* zinazotengwa kwa wananchi zigawanywe Kimkoa kwa sababu Mikoa ya Dar es Salaam na jirani watakimbiliana *shares* zote na Mikoa ya mbali kama Shinyanga, Ruvuma, Rukwa, Kigoma na Kagera watachelewa.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa nini kulikuwa na malumbano ya muda mrefu kuhusu nani apate asilimia ngapi katika *NMB*?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hali inaonyesha kuwa matawi yatabakia kwa idadi ile ile hivyo kuna haja ya kupunguza wafanyakazi? Kama ipo haja yapo maandalizi ya mafao hayo? Kama matawi yote yatafanya kazi ni kigezo gani kitatumika kuyaendeleza matawi hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, lengo la Serikali la kuwa na asilimia ni ili kutoa lishe (*financially*) ili benki hii iimarike. Baada ya Muswada huu kupita na kuwa sheria, je, Bodi ya hivi sasa itaendelea kuwepo? Nne, kuna mpango gani wa muda mrefu juu ya benki hii kufika Vijijini ili angalau kuimarisha uchumi wa nchi hii?

Tano, biashara za kibenki ni ngumu sana na Mabenki mengi ya kigeni ni *blotting paper* badala ya kuwa dodoki na kufyonza uchumi wa nchi hii. Serikali iwe makini kuona kwamba inabanana kwa karibu sana na sheria ya *Financial Institute*. Pongezi kwa wafanyakazi wa *NMB*, wafanyakazi wa Wizara ya Fedha, *BOT* na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Fedha, Manaibu Waziri wote kwa kuwa makini katika kusimamia suala hili la *NMB*. Naomba sana sana tuzungumzie uchumi sio siasa katika vyombo vya fedha. Mwisho tuwe pamoja tuwe makini katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo napenda kuchangia machache yafuatayo:-

(1) Jina zuri la *NMB* libakie kwa vile tayari wananchi wengi wanalipenda.

- (2) Wawekezaji waje na mkakati wa kupanua shughuli zake na kufungua matawi katika kila Wilaya na Jimbo (hasa Bara) za nchi yetu.
- (3) Wakati wa uuzaji wa hisa kwa wananchi basi ziuzwe katika matawi yake yote ya nchi nzima ili kila pembe ya nchi yetu wananchi wapate fursa ya kuzinunua.
- (4) Kwa *consortium* ya wawekezaji wale watakaokuwa na mipango mizuri na ubia wa kutosha na benki na au asasi za fedha za Watanzania ili Watanzania wengi zaidi tuwe na hisa.
- (5) Msisitizo uwe ni *Microfinance* katika kuwapatia mikopo wafanyabiashara wadogo wadogo hasa wakulima, wafugaji, wavuvi, wachimbaji vito, madini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tena naunga mkono hoja, ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii. Naomba niwataje kwa majina ambao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Raphael Mlolwa na Mheshimiwa Leonard Shango. (*Makofi*)

Pia waliochangia kwa maandishi ni mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud na Mheshimiwa Lucas Seleli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hao nawashukuru sana kwa michango yao Kwa bahati mbaya kutokana na hali ya muda siwezi kuwajibu kila mmoja na hoja yake. Lakini nitajaribu kujibu kwa mafungu kwa mambo waliyozungumzia. Niseme tu kwa sasa hivi kwamba hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha kwa bahati nzuri kwa sababu ilikuja kwa maandishi nitaichukua na kuifanyia kazi kama sehemu ya rejea ya majadiliano yetu tutakayofanya na hao wawekezaji. Nafikiri ilikuwa nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala kwa nini *NMB* ibinafsishwe sasa. Sababu kwa kweli ni mbili ya kwanza Serikali toka mwaka 1997 imekuwa ikiandaa benki hii ili ibinafsishwe. Ni sawa na ng'ombe aliyekuwa amekondeana Serikali imekuwa ikimlisha huyu ng'ombe sasa amefika mahali pa kupeleka mnadani kwa sababu anaonekana sasa anauzika. Toka mwaka wa 1997 ni Serikali iliyokuwa ikiilea benki hii na imeilea kwa namna gani, kwanza imeipa leseni ya muda ya kufanya kazi ambapo

ingekuwa ni benki ya kawaida iliyokuja kuomba leseni ya biashara ya benki isingeliruhusiwa kwa sababu haikuwa inatimiza masharti.

Lakini kwa sababu huyu alikuwa mtoto wa nyumbani alikuwa amezaliwa wakati huo, basi tumeendelea kumpa ruhusa ya kufanya biashara pindi akitimiza masharti yaliyotakiwa. Mojawapo ya ushahidi ni kwamba Serikali imeajiri meneja anaitwa DAI ile kampuni ya Marekani ambayo imekuwa ikiendesha benki hii toka mwaka 1997. Serikali imekuwa ikiipa benki hii biashara za upendeleo kwa mfano hata kwenye bajeti hii tuliyonayo ninyi wenyewe ni mashahidi tuliamua kwamba mishahara yote ya watumishi ipitie kwenye benki hii peke yake na hata mngerudi leo kwenye Bajeti, Serikali imetenga shilingi bilioni 9 kuilipa benki hii kwa kazi hii ya kupitishia mishahara ya watumishi wa Serikali. Hakuna benki nyingine yoyote iliyopata biashara hiyo wala pesa hiyo. (*Makofi*)

La tatu kwenye hilo, ni kwamba sheria yenyewe iliyoanzisha benki ya mwaka 1997 ambayo ndiyo sasa tunataka kuifuta imemtaka Waziri wa Fedha abinafsisha benki hii na mimi nanukuu kwenye hiyo sheria "*National Micro Finance Bank Incorporation Act 1997*" ambayo tunaifuta leo ambayo ilipitishwa na Bunge hili mwaka 1997 na kwenye kifungu cha 15 (1) kinasema *It shall be the duty of the Minister* "*(The Minister)*" hapa ni Waziri wa Fedha, *to work towards the early privatization of the Bank*. Kwa hiyo, mimi niliwajibika kwa vyovyote vile kubinafsisha benki hii mapema. *Early privatization* kidogo ningechelewa! Kwa hiyo, nadhani ningepongezwa kwa kutosahau kipengele hiki ndani ya sheria ile iliyonilazimisha kubinafsisha. (*Makofi/Kicheko*)

*Point* ya pili, kwamba tunabinafsisha kwa asilimia 51 kwa 49. Lakini tusingahau hii *point* ambayo nilieleza jana kwenye Kamati ya Fedha kwamba inawezekana kabisa ile asilimia 49 ikazidi kupungua kwa sababu nimesema kwenye hotuba yangu na nitaelekeza hivyo kwamba tutaandika kwenye tangazo la kuuza benki hii, kwamba mwekezaji wa nje atakayeshirikisha Watanzania atapendelewa katika kupata hiyo benki.

Kwa hiyo, akija mtu peke yake na akija aliyesindikizwa na Watanzania huyo atapewa nafasi zaidi ndani ya benki hii. Kwa ile asilimia 49 usije ukashangaa ukakuta pengine kuna asilimia 9 ya Watanzania pia ndani ya ile asilimia 49 au 10%, au 20% kadri watakavyoelewana wenyewe.

Kwa hiyo, mimi naona kabisa uwezekano wa baadhi ya taasisi hizi kuja kuomba kuingia kwenye benki hii na Watanzania kwa sababu huko nyuma tumekuwa tukipata barua za watu waliokuwa wanatambia mambo kama hayo. Huko nyuma tumekuwa tukipata barua za watu waliokuwa wanasema hata tungekuja na Watanzania itafika siku tuuze hisa zetu kwa Watanzania na sisi tuondoke. Kwa hiyo, kama hawa wakiomba sasa inawezekana kabisa zile asilimia 49 zikawa ni za watu wengine. Kwa hiyo, mimi nina matumaini kwamba ukweli tusishangae ikafika siku tukaona asilimia 60 zikawa za Watanzania, asilimia 70 zikawa za Watanzania kwa maana hiyo pana niliyozungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imeulizwa kwa nini *National Bank of Commerce* imefunga matawi Mjini Kibaha. *National Bank of Commerce* ilifunga Matawi Kibaha kwa kuelewana na Benki Kuu ya Tanzania. Hawakujikurupukia na kufunga. Ni Benki

Kuu ya Tanzania kwa kusikiliza sababu zao iliwaruhusu wafunge hilo tawi. Lakini papo hapo Benki Kuu isiiruhusu *National Micro Finance Bank* kufunga kwa hiyo, pale Kibaha mimi nasema ni baraka maana mshindani mkuu wa *NMB* amejiondoa mwenyewe tena kwa kibali cha Benki Kuu. Kwa hiyo, *NMB* imebaki pale sasa inaunguruma na itaendelea kunguruma kule Kibaha mpaka atakapojitokeza mtu mwingine. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama itajitokeza kwenye maeneo mengi benki iliyopo ikaondoka ikapisha *NMB* mimi nitakuwa mtu mwenye raha sana kwa sababu itaipaa *NMB* biashara nzuri bila ushindani mkali.

Lakini pamoja na hayo kama ile itachukuliwa kwamba ni point mbaya kwa *NBC* kufanya hivyo lakini wakati ikifunga tawi lake Kibaha imefungua pia matawi mapya mahali kwingine; Karatu na Mheshimiwa Mbunge Dr. Willbrod Slaa ni shahidi *NBC* imefungua tawi jipya na vile vile Geita Waheshimiwa Wabunge kutoka Geita hapa ni mashahidi, *NBC* imefungua tawi jipya. Kwa hiyo, hawawezi kufanya kienyeji kwa sababu Benki Kuu iko pale ikifanya kazi yake ya kusimamia (*regulation*).

Kwenye kamati kulitokea wasiwasi kwamba hawa watu wanafunga matawi na majengo wanauza, sasa ni kitu gani hiki? Benki siyo majengo, benki ni majengo huko tulikotoka, maana lazima uwe na majengo yenye uzio na *security* kali na *grill* n.k Benki ni *software* unaweza usishangae ukakuta benki iko kwenye *container* lakini mitandao yake ni ya kimataifa itafanya biashara tu.

Kwa hiyo, wala tusihangaikie majengo yako wapi tukiliona sawa, tusipoliona tusihangaikie; tuulize fedha iko wapi na fedha ziko kwenye mtandao. Kwa maana hiyo ndiyo maana kunatokea utata mara nyingine watu wanauliza, sasa hizi fedha za benki zinawekwa wapi? Fedha za Benki niliwahi kusema hapa siku moja, fedha za benki zinakwenda dunia zinazunguka tu kwa sababu kama unaendesha Benki kubwa kama *NBC* au hata hii *NMB* ukapata mtu aliyekuja kukopa hapa kutoka Kenya arudishe ndani ya mwaka kwa nini usimkopesha ukatengeneza biashara; maana huwezi kukalia fedha ndani ya benki. Mwiko mmoja wa *banker* ni kukalia fedha na hata ukizidi kuketilia Benki Kuu itakuja itakuambia usiketilie, zungusha, Mopping up lazima uzungushe fedha yako, huwezi kuketilia. Kwa hiyo, usishangae ukisikia pesa ya Tanzania inafanya kazi New York, pesa ya New York inafanya kazi hapa Tanzania. Hata sasa hivi, hawa watu wanaokuja kuanzisha migodi hapa tuliokuwa nao juzi hawakukopa huku Tanzania, wamekwenda kukopa mabenki ya nje; hela ya nje inafanya Tanzania, tunafaidika, kesho watalipwa na ndivyo ilivyo sasa hivi. Kwa hiyo, hili lisitiwe hofu sana Waheshimiwa Wabunge, la maana ni hesabu zake ziko wapi? Ni sawa na ni sahihi? (*Makofi*)

Hoja nyingine iliyokuwa imejitokeza hapa ni hii ya *NMB* kupewa leseni ya kudumu. Hiki tunachofanya leo ndio mwanzo wa *NMB* kupewa leseni ya kudumu kwa sababu kama nilivyokuwa naeleza jana kwenye kamati; ni kwamba tukishawawekea kivuko cha leo kutoka huku ng'ambo ya Mji wa Dar es Salaam karibu na Ofisi ya Mipango tukielekea Kigamboni tukawawekea kivuko, tunawawekea.



Tukishafika kule Kigamboni ndiyo tutaanza kufanya kazi ya kwanza ya kusema sasa tunauza, wananunua huko huko, huko huko ndipo wanapatia leseni kwa sababu sasa wameshaweka ule mtaji utakuwa umetosheleza na masharti mengine ambayo yalikuwa magumu huko nyuma yatakuwa sasa yameshatekelezwa pindi wakifika Kigamboni. Kule kule watapata leseni kwa sababu huwezi kuuza leo halafu ukamnyima mtu kuendesha biashara ambayo wewe mwenyewe ulimuuzia. In other words huwezi kumfunga mikono na huku umeshachukua fedha yake. Kwa hiyo, sasa hivi tunavyozungumza kwa kutegemea uharaka wa kupata huyu mwekezaji *NMB* itajiendesha kama benki nyingine.

Hoja nyingine kwamba *NMB* kwa sasa ina teknolojia ya kutosha. Ningependa kuzungumzia hili suala la watumishi na teknolojia. Sisi hatujasema kwamba *NMB* haina watumishi wenye ujuzi wa kibenki kwa sababu watumishi hawa hawa ni wale waliokuwa kwenye *NBC* ya zamani wengi wao ni hawa. Kwa hiyo, wale waligawanyika mara mbili, kiasi wakaenda *NMB* na tunao mpaka leo, kiasi wakaenda *NBC* wakabaki huko huko *NBC* na tunao mpaka leo. Kila benki *NBC* na *NMB* haijaongezea watumishi wapya. Kwa hiyo, watumishi wako wa kuweza kufanya kazi za kawaida za kibenki.

Waheshimiwa Wabunge, ni ukweli kwamba kwa bahati mbaya sana, ingawa Tanzania tulifanikiwa sana kufundisha Makarani na watu wa Vyeo vya Kati katika Benki na wanajua, lakini hatukufundisha watu wa Vyeo vya Juu katika Benki. Ndiyo maana hivi leo tunavyozungumza tunayo Benki moja ya *Microfinance* inayoitwa *Akiba Commercial Bank*, Meneja wake ni Mkenya; Benki nyingine kubwa inaitwa *Standard Chartered Bank*, Meneja wake ni Mzimbabwe. Kwa sababu kwa ngazi fulani sisi Tanzania tulikuwa hatujafundisha watu wengi wanaoweza wakaendesha Benki. Kwa hiyo, wataalam tunao lakini aina aina hatuna.

Ya pili, utaalamu. Hata wakati tukibinafsisha, kulikuwa kama *computer* kule *Bank*. Kuna utaalamu na wataalam. Utaalamu kwa maana ya teknolojia, kuna makompyuta, yalikuwepo lakini *computer* siyo teknolojia, ni aina ya teknolojia. Lakini teknolojia tunayozungumza hapa ni kitu kinachoitwa *software*. Kuna *Banking Software*, kuna *Microfinance Software*, kuna *software* za kazi mbalimbali zinazofanyika ndani ya Benki ambayo ni *computer plus*. Kwa hiyo kuwa tu na lile dude linaitwa *computer* haitoshelezi, lazima uwe na ile *software* ambayo unaweza ukaitumia. Hivi ndiyo vitu tunavyotafuta, wataalam wa aina fulani fulani na *software* ya aina fulani fulani. Kwa hiyo, mimi lazima nikiri kabisa kwamba hatujawahi kusema kwamba kwa hapa tulipo, Benki ile haiwezi kujiendesha, itajiendesha kwa hapa tulipo lakini kwa namna Benki nyingine zinavyojiendesha, sisi lazima tufikie viwango vile ili tuweze kushindana nao katika biashara.

Kuhusu hatma ya wafanyakazi. Wafanyakazi kama nilivyosema ni wale wale waliokuwa *NBC*. Jinsi tutakavyouza hiyo Benki, tutauza kama ilivyo. *As is where is*. Kwa hiyo, wafanyakazi waliopo watabaki hapo hapo walipo na kwa kweli kwa kufanya hivyo tutafungua mlango kwa wao kuweza kuingia kwenye mkataba wa hiari na mwajiri. Hivyo sasa kwa sababu ile Benki ni *specified* ilikuwa hairuhusiwi kuingia kwenye mkataba wa hiari na mwajiri kama vile watumishi wa *NBC* walivyokuwa wanadai. Hata hivyo wakati na wenyewe walikuwa wanadai mkataba wa namna hiyo, mimi nilisema

tuendelee, tuanze majadiliano nao ili yule akija akute angalau tumefika ngazi ya maelewano na aridhie hayo maelewano. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba hawa nao wataingia kwenye mkataba wa hiari na huyo mnunuzi mpya. Kwa hiyo, kwa wafanyakazi kuna vitu vitatu vitafanyika. Watabaki, wataingia kwenye mkataba wa hiari, wataendelea kufundishwa na watapewa fursa mahsusi ya kununua hisa ndani ya Benki hii wakati ukifika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba Serikali haikushirikisha *management* katika ubinafsishaji; ile *process* ya ubinafsishaji ina nafasi ya *management* na ina nafasi ya Bodi na kusema kweli yule Mwenyekiti wa Bodi huwa anahusishwa sana wakati wa ubinafsishaji. Kwa hiyo, hawa wamebinafsishwa katika ile *process* ya ubinafsishaji na hakuna wasiwasi kabisa. Lakini vile vile sisi hapa ile Benki ni yetu mia kwa mia, kwa hiyo tunapojadili sisi kuiuza Benki hii sisi ndiyo wenye Benki, yaani sisi Wizara ya Fedha na Serikali ndio wenye Benki na kwa vyovyote vile hatuwezi kufanya jambo lolote lenye madhara makubwa kwenye Benki hiyo. Kwa hiyo, hilo lisitutie wasiwasi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ile hoja kwamba kama Serikali imeshindwa kupeleka huduma za kibenki Vijijini itahakikishaje kwamba huduma hizi zitafikishwa Vijijini. Kwanza Benki itaendelea kuitwa *National Microfinance*. Jina! Jina litabaki *National Microfinance Bank*. Kuna kitu ndani ya jina. (*Makofi*)

Ya pili, tunayo sera ya *Microfinance* ambayo imeshapita na mwaka juzi 2001 niliwagawia Waheshimiwa Wabunge. Sera ile bado iko ni sera ya Serikali na vyombo vyote vya *Microfinance* pamoja na Benki hii vitaendelea kufanya kazi chini ya sera ile. Ni sera kubwa inayotawala Benki hii, inatawala *SACCOS* inatawala *SACAS*, inatawala vikundi vingi vidogo vidogo vya kifedha. Juzi Mheshimiwa George Kahama kwenye sheria tuliyopitisha hapa wiki hii, kuna kipengele kule ndani cha kulea vile vile *SACCOS* na kipya hizo *SACAS*, chini ya Sheria ile ya Ushirika, kuonesha kwamba Serikali ni serious. Ni wiki hii tumebadilisha Sheria ya Ushirika tukaweka kipengele cha kulea hata Vyama vya Ushirika vya Mikopo ambavyo havijakuwa Vyama kamili vya Ushirika. Tumeweka kipengele ili tuendelee kuvilea hata kama havijawa sawasawa kama ilivyokuwa imetakiwa.

Kwa hiyo, ningetaka kuwahakikishia tu kwamba Serikali hata katika huo mkataba wa mauzo tutaweka vipengele na jana tulijaribu kusoma vingine na madhumuni yatakayohakikisha kwamba Benki hii itakuwa ni Benki ya *Microfinance*. Ndiyo maana tumeweka kipengele kwenye mkataba wa mauzo kwamba ile 49 watakuwepo pia wawekezaji ndani ya ile 49 ambao wanaelewa, yaani ni Wana-*Microfinance*, ni wakareketwa wa *Microfinance*. Watu kwa mfano Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya humu ndani na Benki za Kimataifa na za humu ndani ambazo zenyewe ni Benki za *Microfinance*. Pamoja na kwamba sio nyingi sana, lakini ziko nyingi na tumekuwa tukipata enquiries za watu wa namna ile ambao wako tayari kufikiria kuingia na kwa sababu tumeiweka kwamba ni sharti la kuingia humo, nina hakika kwamba itakuwa hivyo na tumaini langu ni kwamba kama alivyokuwa amesema Mheshimiwa Leonard Shango; Wizara ya Fedha kama Wizara ya Fedha ya leo na kesho na keshokutwa, itaendelea kuhakikisha kwamba Benki hii itabaki ni Benki ya *Microfinance*. Ndiyo maana nakubaliana na ile hoja na tutajaribu kuiweka kwamba kuwepo ile dhana ya

*golden share* ili kusudi wakati wowote Wizara ya Fedha ikiona kuna jambo linataka kutokea la kupotosha dhana na mwelekeo na *mission*; jana nilizungumza sana habari za *mission*, mwelekeo na dhamira ya *Microfinance*, Serikali iweze kuingilia kati na kusema hapana. Huko mnakokwenda siyo kuzuri.

Mfano mmoja, mwenye hisa anaweza kuamka siku akasema nauza hisa zangu. Huyu mwenye *Microfinance* angeamka siku akasema anauza hisa na sisi tukaona kwamba mauzo haya yanaweza yakapotosha kule kuwepo kwa dhana ya *Microfinance* ndani ya Benki ile, tunaweza tukashika *break* tukasema hapana, sisi kama Serikali hatuwezi kukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa, Serikali ni kitu kikubwa sana. Unajua Serikali hata bila mkataba ulioandikwa, Serikali ni Serikali. Kama kuna kitu kimoja mfanyabiashara anachoogopa ni Serikali. Serikali, hata bila maandishi, ikiunguruma tu, mfanyabiashara lazima asikilize. Jana hapa nilikuwa na mtu mmoja tajiri mkubwa; huyu Bwana *Oppenheimer*, kijana mdogo ndiye aliyenunua Mwadui ya leo. Amekuja pale anapiga magoti anasema ooh, Mheshimiwa wewe ndiyo hivi, sasa nina tatizo hili, iweje; je, nyie Serikali mnatuonaje, mnafikiri sisi ni watu wazuri au wabaya, iweje! Mimi nikakaa pale nikasema usiwe na wasiwasi kijana, endelea tu lakini kila ukija piga hodi hapa uniambie umefikia wapi. (*Kicheko*)

Eh, kwa sababu Ubepari kwa tabia yake ni lazima ufanye kazi na Serikali. Ni lazima! Kwa hiyo, hawa nina hakika hata bila mkataba watapenda kujua Serikali inasema nini, Serikali inafanya nini juu ya mambo ya namna hii. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru kwa mambo mawili. Kwanza kwa kufikia hatua tuliyofikia leo. Nawashukuru sana sana kwa kufikia hatua tuliyofika leo. (*Makofi*)

Pili, wakati jambo hili lilipoanza kuna watu waliokuwa na wasiwasi; labda hawa watu wamekwishapata watu wa kuwauzia, labda wao wenyewe wanachekelea Benki hii na nini. Nataka kuwahakikishia kwamba ukweli hapa tunapozungumza hakuna jambo lolote lililofanywa, ahadi yoyote iliyofanywa, uuzaji wowote uliofanywa, mazungumzo yoyote yaliyofanywa na mtu yeyote kwa minajili ya kuiuza Benki hii, hakuna kabisa. Ningependa kuwapa *assurance*. Kama mkipitisha hii leo leo, hatua (a) inanza kwangu kuiandikia *PSRC* Jumatatu na kuwaambia sasa anzeni kazi yenu. Maana baada ya hapa inahamia *PSRC* na kuwapa maelekezo haya ninayozungumza, anzeni kazi yenu lakini kule Bungeni msisahau (a), (b), (c), (d), ilivyozungumzwa kule kwenye Kamati na ilivyozungumzwa ndani ya Bunge lenyewe. Ndiyo mwanzo wa kazi hii na mimi mwenyewe nitaismamia. Ahadi ya pili nataka kuwaambieni, mimi mwenyewe *as long as I am in that Ministry* nitaismamia kazi hii kuhakikisha kwamba *in law and in spirit* (kwa maudhui na kwa sheria) Benki hii inaelekea huko mlikotaka iende tangu tuanze mazungumzo haya toka mwezi wa Pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimalizie tu kwa kusema, tuko pamoja na ninatumaini tutasiaidiana mbele ya safari mpaka kazi hii itimie vizuri kama tulivyokuwa tumekusudia. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**MHE. WILFRED LWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na.65(4), naomba uruhusu kura zihesabiwe.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa tutahesabu, tutaita majina. Piga kengele.

*(Hapa kengele iligongwa ili Wabunge Walipo Nje ua Ukumbi wa Bunge Waingie Ndani)*

**NAIBU SPIKA:** Endelea Katibu.

Mhe. Frederick T. Sumaye	- Ndiyo
Mhe. William V. Lukuvi	- Ndiyo
Mhe. Anna Margareth Abdallah	- Hakuwepo
Mhe. Mohamed Seif Khatib	- Ndiyo
Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete	- Ndiyo
Mhe. Zakia Hamdan Meghji	- Hakuwepo
Mhe. Balozi Dr. Pius Y. Ng'wandu	- Ndiyo
Mhe. Edgar D. Maokola-Majogo	- Ndiyo
Mhe. Daniel Ndhira Yona	- Ndiyo
Mhe. Harith Bakari Mwapachu	- Ndiyo
Mhe. Gideon Asimulike Cheyo	- Ndiyo
Mhe. Dr. Abdallah Omar Kigoda	- Ndiyo
Mhe. Prof. Juma Athumani Kapuya	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Mary Michael Nagu	- Ndiyo
Mhe. Edward N. Lowassa	- Hakuwepo
Mhe. Wilson Mutagaywa Masingi	- Hakuwepo
Mhe. John Pombe Joseph Magufuli	-- Hakuwepo
Mhe. Basil Pesambili Mramba	- Ndiyo
Mhe. Prof. Phillemon M. Sarungi	- Ndiyo
Mhe. Omar Ramadhan Mapuri	- Ndiyo
Mhe. Charles N. Keenja	- Hakuwepo
Mhe. Prof. Mark James Mwandosya	- Hakuwepo
Mhe. Joseph J. Mungai	- Hakuwepo
Mhe. Arcado Dennis Ntagazwa	- Ndiyo
Mhe. Brig. Jen. Hassan Ngwilizi	- Hakuwepo
Mhe. Balozi George Clement Kahama	- Ndiyo

Mhe. Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro	- Ndiyo
Mhe. Dr. Juma Alifa Ngasongwa	- Hakuwepo
Mhe. Andrew John Chenge	- Ndiyo
Mhe. Shamim Parkar Khan	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Maua Abeid Daftari	- Hakuwepo
Mhe. Abdislaam Issa Khatibu	- Ndiyo
Mhe. Tatu Mussa Ntimizi	- Ndiyo
Mhe. Prof. Pius P. Mbawala	- Ndiyo
Mhe. Mudhihir M. Mudhihir	- Hakuwepo
Mhe. Bujiku K. Sakila	- Ndiyo
Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda	- Hakuwepo
Mhe. Zabein Muhaji Mhita	- Hakuwepo
Mhe. Capt. John Z. Chiligati	- Ndiyo
Mhe. Dr. Ibrahim S.R. Msabaha	- Ndiyo
Mhe. Dr. Hussein Alli Mwinyi	- Hakuwepo
Mhe. Hezekiah N. Chibulunje	- Ndiyo
Mhe. Dr. Festus Bulugu Limbu	- Ndiyo
Mhe. Hamza Abdallah Mwenegoha	- Ndiyo
Mhe. Anthony Mwandu Diallo	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Abdulkader A.M. Shareef	- Hakuwepo
Mhe. Rita Louise Mlaki	- Hakuwepo
Mhe. Njelu E.M. Kasaka	- Ndiyo
Mhe. Athumani S.M. Janguo	- Ndiyo
Mhe. Dr. Aman W.A. Kabourou	- Hapana
Mhe. William H. Shellukindo	- Ndiyo
Mhe. Dr. William F. Shija	- Hakuwepo
Mhe. John Samwel Malecela	- Hakuwepo
Mhe. Eliachim J. Simpasa	- Ndiyo
Mhe. Omar S. Kwaangw'	- Hakuwepo
Mhe. Anne S. Makinda	- Hakuwepo
Mhe. Halima Omar Kimbau	- Hakuwepo
Mhe. Mgana I. Msindai	- Hakuwepo
Mhe. Isaac M. Cheyo	- Hapana
Mhe. Thomas Ngawaiya	- Hapana
Mhe. Frank G. Maghoba	- Hapana
Mhe. Muttamwega B. Mgaywa	- Hapana
Mhe. Grace Sindato Kiwelu	- Hapana
Mhe. Dr. Wilbrod Peter Slaa	- Hapana
Mhe. Teddy Louse Kasella-Bantu	- Hapana
Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare	- Hapana
Mhe. Philemon Ndesamburo	- Hapana
Mhe. Benedicto Mutachoka Mutungirehi	- Hapana
Mhe. Major Jesse J. Makundi	- Hapana
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe	- Hapana
Mhe. Janeth Edward Mashele	- Hapana
Mhe. Aisha Philipo Magina	- Hapana

Mhe. Hamad Rashid Mohamed	- Hapana
Mhe. Adelastela E. Mkilindi	- Hapana
Mhe. Mohamed Rished Abdallah	- Ndiyo
Mhe. Zuhura Shamis Abdallah	- Ndiyo
Mhe. Alhaj Shaweji Abdallah	- Ndiyo
Mhe. Mohamed A. Abdulaziz	- Hakuwepo
Mhe. Bahati Ali Abeid	- Ndiyo
Mhe. Khamis Awesu Aboud	- Ndiyo
Mhe. Kijakazi Khamis Ali	- Ndiyo
Mhe. Omar Mjaka Ali	- Ndiyo
Mhe. Salim Omar Ali	- Ndiyo
Mhe. Fatma Said Ali	- Ndiyo
Mhe. Khamis Salum Ali	- Hakuwepo
Mhe. Aziza Sleyum Ali	- Hakuwepo
Mhe. Mohamed Abully Ally	- Ndiyo
Mhe. Shahibu Ahmada Ameir	- Ndiyo
Mhe. Kheri Khatib Ameir	- Ndiyo
Mhe. Rostam Aziz	- Hakuwepo
Mhe. Faida Mohamed Bakar	- Ndiyo
Mhe. Elizabeth N. Batenga	- Ndiyo
Mhe. Joel Nkaya Bendera	- Ndiyo
Mhe. Lydia Thecla Boma	- Hakuwepo
Mhe. Zamda S. Bozzen	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Batilda Salha Burian	- Hakuwepo
Mhe. Robert Jacob Buzuka	- Hakuwepo
Mhe. Margareth J. Bwana	- Hakuwepo
Mhe. Kisyeri W. Chambiri	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Aaron D. Chiduo	- Ndiyo
Mhe. Diana Mkumbo Chilolo	- Ndiyo
Mhe. Samwel M. Chitalilo	- Ndiyo
Mhe. Anatory K. Choya	- Ndiyo
Mhe. Omar Said Chubi	- Ndiyo
Mhe. Paschal C. Degera	- Ndiyo
Mhe. Leonard N. Derefa	- Ndiyo
Mhe. Balози Ahmed Hassan Diria	- Hakuwepo
Mhe. Abdullatif Hussein Esmail	- Hakuwepo
Mhe. Bakari Shamis Faki	- Hakuwepo
Mhe. Abdallah Khamis Feruzi	- Ndiyo
Mhe. Chief Abdallah Fundikira	- Ndiyo
Mhe. Dr. Zainab A. Gama	- Ndiyo
Mhe. Dr. Lawrence M. Gama	- Hakuwepo
Mhe. Lephy Benjamin Gembe	- Ndiyo
Mhe. Jina Khatib Haji	- Ndiyo
Mhe. Dr. Haji Mwita Haji	- Ndiyo
Mhe. Ussi Yahaya Haji	- Ndiyo
Mhe. Edson Mbeyale Halinga	- Hakuwepo

Mhe. Parmukh Singh Hoogan	- Ndiyo
Mhe. Salama Khamis Islam	- Ndiyo
Mhe. Yahya Kassim Issa	- Ndiyo
Mhe. Khalifa Mohamed Issa	- Hapana
Mhe. Esmail J.R. Iwvatta	- Ndiyo
Mhe. Mwadini Abbas Jecha	- Hapana
Mhe. Shoka Khamis Juma	- Hapana
Mhe. Yusuf Kombo Juma	- Ndiyo
Mhe. Ali Said Juma	- Hapana
Mhe. Peter Kabisa	- Hakuwepo
Mhe. Charles H. Kagonji	- Ndiyo
Mhe. Janet Bima Kahama	- Hakuwepo
Mhe. Rhoda L. Kahatano	- Ndiyo
Mhe. Stephen M. Kahumbi	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Diodorus Buberwa Kamala	- Ndiyo
Mhe. Nazir Mustafa Karamagi	- Ndiyo
Mhe. Ally Amani Karavina	- Ndiyo
Mhe. Capt. Theodos James Kasapira	- Hakuwepo
Mhe. Stephen Masaba Kazi	- Ndiyo
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa	- Hapana
Mhe. Ramadhani Hashim Khalfan	- Ndiyo
Mhe. Zahor Juma Khamis	- Ndiyo
Mhe. Sharifa Mbarouk Khamis	- Hapana
Mhe. Mohamed Juma Khatib	- Hapana
Mhe. Hassan Rajab Khatib	- Ndiyo
Mhe. Juma S. Kidunda	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Aisha O. Kigoda	- Ndiyo
Mhe. Hassan Chande Kigwalilo	- Hakuwepo
Mhe. Anne Kione Kilango	- Hakuwepo
Mhe. Estherina Kilasi	- Hakuwepo
Mhe. Paul P. Kimiti	- Ndiyo
Mhe. Emmanuel E. Kipole	- Ndiyo
Mhe. Remidius Edington Kissassi	- Ndiyo
Mhe. Dr. Hassy H.B. Kitine	- Hakuwepo
Mhe. Abu Towegale Kiwanga	- Ndiyo
Mhe. Stanley Haule Kolimba	- Ndiyo
Mhe. Mwanamkuu Makame Kombo	- Ndiyo
Mhe. Parseko Vincent Kone	- Hakuwepo
Mhe. Hadija Kasola Kusaga	- Ndiyo
Mhe. William Jonathan Kusila	- Ndiyo
Mhe. Lekule M. Laizer	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Masumbuko R.M. Lamwai	- Ndiyo
Mhe. Benedict K. Losurutia	- Ndiyo
Mhe. George M. Lubeleje	- Ndiyo
Mhe. Dr. Thadeus M. Luoga	- Ndiyo
Mhe. Musa A. Lupatu	- Ndiyo

Mhe. Abdula Suleiman Lutavi	- Ndiyo
Mhe. Ernest Gakeya Mabina	- Ndiyo
Mhe. Philip Alfred Magani	- Ndiyo
Mhe. Beatus Ruzuba Magayane	- Hakuwepo
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe	- Ndiyo
Mhe. Dr. Milton Makongoro Mahanga	- Hakuwepo
Mhe. Mwanaidi Hassan Makame	- Hakuwepo
Mhe. Paul Ng'wala Makolo	- Ndiyo
Mhe. Jackson M. Makwetta	- Ndiyo
Mhe. Benito W. Malangalila	- Ndiyo
Mhe. Philip S. Marmo	- Ndiyo
Mhe. Ibrahimu Wankanga Marwa	- Ndiyo
Mhe. Robert Kaji Mashala	- Ndiyo
Mhe. Haroub Said Masoud	- Ndiyo
Mhe. Dr. Chegeni Raphael Masunga	- Ndiyo
Mhe. Zubeir Ali Maulid	- Ndiyo
Mhe. Halimenshi K.R. Mayonga	- Ndiyo
Mhe. Salome Joseph Mbatia	- Ndiyo
Mhe. Monica N. Mbega	- Ndiyo
Mhe. Prof. Simon M. Mbilinyi	- Hakuwepo
Mhe. Talala Bana Mbise	- Ndiyo
Mhe. Bakari Muhema Mbonde	- Ndiyo
Mhe. Mchande Salim Mchande	- Hakuwepo
Mhe. Mwanne Ismaili Mchemba	- Ndiyo
Mhe. Bernard Kamillius Membe	- Ndiyo
Mhe. Mariam Salum Mfaki	- Ndiyo
Mhe. Feteh Saad Mgeni	- Ndiyo
Mhe. Prof. Henry Robert Mgombelo	- Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama	- Ndiyo
Mhe. Prof. Juma Mtupa Mikidadi	- Ndiyo
Mhe. Mohamed H. Missanga	- Ndiyo
Mhe. Margareth Agness Mkanga	- Ndiyo
Mhe. Nimrod Elirehema Mkono	- Ndiyo
Mhe. George Francis Mlawa	- Ndiyo
Mhe. Oscar Thobias Mloka	- Ndiyo
Mhe. Raphael Nkuli Mlolwa	- Ndiyo
Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o	- Ndiyo
Mhe. Mohamed Aboud Mohamed	- Ndiyo
Mhe. Ali Ameir Mohamed	- Ndiyo
Mhe. Sumri Abdallah Salum Mohamed	- Ndiyo
Mhe. Elisa David Mollel	- Ndiyo
Mhe. Balozi Getrude Ibengwe Mongella	- Ndiyo
Mhe. Alhaj Ahamadi Hassan Mpeme	- Ndiyo
Mhe. Benson Mwilugula Mpesya	- Ndiyo
Mhe. Kilontsi M.M. Mporogomyi	- Ndiyo
Mhe. Felix C. Mrema	- Ndiyo



Mhe. Raynald Alfons Mrope	- Ndiyo
Mhe. Ruth Blasio Msafiri	- Ndiyo
Mhe. Dr. James Alex Msekela	- Ndiyo
Mhe. Herbert James Mntangi	- Ndiyo
Mhe. Jeremiah J. Mulyambatte	- Ndiyo
Mhe. Hasnain Mohamed Murji	- Ndiyo
Mhe. James Phillip Musalika	- Ndiyo
Mhe. Ali Machano Mussa	- Ndiyo
Mhe. Ali Sheha Mussa	- Ndiyo
Mhe. Mossy Suleiman Mussa	- Ndiyo
Mhe. Frank Michael Mussati	- Ndiyo
Mhe. Prof. Daimon M. Mwaga	- Ndiyo
Mhe. John Livingstone Mwakipesile	- Ndiyo
Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa	- Ndiyo
Mhe. Yete Sintemule Mwalyego	- Ndiyo
Mhe. Venance Methusalah Mwamoto	- Ndiyo
Mhe. Mbaruk Kassim Mwandoro	- Ndiyo
Mhe. Shamsa Selengia Mwangunga	- Ndiyo
Mhe. Ludovick J. Mwananzila	- Ndiyo
Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri	- Ndiyo
Mhe. Omar Mohammed Mwenda	- Hakuwepo
Mhe. Dr. Chrisant M. Mzindakaya	- Ndiyo
Mhe. Damas Pascal Nakei	- Ndiyo
Mhe. Abdillahi O. Namkulala	- Ndiyo
Mhe. Bernadine R. Ndaboine	- Hakuwepo
Mhe. Richard Mganga Ndassa	- Ndiyo
Mhe. Job Yustino Ndugai	- Hakuwepo
Mhe. Asha Ali Ngede	- Ndiyo
Mhe. Kingunge Ngombale-Mwiru	- Ndiyo
Mhe. Cynthia Hilda Ngoye	- Ndiyo
Mhe. Khadija Saleh Ngozi	- Ndiyo
Mhe. Hamisi Jumanne Nguli	- Ndiyo
Mhe. Ireneus Ndunguru Ngwatura	- Ndiyo
Mhe. Juma Suleiman N'hunga	- Ndiyo
Mhe. Said Juma Nkumba	- Ndiyo
Mhe. Dr. Lucy Sawere Nkya	- Ndiyo
Mhe. Paul E. Ntwina	- Hakuwepo
Mhe. Tembe Kerenge Nyaburi	- Ndiyo
Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu	- Hakuwepo
Mhe. Ponsiano Damiano Nyami	- Hakuwepo
Mhe. Esther K. Nyawazwa	- Ndiyo
Mhe. Rosemary Huria Kambarage Nyerere	- Hakuwepo
Mhe. Thomas S. Nyimbo	- Ndiyo
Mhe. Mathew Taki Ole-Timan	- Ndiyo
Mhe. Omar Juma Omar	- Hapana
Mhe. Dr. Suleiman Juma Omar	- Hakuwepo

Mhe. Karim Said Othman	- Ndiyo
Mhe. Ramadhani Nyonje Pandu	- Ndiyo
Mhe. Semindu K. Pawa	- Ndiyo
Mhe. Mwaka Abraham Ramadhanani	- Ndiyo
Mhe. Kabuzi Faustine Rwilomba	- Ndiyo
Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq	- Hakuwepo
Mhe. Hashim A.Z. Saggaf	- Ndiyo
Mhe. Mohamed Ali Said	- Hapana
Mhe. Kidawa Hamid Saleh	- Hakuwepo
Mhe. Masoud Abdallah Salim	- Hakuwepo
Mhe. Issa Mohamed Salim	- Ndiyo
Mhe. Gwassa Angus Sebabili	- Ndiyo
Mhe. Lucas L. Seleli	- Ndiyo
Mhe. Haji Juma Sereweji	- Ndiyo
Mhe. Sijamini Mohamed Shaame	- Ndiyo
Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah	- Ndiyo
Mhe. Leonard Mlumba Shango	- Ndiyo
Mhe. Henry D. Shekiffu	- Ndiyo
Mhe. Jacob Dalali Shibiliti	- Ndiyo
Mhe. Iddi M. Simba	- Ndiyo
Mhe. Sophia M. Simba	- Hakuwepo
Mhe. John E. Singo	- Ndiyo
Mhe. Mohammed Rajab Soud	- Ndiyo
Mhe. Esha Hassan Stima	- Ndiyo
Mhe. Issa Mohammed Suleiman	- Hakuwepo
Mhe. Khalid S. Suru	- Ndiyo
Mhe. Aridi Mwananche Uledi	- Ndiyo
Mhe. Dr. James Mnanka Wanyancha	- Ndiyo
Mhe. Maria D. Watondoha	- Hakuwepo
Mhe. Christopher Semanini Wegga	- Ndiyo
Mhe. Martha Michael Wejja	- Hakuwepo
Mhe. Mzee Ngwali Zubeir	- Ndiyo
Mhe. Joseph J. Mungai	- Ndiyo

*(Hapa Mheshimiwa Asha Ali Ngedede Alitoka nje ya Ukumbi)*

**NAIBU SPIKA:** Taarifa! Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Naomba nipige kura.

**NAIBU SPIKA:** Unasemaje?

Mhe. Edward Nziriye Ndeka - Ndiyo *(Makofi)*

Mhe. Lydia Thecla Boma: Mimi napiga kura ya Ndiyo! *(Makofi)*

*(Hapa Kura Zilihesabiwa)*

## MATOKEO YA KURA

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 65 Fasili ya 6, naomba kutangaza kwamba walioafiki ni kwa kura za Ndiyo ni 219 na waliosema kura za Hapana ni 26. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa matokeo haya sasa natamka rasmi kwamba walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya *National Microfinance Bill* ya Mwaka 2003  
(*The National Microfinance Bank Limited Incorporation (Repeal) Bill, 2003*)**

Jina la Muswada halina marekebisho

*(Jina la Muswada lilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila marekebisho)*

Kifungu cha 1  
Kifungu cha 2  
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila marekebisho)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu kipyua cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila marekebisho)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya *National Microfinance Bill*  
ya Mwaka 2003 (*The National Microfinance Bank  
Limited Incorporation (Repeal) Bill, 2003*)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya *NMB* yaani *(The National Microfinance Bank Limited Incorporation (Repeal Act, 2003))*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada huo sasa ukubaliwe rasmi. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kupitishwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa)*  
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa katika Mkutano huu wa 13 sasa zimemalizika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hoja ya kuahirisha Bunge.  
*(Makofi)*

### **KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa 13 wa Bunge lako Tukufu umekamilisha shughuli zote zilizokuwa zimepangwa. Katika Mkutano huu Serikali imejibu maswali 130 ya msingi na mengine mengi ya nyongeza. Aidha, Bunge lako Tukufu limekubali na kupitisha Miswada ya Sheria minane ambayo itakapokuwa Sheria itasaidia sana kuimarisha usimamizi na utawala wa Sekta zinazohusika. Tunapita katika mabadiliko mengi ya kiuchumi na kijamii ambayo yanapewa msukumo mkubwa na utandawazi pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Hivyo ni muhimu kila mara tufanye mabadiliko ya Sheria zetu ili ziweze kukidhi mabadiliko haya. Tusipofanya hivyo usimamizi na hata wakati mwingine udhibiti wa athari za mabadiliko hayo unakuwa mgumu au hata kushindikana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Vyama vya Ushirika wa mwaka 2003 uliopitishwa una lengo la kuvisaidia vyama vya Ushirika kujengeka na kuimarika kiuongozi na kiutendaji ili viweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Vyama vya Ushirika bado ndiyo tegemeo kuu la wazalishaji wadogo wadogo iwe katika kilimo au shughuli nyinginezo. Kulegalega kwa ushirika iwe katika ngazi ya chini ya vyama vya msingi au ngazi ya juu kabisa kutachelewesha kwa kiasi kikubwa kujengeka

kwa uwezo wa wazalishaji wadogo kupambana na umaskini. Upo ushahidi kuwa pale ambapo wanaushirika wamefanikiwa kujenga ushirika imara wameweza vile vile kujiimarisha kiuchumi kwani wameweza kupambana na wafanyabiashara wa kati ambao mara kwa mara wanazingatia faida zaidi kuliko kujenga uwezo wa wazalishaji. Wito wangu ni kuwa sisi viongozi tuna dhamana kubwa ya kuwasaidia wana ushirika kutambua mabadiliko haya yanaletwa na Muswada uliopitishwa na Bunge na hivyo kuyatumia kikamilifu katika kujenga ushirika imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko yaliyopitishwa katika Muswada wa Sheria ya Kuunda Chombo cha Majadiliano ya Utatuzi wa Migogoro ya Kikazi katika Sekta ya Utumishi wa Umma wa Mwaka 2003 unatusaidia kujiwekea mazingira ya utulivu kwenye utumishi wa umma yatakayosaidia kuongezeka kwa tija. Kuwepo kwa mazingira ya maelewano na mashauriano katika sehemu za kazi ni kichocheo kikubwa katika kufikia malengo ya kazi. Migogoro na migomo kazini huleta usumbufu sio kwa waajiri tu bali pia kwa wafanyakazi wenyewe na pia kwa wadau wengine. Kwa msingi huo, kuwepo kwa taratibu zinazowezesha kuepukwa kwa hali kama hizo katika maeneo ya kazi kutasaidia sana kujenga mshikamano na maelewano kati ya waajiri na wafanyakazi katika utumishi wa umma na hivyo kuwezesha kutoa huduma bora na zenye tija kwa wananchi. Waajiri na wafanyakazi hata hivyo hawana budi kutambua kuwa tupo kwenye mazingira tofauti na yale ya uchumi hodhi. Tupo kwenye dunia ya ushindani na kwetu Watanzania tupo kwenye mazingira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo ajira nayo itanza kutazamwa kwa kuangalia soko hilo pana. Kwa msingi huo, pamoja na kulinda na kutetea haki zao wafanyakazi wa Tanzania lazima wajizatiti na kujiendeleza ili tija yao ifanane au kuzidi ile ya wafanyakazi kutoka nchi nyingine za Afrika Mashariki. Tunakoelekea, ajira haitalindwa kwa migomo au migogoro bali kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni moja ya nchi zenye mifugo wengi katika Bara la Afrika. Lakini pamoja na wingi wa mifugo hiyo, bado hatujaweza kufaidika nayo kwa sababu ya vikwazo mbalimbali. Mahitaji ya mazao yatokanayo na mifugo kwenye soko la ndani na hata la nje ni makubwa sana. Tungeweza kuuza nyama kwenye soko la Ulaya, au soko la Uarabuni lakini ubora wa nyama kutoka nchi yetu bado siyo wa kuridhisha. Moja ya matatizo yanayotukwamisha ni tatizo la magonjwa ya mifugo.

Bunge lako Tukufu limepitisha Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Magonjwa ya wanyama wa Mwaka 2003 ambao unaweka taratibu za kisheria za kuzuia na kudhibiti ueneaji wa magonjwa ya wanyama. Hivi sasa tatizo la kuenea kwa magonjwa ya wanyama linasababishwa pamoja na mambo mengine na kuhamahama kwa mifugo bila utaratibu maalum. Ni kweli kuwa wafugaji wanao uhuru wa kutafuta malisho na huduma nyingine kwa wanyama wao.

Lakini ni vyema tukubaliane kuwa uhamaji usio na udhibiti hauwezi kutusaidia katika mapambano yetu dhidi ya magonjwa ya wanyama. Wakati umefika sasa kwa Watanzania kubadilika na kuona mifugo kama rasilimali ambayo inaweza kutuletea faida nyingi zikiwemo fedha za kigeni endapo tu tutabadili utaratibu wetu wa ufugaji. Serikali tayari imechukua hatua za kuimarisha taasisi zake za utafiti na tiba ya magonjwa ya

wanyama. Jukumu kubwa sasa ni kwa wataalam wetu wa mifugo hasa katika ngazi za chini kuhakikisha wanafahamu na kuzisimamia ipasavyosheria, kanuni na taratibu hizi za ufugaji bora.

Suala la uhamaji wa mifugo vile vile limeleta sura nyingine ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Yapo baadhi ya maeneo nchini ambayo yamefanya kazi kubwa na nzuri ya kujenga na kuweka mazingira mazuri ya maelewano kati ya wafugaji na wakulima, lakini yapo mengine ambayo bado migogoro ya wakulima na wafugaji inatokea mara kwa mara.

Napenda kutumia fursa hii kukariri na kusesitiza agizo la Mheshimiwa Rais la kuwataka viongozi wa mikoa na wilaya zinazohusika kuchukua hatua zinazopasa kukomesha migogoro hiyo ikiwa ni pamoja na kujifunza kutoka kwa viongozi wenzao walioweza kujenga maelewano kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limepitisha vile vile Muswada wa Sheria ya Usafiri wa Majini wa Mwaka 2003. Nchi yetu imejaliwa kuwa na eneo kubwa la maji ya bahari na maziwa. Aidha, tunayo vile vile mito mikubwa na ambayo inaweza kutumika kwa usafirishaji. Rasilimali hizi za asili zina manufaa makubwa kwetu kwa ustawi na maendeleo ya jamii na nchi yetu.

Kwa kutumia usafiri wa majini na kwenye maziwa tunaweza kupata huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka eneo moja hadi jingine. Kama ilivyo kwa usafiri wa nchi kavu tunawajibika kuhakikisha kuwa tunazo taratibu za kisheria na za kiutawala zinazosimamia sekta hii na ambazo zinaendana na zile za kimataifa. Usalama wa usafiri wa majini ni suala muhimu sana kwa maisha ya watu na mali zao. Kwa msingi huo ni vyema tuwe na sheria ambayo itatuwezesha kulinda vyombo vinavyotumia eneo letu la bahari na maziwa na vile vile kuhakikisha kila mara kuwa vyombo vinavyotumika kwenye usafiri wa majini ni imara na vinavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya kiteknolojia yanayotokea hivi sasa na umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira katika maeneo yetu ya bahari na majini yanatulazimisha nasi kuhakikisha kuwa hatuachwi nyuma katika maendeleo ya sekta hii muhimu ya usafiri wa majini. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itawasilisha kwenye Bunge mikataba yote muhimu inayostahili kuridhiwa na nchi yetu kuhusu usafiri wa majini ili Bunge liweze kuridhia na ili kurahisisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo makubwa ya maji baharini kwenye maziwa na mito. Kwa hiyo, ni wazi kuwa uvuvi ni tegemeo la sehemu kubwa ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya mwambao wa bahari, maziwa na mito. Bunge lako Tukufu limepitisha Muswada wa Sheria ya Uvuvi wa Mwaka 2003 yenye lengo la kusimamia na kuweka masharti ya uangalisi wa sekta hii.

Katika mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia yanayotokea ni vyema tuwe na Sheria na taratibu zitakazotuwezesha kudhibiti raslimali za uvuvi na vile vile

kuwawezesha wavuvi wetu kufaidika nazo. Uchafuzi wa mazingira ya bahari, maziwa na mito ni eneo moja ambalo ni lazima Watanzania tuwe waangalifu sana kulidhibiti. Samaki wanaovuliwa wanatumiwa na binadamu kama chakula. Pale ambapo upo uchafuzi mkubwa wa mazingira samaki na viumbe wengine wa bahari watadhurika, lakini vile vile hata ubora wa samaki wenyewe kama chakula utakuwa haukubaliki. Kwa msingi huo ni vyema wananchi wote wanaoishi katika maeneo ya Pwani na mwambao mwa maziwa na mito, washiriki kikamilifu kulinda na kutunza raslimali hiyo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge pia limepitisha Muswada unaowezesha hisa za *National Microfinance Bank (NMB)* kuhamishiwa kwa Msajili wa Hazina ili sasa Benki hiyo iweze kubinafsishwa. Katika ubinafsishaji huo, hisa nyingi yaani asilimia 51 zitakuwa za Watanzania na Serikali, ambapo baadaye hatua kwa hatua hisa za Serikali zitakuwa za wananchi. Mwekezaji au kundi la wawekezaji watamiliki hisa asilimia 49. Lengo la hatua hii ni kujenga Benki ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kutoa huduma hasa katika maeneo ya Wilayani na hata Vijijini. Aidha, tahadhari pia imechukuliwa kuwa matawi yasiyotengeneza faida yasifungwe bali yaendeleo kutoa huduma. Hili linaweza kufanyika tu kwa Serikali kugharamia hasara hizo. Wito wangu ni kwa Watanzania kujitokeza kununua hisa za Benki hiyo wakati zitakapotangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada mingine iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu ni Muswada wa Sheria ya Udhhibiti wa Viwango vya Mbegu wa mwaka 2003 na Muswada wa Sheria ya Utoaji wa Huduma za Afya ya Mifugo wa mwaka 2003. Aidha, Azimio la kuwahishwa kwa uchaguzi wa Majimbo yaliyo wazi pia limepitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya muhtasari wa kazi zilizofanyika katika Mkutano huu, naomba nigusie masuala mengine ya jumla. Mpango wetu wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi unaendelea vizuri katika nyanja nyingi. Uandikishaji wa watoto unaendelea vizuri, ajira ya walimu inaendelea vizuri na uboreshaji wa majengo mbalimbali na samani za shule pia unakwenda vizuri. Aidha, taaluma pia inaendelea kuboreka. Hata hivyo, kuna maeneo yanayoonyesha udhaifu. Bado kuna watoto wanaostahili kuwa shuleni lakini hawako shuleni. Lipo tatizo la kiwango kikubwa cha watoto wanaoingia shule kutokumaliza darasa la saba kwa sababu mbalimbali kama vile utoro, watoto wa kike kutiwa mimba na kadhalika. Maagizo mbalimbali yamekwishatolewa ili kurekebisha kasoro hizi, maagizo hayo yatekelezwe kwa ukamilifu. Aidha, lipo tatizo la malipo kwa mishahara au posho kwa walimu wapya. Ubishi uliopo baina ya Wizara za Serikali ufikie mwisho na walimu hawa walipwe maslahi yao haraka. Kwa Wakurugenzi ambao hawajawasilisha orodha za walimu hao Idara Kuu ya Utumishi wawe wamefanya hivyo kabla ya mwisho wa mwezi huu. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika juhudi za kupunguza makali ya matatizo haya hasa katika yale maeneo yanayohitaji uhamasishaji wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwezi Julai 2003 hadi Septemba 2003, nchi yetu ilishiriki katika maonyesho ya Kimataifa ya maua, mboga mboga, matunda na viungo yaliyofanyika Rostock, Ujerumani. Nchi yetu ilifanya vizuri kwa kupata jumla ya

medali 34 ikiwa ni medali 15 za dhahabu, 13 za fedha na sita (6) za shaba. Aidha, nchi yetu pia ilishinda medali kubwa ya dhahabu inayoitwa Grosse Gold Medallion, nchi pia ilipewa tuzo maalum ya heshima ya Mstahiki Meya wa Rostock na nchi yetu pia ilipewa siku maalum ya Taifa la Tanzania (*Tanzania National Day*). Maonyesho hayo yalisimamiwa na Wizara ya Ushirika na Masoko. Napenda kuwapongeza sana Waziri na Katibu Mkuu wake na wataalam wote walioshirikiana nao na pia kuwapongeza sana wote walioshiriki katika maonyesho hayo hasa waliopeleka bidhaa zao kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia tarehe 4 Novemba, 2003 hadi tarehe 9 Novemba, 2003 Jijini Dar es Salaam kulikuwepo pia maonyesho ya tano ya bidhaa za sekta isiyo rasmi au kama inavyojulikana bidhaa za Jua Kali au Nguvu Kazi ya nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Aidha, mapema mwezi Desemba, 2003 tutakuwa na maonyesho makubwa ya bidhaa kutoka baadhi ya nchi za Kiarabu na zile za Kiafrika. Kuwepo kwa maonyesho haya muda mfupi kati ya miezi minne na mitano tangu maonyesho ya Kitaifa ya Biashara ya Dar es Salaam ni uthibitisho mwingine kuwa sasa Taifa letu limetambua umuhimu wa maonyesho ya bidhaa kama nafasi ya kujitangaza na vile vile kama nafasi kwa wazalishaji wetu wa ndani wakubwa kwa wadogo kuonyesha uwezo na ubunifu wao. Aidha, maonyesho haya yanatoa changamoto vile vile kwetu ya kujifunza kutoka kwa wengine jinsi ya kuboresha bidhaa zetu ili ziweze kushindana katika masoko ya Kimataifa. Maonyesho ya bidhaa vile vile yanawawezesha wazalishaji kufungua milango mipya ya masoko ya bidhaa zao kwani watu na Taasisi mbalimbali za ndani na hata nje ya nchi zinapata fursa ya kuona bidhaa hizo na hivyo kuwa tayari kuzinunua. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu katika Mkutano wake wa kumi na mbili ubora wa bidhaa zetu za viwandani na hata zile zinazotengenezwa kwa mikono na watengenezaji wadogo wadogo unazidi kuimarika. Ni wazi basi kuwa kadri maonyesho yanavyoongezeka ndivyo wazalishaji wetu wanavyoelewa mahitaji halisi ya soko na hivyo kujiwekea mikakati yao ya kuweza kukidhi mahitaji ya soko hilo.

Tanzania ni sehemu ya dunia ambapo utandawazi umerahisisha mawasiliano na ushirikiano kiteknolojia. Kwa hiyo, hatuwezi kukwepa kuingia kwenye soko la Kimataifa. Tunao wajibu wa kuendelea kujijenga na kujiimarisha ili bidhaa zetu za ndani ziweze kuwa na ubora unaokidhi matakwa ya soko la Kimataifa. Wazalishaji wetu wakubwa kwa wadogo wanalo jukumu la kujifunza kila mara na kuwa tayari kuiga mifano bora ya wenzetu watakaoleta bidhaa zao kwenye maonyesho hapa nchini. Kwa upande wake Serikali katika ngazi zake zote itajitahidi kujenga mazingira yatakayowawezesha wazalishaji wa ndani kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ukame imeendelea kutuathiri katika nyanja nyingi, kama vile kukumbwa na upungufu wa chakula, upungufu wa maji ya kunywa kwa binadamu na mifugo katika maeneo mengi nchini na upungufu mkubwa wa maji katika mabwawa ya kuzalishia umeme. Kutokana na hali hii uwezo wa uzalishaji wa umeme katika vituo vyote nchini vinavyoendeshwa kwa msukumo wa maji umeshuka kwa karibu asilimia 50 na hivyo kusababisha Shirika la Umeme Tanzania yaani *TANESCO* kununua karibu umeme wote unaozalishwa na *IPTL*.



Kwa upande wa Bwawa la Mtera ambalo ndilo lenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi maji yanayozalisha umeme mwingi zaidi maji yanayotiririka kutoka kwenye chemichemi na vijito yamepungua sana. Pamoja na ukame wa muda mrefu tatizo lingine kubwa linalosababisha hali hii ni uharibifu wa mazingira. Uharibifu wa mazingira husababisha chemichemi kukauka kwani miti inakatwa ovyo na uchomaji wa moto kwenye milima na mbuga nao umeongezeka kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua kulisaidia Shirika la Umeme nchini ili liweze angalau kumudu baadhi ya gharama kubwa za kununua umeme kutoka *IPTL* na vile vile kuondoa kodi katika mafuta kwa ajili ya mitambo inayotumia mafuta. Athari za ukosefu wa umeme kwa uchumi wa Taifa ni kubwa hivyo Serikali itafanya kila linalowezekana kukabiliana na tatizo hili. Hata hivyo, ni vyema wananchi nao watambue kuwa katika mazingira kama haya, ni wazi kuwa *TANESCO* watafungukiwa uwezo wa kusambaza umeme hasa kwa maeneo mapya kwa kasi ambayo walitarajia. Aidha, ni vema sasa sote tukawa waangalifu na matumizi ya umeme katika maeneo yote ya kazi na majumbani. Kila mmoja achukue tahadhari ili tuepoke matumizi ya umeme yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa, hivi sasa katika baadhi ya maeneo nchini, mvua za vuli zimeshaanza ingawa bado hazijafikia viwango vya kawaida na mategemeo ya kufikia viwango hivyo pia ni madogo. Katika baadhi ya Mikoa inayoanza kupata mvua za mwaka yaani mvua kubwa, mvua hizo zimeanza kunyesha na zinategemea kuwa za kawaida katika baadhi ya Mikoa ingawaje kutakuwepo na upungufu vile vile katika baadhi ya maeneo katika Mikoa hiyo. Kwetu sisi Watanzania suala lililopo mbele yetu ni kutumia kikamilifu mvua zilizoanza kunyesha katika maeneo yetu. Viongozi na wataalam wanatakiwa sasa kuelekeza nguvu zao kubwa kwa wakulima kwa kusimamia na kutoa ushauri utakaowasaidia wakulima kuandaa mashamba yao mapema na kwamba mazao yanayostahili hali ya upungufu wa mvua na yanayokoma katika muda mfupi yanapandwa.

Aidha, katika maeneo ya mabonde tepetepe na yale yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji hatua zinapasa zichukuliwe kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanatumika kikamilifu. Lipo tatizo linalojitokeza katika baadhi ya skimu za umwagiliaji la usimamizi hafifu na wataalam kutokuwafikia wakulima na kuwasaidia ili mabonde hayo yatumike kikamilifu. Lipo pia tatizo la baadhi ya wakulima wachache wakorofi wasiotaka kuzingatia ushauri wa wataalam. Uongozi wa Mikoa yote yenye mabonde yanayofaa kwa kilimo cha kiangazi na kilimo cha umwagiliaji wanao wajibu wa kulichukulia suala la matumizi mazuri ya mabonde haya kama suala la kufa na kupona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa mafanikio yetu katika kujitosheleza kwa chakula yanategemea pia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa mbegu, Serikali imechukua hatua zinazopasa ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wahisani ili mbegu ziweze kupatikana na kusambazwa katika baadhi ya Mikoa ambayo iliathirika na ukame. Katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2003/2004 Serikali iliamua kutoa ruzuku ya mbolea kwa Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini. Waziri wa Kilimo na Chakula amekwishaelezea juu ya hatua zilizofikiwa na utaratibu utakaotumika kufanikisha zoezi

hili. Ni jukumu sasa la Wizara husika, Mikoa na wafanyabiashara wa mbolea kushirikiana ili wakulima wapate manufaa kama ilivyotarajiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inashughulikia tatizo la upungufu wa chakula katika baadhi ya Mikoa nchini. Hadi sasa jumla ya tani 15,938 zimekwishatolewa kutoka Hifadhi ya Chakula cha Taifa kwa ajili ya Wilaya 58 nchini. Aidha, hadi tarehe 10 Novemba, 2003 Serikali imeshatoa jumla ya takriban shilingi milioni 480 kwa ajili ya kusomba na kukisambaza chakula hicho. Hii ni tofauti na chakula ambacho kinagawa kwa ajili ya biashara. Ni kweli kuwa kuchelewa kwa mvua kutaongeza mahitaji ya chakula katika baadhi ya maeneo.

Kwa kutambua kuwa uwezo wetu wa kukabiliana na hali hii hauwezi kutosheleza mahitaji makubwa yanayojitokeza, Serikali iliwasilisha maombi rasmi kwa wahisani ili kuweza kupata chakula cha nyongeza. Serikali vile vile imechukua hatua za kuondoa kodi kwenye mahindi na mchele ili kuwawezesha wafanyabiashara nao kusaidia katika juhudi zetu za kukabiliana na tatizo hili. Taarifa tulinazo zinaonyesha kuwa wafanyabiashara na wahisani wameitikia vyema wito na maombi ya Serikali na kwamba wapo katika hatua mbalimbali za kukamilisha ahadi zao. Wakuu wa Wilaya kwa kutumia Kamati za Maafa za Wilaya waendeleo kusimamia utoaji wa chakula cha misaada ili kiwafikie walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu napenda kutoa ufafanuzi kuhusu umeme unaoitwa wa bei poa wa Mheshimiwa Mrema, Mwenyekiti wa *TLP*. Suala hili la umeme lisipotoshwe kwa malengo ya kisiasa. Msimamo wa Serikali ni kuwa mtu yeyote au kampuni yoyote inaweza kuleta umeme nchini ili mradi umeme huo hauna madhara kwa afya za wananchi wala mazingira.

Umeme anaouzungumzia Mheshimiwa Mrema na Kampuni yake ya Marekani unatokana na Nguvu za Mionzi ya Jua (*Solar*) au chanzo kingine na upo sehemu nyingi nchini na wala hauna madhara na wala siyo teknolojia mpya. Anaouita *DC* yaani *Direct Current* Mheshimiwa Mrema, ni aina tu ya umeme na siyo chanzo cha umeme. Hata umeme wa gari ni *DC* lakini chanzo ni betri, gharama yake haitokani na kuwa ni umeme wa *DC* bali ni betri na viungio vingine vya umeme. Mheshimiwa Mrema na Kampuni yake wanachotakiwa kufanya, ni kwenda Kituo cha *Tanzania Investment Center* kama ni wawekezaji na *TANESCO* ili kupewa maelekezo yanayohusika na siyo kumzungusha huyo mama katika Ofisi za Mawaziri. Kama ni wafanyabiashara tu (*traders*) taratibu nazo ziko wazi hadi kupata leseni zinazohusika wala huhitaji kuzunguka katika Ofisi za Mawaziri.

Hivyo basi kwa vile taratibu zote zinajulikana, Mheshimiwa Mrema na mgeni wake wanachotakiwa ni kuzifuata, hakuna haja ya kuanzisha malumbano na Serikali na kuanza kutoa tuhuma zisizo za maana wala ukweli dhidi ya Serikali. Wizara ya Nishati na Madini kama wataalam na wahusika walichoelezea tu ni kuwa ni teknolojia inayojulikana na inayotumika duniani na wala siyo rahisi kuliko umeme unaotokana na vyanzo vingine hasa vya maji na hii ni kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imefungua milango ya biashara na haina utaratibu wa kuzuia watu wanaotaka kufanya biashara halali. Tatizo la Mheshimiwa Mrema nadhani ni kuwa alitumbukia katika suala hili bila kuwa hata na ujuzi wa awali wa suala la umeme. Ni vizuri akapata ushauri wa wataalam kabla ya kutumbukia katika masuala ya kitaalam na kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki na hatimaye kutaka kupeleka lawama kwa Serikali. Mimi kwa niaba ya Serikali, ninampa changamoto Mheshimiwa Mrema na Kampuni yake, akafanye niliyoyaelezea tena kwa haraka na alete huo umeme wake wa bei poa ambao haupo popote duniani. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limeweza kukamilisha shughuli zake zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa kumi na tatu kutokana na uongozi wa Mheshimiwa Spika na uongozi wako. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati kwa ushirikiano wenu mkubwa pamoja na uongozi wenu ndani ya Bunge ambao umetuwezesha kutimiza wajibu wetu kikamilifu.

Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Eliachim Simpasa ambaye aliongoza shughuli za Bunge wakati Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti mwenza walipokuwa nje ya nchi kikazi. Aidha, nawashukuru watumishi wote wa Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Kipenka M. Mussa, kwa huduma zao mbalimbali kwa Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru vile vile watumishi wote wa Serikali na wa Mashirika ya Umma kwa kazi yao nzuri iliyoiwezesha Serikali kutekeleza wajibu wake kikamilifu katika vikao vyote vya Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu naomba nivishukuru vyombo vyote vya habari na hususan waandishi wote wa habari waliokuwepo hapa Dodoma kwa muda wote wa Mkutano huu kwa kazi yao nzuri sana. Wananchi wamefaidika sana na huduma zao ambazo zimewawezesha kufuatilia majadiliano na maamuzi yote yaliyofikiwa katika Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa waumini wa dini ya Kiislam nchini wameungana na waumini wenzao duniani kote katika kutimiza moja ya nguzo muhimu ya dini ya Kiislam ya kufunga katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Napenda kutumia fursa hii kuwatakiwa wote mfungo mwema na wenye kheri na matumaini mema. Katika muda mfupi ujao vile vile watasherehekea sikukuu ya *Eid el Fitri* mara baada ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Aidha, Bunge lako Tukufu halitakutana tena hadi mwaka kesho, kipindi ambacho Wakristo nao watakuwa na sikukuu ya Krismasi. Vile vile, tutakuwa tumekwishaaga mwaka wa 2003 na kuukaribisha mwaka mpya wa 2004.

Kwa msingi huo, naomba nitumie fursa hii kutoa salamu zangu za kheri na baraka kwenu Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania wote wakati tutakapokuwa tunasherehekea sikukuu hizi zote nilizozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 3 Februari, 2004, Siku ya Jumanne, Saa Tatu Asubuhi litakapokutana hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji na mimi niwatakie wote *Eid* njema na wale wanaofunga wafunge vizuri, nawatakia Krismasi njema na pia nawatakia na mwaka mpya mwema. Pia niwashukuru kwa ushirikiano wenu wakati niko kwenye kitimoto hapa. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa napenda kuwatangazia ya kwamba baada ya kuahirisha shughuli za Bunge wote tubaki humu ndani, Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Tawala na Wapinzani, kuna taarifa kutoka Ofisi ya Spika nataka kuwaarifu na kutakuwa na matangazo mengine. Kwa hiyo, baada ya kuahirisha naomba mbaki humu ndani.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 11.53 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne  
Tarehe 3 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*